(CKRC)

Verbatim Report Of

# DISSEMINATION OF REPORT & DRAFT BILL,ELDORET SOUTH CONSTITUENCY, HELD AT ELDORET ASK SHOW GROUND.

ON

14TH OCTOBER 2002

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL – ELDORET SOUTH CONSTITUENCY AT ELDORET ASK SHOW GROUND**

**Present:**

| | |
|---|---|
| Chairlady | Com. Salome Muigai |
| Assistant P.O | Dan Juma |
| Verbatim | Asenath Kanga |
| District Co-ordinator | Borr |

The meeting started at 11.15 am

**Borr:** Ningependa mtu wa kujitolea atuongoze na maombi. Ningeomba musimame.

**Prayers:** Mwenyezi Mungu nina shukuru kwa sababu **(inaudible**) Amen

**Borr:** Madam Commissioner, wacha nidelee kwa kusema kati yetu kuna watu wale watatuakilisha katika National Conference. Kuna watu watatu lakini mmoja ndio amefika. Samahani kuna watu watano, watu watatu wamechaguliwa na County Council na watu wawili wamechaguliwa na NGO Council. Kuna wawili sasa nitawapatia nafasi wasitambulishe.

**Julius Kipchebet**: Kwa majina naitwa Julius Kipchebet na nina sema asanti kwa the Commission kwa kuja hapa. Nafikiria hii ni mkutano tutajadiliana na **(inaudible**)

Nafikiria ya kwamba ikifika saa ikifika tarehe tumeambiwa tutakuwa kwa National Conference tulikuwa tumepata report to confirm the procedure kama mnajua.

**Toroei:** Madam Commissioner mimi naitwa Toroei. Mimi nitawakilisha sehemu ya NGO's pamoja na walemavu katika

Constituency na nina furaha ya kwamba katika hii District kuna watu wa tano. Yuko mwenzangu Mrs Biego atakuja pia atawajulisha Civil society na wale wengine wawili pengine tunawajua. Vizuri tujuane hivi hivi ndiyo tuweze kushirikiana kutoa maoni. Nafikiri baadaye tutapata nafasi ili tuweze kusema mengi zaidi. Pahali ninapo kaa ni hapo karibu ukiuliza hapo utanipata lakini siko sababu niko mgonjwa.

**Borr:** Bwana Toroei ni mwalimu wa university, kwa hii university. Tungeuliza Madam Commissioner tungependa unajua ya kwamba kuna viongozi wengine ambao wanahusika kwa kazi ya Katiba, hao ni wanakamati wa Eldoret South Constitutional Committee, tuaomba wasimame na wakuje mbele. Toroitich ndiyo Chairman wa Constituency Committee, kwa hivyo yeye ndiyo atapatia nafasi mwenzake.

**Toroitich:** Madam Commissioner, na wale ambao mumeweza kufika hapa wakati wa leo hamjambo? Hatujambo. Nikiwa mwenye kiti wa Eldoret South kwa mambo ya Katiba ningependa sisi sote tushirikiane pamoja. Kwanza hiyo ni kosi ambaye nilismea.

Lakini ninjua wakati wa leo tuweze kuchagua yule ambao mume sema siku ile ndiyo report iwe mzuri iende Nairobi kwa National Conference. Asante sana.

**Beatrice Cherono:** Kwa majina naitwa Beatrice Cherono mimi na represent (**inaudible)** Location Eldoret South akina mama. Naona kutoka Constituency huo ni mimi peke yangu nilikuja. Tuko wamama wawili ambao tulichaguliwa katika Eldoret South. Asante.

**Ruphas Chege**: Hamjambo nyote? Kwa majina yangu ni Ruphas Kiarie Chege mimi nawakilisha upande wa Timboroa , Kasarafa Location. Asante.

**Stanley Mutai**: Madam Commissioner, washiriki wote, viongozi ambao mumehuthuria asubui ya leo, hamjambo? hamjambo tena?. Naona hii ni siku ya furaha kwa sababu ni sehemu ya kilele ya tatu ambaye tutakuwa tukiendelea kufanya kwa miaka miwili mitatu hivi. Jina langu ni Stanley Mutai. Nimetoka pande ya Geria Cheptiret kazi yangu ni ku-support elimu ya Katiba kwa raia. Na mimi na wapongeza kazi hii kwa sababu matokea tumeyaona kwa kitabu. Kwa umri wangu igawa sijawai kuona nimeona ikianzishwa na ifike mwisho. Asante.

**Micah Rop**: Commissioner na wenzangu wote hamjamboni? Mimi ni Micah Rop na wakilisha upande wa walemavu, upande wa Eldoret South. Asanteni.

**Steven Simato:** Commissioner, viongozi ambaye wamefika na wananchi kwa jumla hajambo? Kwa majina naitwa Steven Simato na wakilisha upande wa Simat Location, kwenye hii team ya Katiba. Asante.

**Samuel Ruto:** Madam Commissioner ushirikishi wa wilaya, mwenyekiti wa Eldoret kusini, wanakamati na wananchi wote,

hamjamb. Kwa majina mimi naitwa Samuel Ruto na wakilisha Tarakwa, Maimuse na Timboroa. Sana mimi ni kati ya kabila ndogo ya wadorobo na ninashukuru sana kwa sababu wakati maoni ilitolewa mulitukumbuka. Asante.

**Borr:** Asanteni sana wanakamati munaweza kuketi. Pia Madam Commissioner ningependa kutambua kwamba kuna baadi ya wale watu ambao tulishirikiana tukiangalia Civic Education na ningependa pia waje mbele wajitambue. Naona Bwana Edwin Baraza wa KCC tafathali kuja mbele. Naona Grace Kuria kutoka kwa ACK, naona Bwana Kimotho from Eldoret trade club naona Bwana Simiyu, is there anybody else ambaye sijataja.

**Edwin Baraza:** Hamjambo yote? Kwa jina naitwa Edwin Baraza Ongeni niko hapa kuwakilisha tume ya haki na amani ya kanisa ya Katholiki katika jimbo la Eldoret. Asanteni.

**Daniel Simato:** Hamjamboni nyote? Mimi naitwa Daniel Simato, mimi ni mwandishi hapa Eldoret, na bado niko kwa hiyo lini ya kufundisha wanafunzi wa District wa (**inaudible)**. Na nilikuwa nafanya mambo ya kufundisha elimu katika mambo ya Kikatiba nafikiri tutasema mengi wakati tutakuwa tukitoa maoni.

**Grace Kuyo**: Nyinyi nyote hamjambo? Kwa majina ni Grace Kuyo tulikuwatnafanya kazi na Constitution Eldoret team, south na north. Na tunafanya na shirika la development awareness programme, tukiwa chini ya kanisa la ACK Eldoret Team.

**Jeremiah Simiyu:** Hamjambo nyote? Kwa majina naitwa Jeremiah Simiyu nikiwa nikitumikia Tume ya haki na amani ya kanisa Katholiki. Mimi ndio nasimamia hii Wilaya ya Wasingishu. Natume kuwa tukishiriki kupeana elimu kwa raia na kweli hapa mukiona maoni yao nafikiri imeonyesha kazi haikuwa mbaya tulijaribu.

**Anne Mumei:** Madam Commissioner na washiriki wote hamjambo? Kwa majina naitwa Anne Mumei kutoka maendeleo ya wanawake. Sisi tumeshirikiana na ofisi ya CKRC katika kutoa Civic Education. Na ninatumaye katika hii Draft Constitution masilai ya kina mama imeangaliwa.

**Borr:** Asante sana. Vile vile kuna mtu moja ambaye atatusaidia katika kutafsiri kwa hii mambo ambayo iko na maswali.

**Solomon Haswai:** Bwana Commissioner na wageni wote hamjambo? Mimi ni Solomon Haswai nimekuwa nikisaidia kwa upande wa kutafsiri kwa hawa watu wale hawajui kizungu. Na kuna mwenzangu pia amekuwa akinisaidia Emmanuel.

**Emmanuel Nyekuri:** Hamjambo wote? Vile mumesikia jina langu na itwa Emmanuel Nyekuri tumekuwa tukifanya kazi hii katika Civic Education Exercise, Asante.

**Borr:** Basi mwisho Madam Commissioner ningependa kutambua the entire clerks ambao tulishirikiana na hao sana wakati wa

seminar ya Councillors na pia wakati wa kuchukua district

**Clerk:** Wananchi wote Hamjambo? Mimi ni katibu wa County Council Tinderet na vile co-ordinator amesema kitu ya sheria County Council is the host secretariat, district co-ordinator ata ingawa ofisi yake haikukuwa ofisi yetu, tunajua mambo yako ni kushirikiana naye vilivyo wakati wa Commission. Ya pili ni vile amesema kwamba atanifilia kutakikana kwa election kwa wale watu wa National Conference kwa njia ambaye inatakikana kwa sheria. Na sisi tunamatumaini makubwa sana, tunafikiri kama tutakuwa hapa tutazungumza juu kwa niaba ya Council yote tunawatakia kazi ambaye itafanywa kazi nzuri na ninawambia kwamba sisi kama Council tunahamu sana hii Katiba, mambo ya hii Katiba ikuishe na hii Katiba turudi tutumie katika Council na katika District. Asanteni sana.

**Com. Salome Muigai:** Hamjambo Mabibi na Mabwana? Kwa niaba ya Tume ya marekebisho ya Katiba ya Kenya, Mwenye kiti yangu Bwana Prof. Yash Pal Ghai na sisi wanatume wenzake ningetaka kuwakaribisha sana kwenye hii kikao cha kuangalia hii Katiba inavyo sema tumetengeneza pamoja. Ningeanza kwanza pengine kuwajulisha wenzangu wenye nimekuja nao kutoka ofisini. Pande wangu wa kulia kuna mama Asenath Kanga ambaye atakuwa akitufanyia kushika habari yetu moja kwa moja kwa hivyo ningeomba kelele tupunguze ndiyo akishika maneno ile atashika iwe tu ni maneno ya mkutano peke yake. Upande wangu wa kushoto ninaye Bwana Juma Programme Officer kutoka ofisini kwetu. Naye ndie ofisi ya PLO ya Limumba, yeye ndio Limumba wa hapa, kwa wajibu wa kikao hiki chetu cha leo. Mimi mwenyewe majina yangu ni Salome Wairimu Muigai. Nafurahi kuja Uwasingishu kwani mimi mwenyewe ni mzaliwa wa hapa. Nilisoma Township primary school. Baba yangu anakaa Kamkunji, kwa hivyo huku ninajiskia niko nyumbani kabisa. Leo mimi ni mtembea kwao. Asante. Leo mimi ni mtembea kwao na waswahili usema mtembea kwao hufanywa nini? Atatulipofika kwenye club jana wakaniambia hawana nafasi pale wanamkutano, niliwaeleza nikienda Kitale wakiniambia hawana nafasi nitawasikiza, nikienda Nandi District niambiwe hakuna nafasi nitafanya nini? Nitasikiza kwani mimi ni mgeni. Lakini hapa ni kwetu na lazima nipatiwe mahali pa kulala. Na mwishowe kweli walinipa, kwa hivyo nafurahi sana kuwa hapa kwani hapa niko nyumbani kabisa.

Sasa ningetaka kurudia kitu fupi kati yetu kama wanatume. Tulichagua Tume ya watu 29 kama vile munavyo jua, mwishoni tulipoteza moja wetu alikekuwa ndio Naibu wa Mwenye Kiti. Na pia tukapata mtu mwingine wa kurudi pahali pake. Kwa hivyo baado tuko Wanatume 29. Na kazi yetu ilikuwa kuja kuchukua maoni yenu. Halafu tukishayachukua tuende tuyaweke pamoja na tuyafikirie na tuifakari ili tutoe mswaada wa Katiba ya mageuzi ya Katiba yetu. Na hiyo kazi tumeshafanya. Na leo baada ya kufanya hivyo kabla hatujafanya mswaada tulifanya dimoki sijui kama wengi wenu waliona report tuliowega kwa gazetti ilioitwa chaguo la wananchi. Muliiona? Tuliweka kwa magazetti ili watumie ama people’s choice. Tuliweka kwa kiswahili na tukaweka kwa kingereza. Baada ya hiyo tulienda Mombasa na kukaa kwa karibu mwezi mzima tukifikiria wananchi wameleza nini. Hii haikukuwa kazi rahisi wala haikukuwa kazi ndogo. Kwani tulienda kwa vikao vya mbunge. Na tuna vikao vingapi inchini? Tuna vikau vingapi vya bunge? Constituency zetu ni gapi? 210. Kwa hivyo tulikaa kwenye hizo vikao 210 kwa siku moja, siku mbili na kwengine pahali ilikuwa kubwa ama geography ilikuwa shida sana watu wote kukutana pamoja tulikaa siku tatu. Tulienda mahali kama Rongo wakati tulienda Tarakwe. Tukaenda Kapsowar one, tukenda pahali

pengi, tukaenda kukutana na wananchi. Tuelienda Mandela, tukaenda Wajir, tukeanda Lamu, tukaenda Mombasa, tukaenda Nanyuki, tukaenda Nyeri, takaenda Laikipia, tukaenda Muranga. Kwote tulienda Siaya na tukaenda Kakamega, na tukaenda Keiyo district. Tulienda Mount Elgon, na tukaenda Loitoktok. Kwa hivyo hii habari kuikaliachini na kuzugumza na kuzugumza na kuzungumza ili ikawa report ndogo kama hii iliyo report, ile tunaita report fupi ilikuwa kazi kubwa lakini imefanyika.

Ningetaka kueleza kuwa hii repoti tunaita report fupi kwani kuna ile repoti itakaye kuwa ndefu yenye itakuwa na volume tatu. Hiyo volume tatu inaeleza kila pahali tulipoenda vile tuliambiwa. Pia tulitaja report nyingine ya kila kikao cha bunge. Tulipokuja Eldoret South tuliambiwa nini? Yale mambo yote yenye mulituambia tumeikusanya pamoja naiko kwa repoti moja inaiyo itwa Eldoret South Constituency, Rift Valley Province. Habari zenu zote ziko kwenye hii repoti fupi ya Eldoret South peke yake. Kesho ukitaka kuangalia kama maoni yako yalibookiwa, yameabukizwa, yameangaliwa tafadhali ukienda kwa ofisi yetu ya kuenda board utaikuta repoti kule. Utaikuta repoti fupi yenye kueleza habari ya nchi nzima huko na pia utakuta huu mswaada wenye tumeshatayarisha.

Leo ningetaka kueleza kazi yetu. Leo kazi yetu ni kazi fupi. Nikuangalia mswaada wa Katiba yenye tumeletewa unasema nini? Na kueleza kama vile tunavyoelewa kitu kama Wanatume na pia nikisha maliza kwani mimi mwenyewe ndio nitaeleza hayo nitawaomba munieleze nyinyi munaelewa vipi ama tafshishi iko wapi? Ama ni jambo gani mungetaka ufafanuliwe zaidi. Tukimaliza hayo tutaelezana hapo tutakapoanza. Tutakapo toka tutaelewana. Ndio kazi yangu ni rahisi kidogo, wakati tulipokuwa Trans Nzoia repoti ilikuwa haijatoka kwa kiswahili kwa hivyo tulikuwa tukifanya tafsiri, tukiendelea. Lakini leo wale wenye walikuwa barasa ya weekend, ya jana walipata lakili ya Constitution kwa kiswahili. Kwa hivyo kazi yangu leo itakuwa rahisi kidogo. Kwa hivyo kazi yangu nikuwaeleza huu Mswaada unasema nini. Nakama mukinikubalisha nitaanza. Ninaweza kuanza?

**Wananchi:** Ndio.

**Com. Salome Muigai:** Okay. Na nyiyi pia munaweza kaa na nakala zenu lakini mjaadala nyingi zimeelezwa kwa kingereza. Lakini mimi ningetaka kuzungumzia kwa Kiswahili ama mungetaka nizungumuze kwa Kingereza? Kwa Kiswahili. Leo atatulifanya bidii tumetengeneza kakaratasi kidogo ambavyo ya chapter ya ulemavu, tumentengeneza hata kwa kirefu sababu nilijua nikija Eldoret bila brief utaonana Samwel Tororei Kwa hivyo tumefanya bidii tukahakikisha kuwa tumetengeneza brief. Lakini nami ningetaka uelewe kwamba ni habari tu ya ulemavu tumetengeneza kwa kirefu. Kwa hivyo mambo mengi yenye nitazungumuzia itakuwa haiko kwa kirefu. Lakini bado iko kwa Katiba AP3. Wanaitengeneza ile ya tuna tulianza tuna fahari hapo ili ujue kuwa tuna masilahi ya walemavu katika Tume.

Sasa tuangalie ukurasa wa pili wa Constitution yenye muko nayo. Kwanza tulipotembea watu wengi walitueleza kuwa Katiba yetu ya leo haina utangulizi. Na tukambiwa maneno mengi yenye watu wangetaka kuona katika huo utangulizi. Natulipo yachuja sisi wenyewe tumekuja tumeanza na hii utangulizi.

Sisi wananchi wa Kenya tukifahamu witu wa tumaini zetu za kikabila na za nini tena. Mimi ni mwalimu kwa hivyo nimezoea kuzungumuza na watu. Sio mimi nisimame miseme nikihubiri. Kwa hivyo sijazoeya kuzungumza mimi peke yangu, tutazungumza wote pamoja. Kwa hivyo tuanze mimi nimeanza nikasema kwa utangulizi.

**Com. Salome Muigai:** Preamble inasema, sisi wananchi wa Kenya , tukifahamu wingi wa tafauti zetu za kikabila, na za nini tena?

**Audience:** za kitamaduni

**Com. Salome Muigai:** Na nini tena?

**Audience:** Na kidini

**Com. Salome Muigai:** Na tukithanilia kuishi kwa Amani na nini?

**Audience:** na Umoja

**Com. Salome Muigai:** Kama nani?

**Audience:** Kama Taifa moja, huru, kwa kufanya nini?

**Com. Salome Muigai:** Kwa kutanganyika, tukijitolea kulea na kulinda nini?

**Audience:** Masilahi ya kila mmoja.

**Com. Salome Muigai:** Wewe utatolea kwa kiswahili wengine wa ethics, We are trying to translate that Preamble so that we come to a common understanding. Tunajaribu kuiangalia hiyo Preamble tukijitolea kulea na kulinda masilahi ya kila msoja, ya familia na ya dini katika taifa letu. Tukitambua matumaini ya nani?

**Audience:** Ya wanawake

**Com. Salome Muigai:** Na nani mwingine?

**Audience:** na wanaume

**Com. Salome Muigai:** na wanaume wetu ya kuwa na Serikali ambayo imejengwa katika msingi muhimu inayo thamini nini?

**Audience:** nguvu

**Com. Salome Muigai:** na nini tena?

**Audience:** Demokrasia

**Com. Salome Muigai:** Demokrasia na nini tena?

**Audience:** haki ya kijamii

**Com. Salome Muigai:** haki ya kijamii na pia tutii jamii. Utawala wa sheria, hiyo ndio point two. Na tukitekeleza haki yetu isiotengeka ya uhuru ili kuamua aina ya utawala wa inchi yetu na tukiwa tumeshiriki kikamilifu katika utaratibu wa kufanya nini?

**Audience:** wakuadaa Katiba.

**Com. Salome Muigai:** Wakuadaa Katiba. Mumeshiriki kwa kuaada Katiba hii?

**Audience:** Ndio

**Com. Salome Muigai:** Mumeshiriki

**Audience:** ndio

**Com. Salome Muigai:** Okay, tumekubali hii Katiba tunaifanya sheria na tunaitoa kwetu wenyewe kufika kwa vizazi vietu vijavio Katiba hii. Yani tunaikubali, tunajipatia sisi wenyewe sio Katiba yenye mtu anatuletea na kutupa sisi. Mwenye kutupatia ni nani?

**Audience:** Sisi wenyewe.

**Com. Salome Muigai:** Natunampatia nani?

**Audience:** tunajipatia

**Com. Salome Muigai:** tunajipatia sisi, na tunasema Mungu afanye nini?

**Audience:** Mungu ibariki Kenya

**Com. Salome Muigai:** Sasa hiyo ndiyo utangulizi wetu. Na hiyo utangulizi unatoa thamana zetu, our value. Value zetu ni nyingi kwenye hiyo utangulizi tutaziona tukiandamana kwenye Katiba sura kwa sura. Hii Katiba mpya inasura ishirini. Sura ya kwanza inazungumzia juu ya uhuru wa wananchi na ukuu wa Katiba. Uhuru ni sovereignty sijui kama ili neno linatolea maana. Sovereignty of the people. Yani ukuu pia wawatu sio uhuru tu, ni ya mtu ni ya uhuru wa mtu anayejitawala mwenyewe. The sovereignty of the people, ukuu wa watu na ukuu wa Katiba. The supremacy of the Constitution. Tunasema uhuru wa Katiba ama sovereignty ya uhuru wote wa kitaifa umetoka kwa nani?

**Audience:** kwa wananchi.

**Com. Salome Muigai:** Yani uhuru wa kila mtu ama kila institution. Institution inaitwa nini?

**Audience:** tafshishi

**Com. Salome Muigai:** Kila tafshishi imepata uhuru wake na imepata mamlaka yake kutoke kwa nani?

**Audience:** wananchi

**Com. Salome Muigai:** wananchi, kwa hivyo mwananchi ndio mwenye mamlaka ya mwisho. Ndio mwenye mamlaka ya kujitawala yeye mwenyewe ama ya kupangia tafshishi yoyote ama mtu yoyote hayo mamlaka yake ili amtawale. Tunazumzia pia ukuu wa Katiba. Kuwa mambo yote itafanyika kwenye hii taifa iko chini ya nini?

**Audience:** ya Katiba

**Com. Salome Muigai:** Hakuna mtu alieye juu ya Katiba na hakuna tafshishi yenye tutatengeneza yenye itakuwa juu ya nini?

**Audience:** ya Katiba

**Com. Salome Muigai:** Tunazumgumzia pia kwenye hiyo sura juu ya ulinzi wa Katiba. Je Katiba itahitaji kulindwa?

**Audience:** ndio

**Com. Salome Muigai:** naitalindwa na nani?

**Audience:** na sisi wenyewe

**Com. Salome Muigai:** Na sisi wenyewe, kama ni Katiba yetu lazima tuilinde sisi wenyewe. Pia inazungumzia sheria za Kenya. Sheria za Kenya nauliza zitatoka wapi? Sheria ya kwanza ya Kenya itatoka kwenye nini?

**Audience:** kwenye Katiba yenyewe.

**Com. Salome Muigai:** Kwenye katiba yenyewe, sivyo

**Audience:**

**Com. Salome Muigai:** Kutakuwa na sheria yenye imetungwa na Katiba. Tutakuwa pia na sheria yenye imefanya nini? Ukiangalia ukurasa, ukurasa wa ngapi? Ukiangalia kwenye gazetti lako kwenye ukurasa wa nne utaona pahali sheria za Kenya zimeelezwa kwa kirefu. Kwa hivyo tumesema sheria ya kwanza itatoka kwa Katiba. Sheria pia zitatoka kwa bunge. Bunge ndiyo itaunda nini? Sheria zake. Sheria zingine zitatoka wapi?

**Audience:** **(inaudible)**

**Com. Salome Muigai:** Thamani zetu pia zitatupa ni ? sheria zingine. Na zingine?

**Audience:** Jumuia ya Africa ya mashairiki

**Com. Salome Muigai:** Kwa jumuia ya Africa ya mashariki, sababu gani? Sababu sisi tumeungana kuwa shirika la Africa Mashariki. Tumeipa bunge, na hiyo bunge pia italeta nini? Sheria zingine. Kwa hivyo sisi kama wana Kenya tutahitaji tufuate

sheria zatakapo undwa pale. Na nini mwingine atatupa sheria?

**Audience**: (**inaudible)**

**Com. Salome Muigai:** Sheria za kimataifa pia. Kwani sisi ni wanachama ya jumuia ya madola, kwa hivyo hatuwezi kujitenga. Kwa hivyo mataifa yote ya kikubaliana kuwa kuna sheria hii na sisi wenyewe itatubidi kufanya nini hiyo sheria?

**Audience:** (**inaudible**)

**Com. Salome Muigai:** Kama ingekuwa wakati ile nilikuwa mwalimu nigeambia darasa ikimbie ishike gate halafu turudi. Lakini leo siwezi. Kwa hivyo tafathali mungenijibu bila kukimbia kushika gate. Amamungependa kukimbia mushike gate. Na hatuna St Johns Ambulance hapa wenda tukaenda hasara kubwa. So, please can we be able to interact. Tunzugumzie hii Katiba yetu tukiwa pamoja. Basi hiyo ni mpango tu ya pahali gani tutatoa sheria zetu. Na ndiyo imeelezwa kwenye kitengele cha sura ya kwanza, kitengele cha tano. Tuendelea kwenye sura ya pili.Sura ya pili inazugumzia Kenya yetu kuwa nini?

**Audience:** (**inaudible)**

**Com. Salome Muigai:** kuwa jamhuri. Kipande cha sita kinaitangaza kuwa Kenya ni jamhuri. Cha saba kinaeleza ineo letu ni mpaka wapi, tunamipaka na nani, na hiyo mipaka imefika wapi? Kitengele cha nane kinaelezea makao yetu makuu na wakati huu makao yetu makuu iko wapi?

**Audience: (inaudible)**

**Com. Salome Muigai:** Nairobi. Lakini ukisoma zaidi utaelezwa kuwa kwenye Katiba mpya tumesema kuwa Serikali itajitahidi kuona kuwa wizara tafauti zinakaa katika makao tafauti katika nchi ya Kenya. Ikiwa ni wizara ya kilimo, hamna haja ya kuipeleka North Eastern Province kwani huko hakuna kilimo kingisio. Kwa hivyo itaenda ipelekwe kwa kule kimependa nacho. Kutaka ipelekwe pahali itahitajika zaidi. Halafu tunazungumzia habari ya lugha. Lugha zetu za kirasmi, tunasema ni lugha mbili, lugha vipi hizo?

**Audience:** Kiswahili na kingereza.

**Com. Salome Muigai:** Na lugha yetu ya kitaifa tunasema ni moja na hiyo ni gani?

**Audience:** ni Kiswahili

**Com. Salome Muigai:** Basi na hiyo tunasema kuwa itakuwa jukumu ya Serikali kujaribu iwezavyo kuwekeya manani lugha zetu za kimsingi. Na kujaribu kuendeleza lugha ya Kiswahili na lugha zetu za kimsingi na zaidi ya hapo tumeongezea lugha mbili. Kuwa tutaendeza sana lugha ya ishara ama sign language na pia maandishi ya zera ili kila mtu afundishwe. Ndiyo hiyo yenye fahid leo anatuonyesha. Tumezungumzia pia habari ya taifa na dini. Tuliposema kuwa Kenya sio taifa la kidini yani sisi hatuna dini yeyote tunaweza sema hii ndiyo dini ya Taifa. Lakini Kenya kama taifa itatambua kila dini na itawekea kila dini mamlaka sawa. Hakuna dini yenye itakuwa na mamlaka kubwa kuliko nini?

**Audience:** nyingine

**Com. Salome Muigai:** Lakini mrathi tu, wenye dini pia wafuate Katiba yetu. Pale kwenye tulizungumzia habari ya sheria zetu zitatoka wapi, kulikuwa pia sheria ya dini ya Kislaam. Lakini hiyo dini ya Kislaam tutaitia manani kwa jambo moja tu kwa initital hii ya kibinafasi., personal law. Mtu akitaka kuowa anaweza kuowa kisalaam, pia akitaka kuo kikatholiki hajakatazwa, mtu akitaka kwenda kwa sadaka kwa dini ya kislaam atakubaliwa. Urithi, kuolewa na mambo nyingine ya kibinafsi. Lakini mtu akiuwa ama akiiba wakati huo hujaikosea dini, hujakosea kabila lako, haujaikosea dini yako, umekosea nani?

**Audience:** Taifa

**Com. Salome Muigai:** Ndiyo hata mtu akikuibie ukienda ukimstaki wakati wa kuenda kotini wewe huendi kama mlalamishi, unaenda kama nani?

**Audience:** shahidi

**Com. Salome Muigai:** shahidi, wewe ni shahidi wa nani?

**Audience:** wa Taifa.

**Com. Salome Muigai:** Tunaelewa, kwa hivyo ile mambo yote yenye ni criminal law itaenda kwa Taifa. Hii dini ya tutazungumzia siada kwa mwaada tukija habari ya mahakama, habari ya inchi ya kislaam na koti zao. Halafu tunazungumzia habari ya alama zetu za Taifa. Ili Taifa letu kama tumesema ni Jamhuri, Jamhuri itakuwa na alama zake, na alama zake zitakuwa zina nini? Nini yenye itakuwa alama ya Taifa?

**Audience:** Bendera

**Com. Salome Muigai:** nini tena?

**Audience:** Wimbo wa Taifa

**Com. Salome Muigai:** na nini tena?

**Audience:** Court of Arms

**Com. Salome Muigai:** Court of Arms, na hiyo Court of Arms inaitwa nani? Nani mwenye gazetti la Kiswahili?

**Audience:**

**Com. Salome Muigai:** page 4, ebu taumbie hiyo ishara la Taifa ni nini moja? Kuna mtu mwenye amezungumza lakini hakusema kwa sauti kubwa. Ni nini?

**Audience:** ni mimi

**Com. Salome Muigai:** Nembo, nembo ni crowni, yenye tulikuwa tukiita crowni sasa tumeanza kugusa lugha yetu ya Taifa na tumejifunza neno mpya kwa wengi wetu. Lenye ni nembo. Na nini tena? Ishara zetu za Taifa?

**Audience:** Mhuri wa Taifa

**Com. Salome Muigai:** Mhuri wa Taifa pia. That is our shield. Ndiyo kitu ikikuwa na hiyo mhuri tunajua hiyo ni kitu rasmai kilicho toka kwa Taifa letu ama kwa Serikali yetu. Pia kwenye hiyo tume ya Jamhuri tutafikiria pia haki yako ya kitaifa na matamko ya haki. Yaani what are those in English?

**Audience:**

**Com. Salome Muigai:** National oath and apervasion. Kwa hivyo yule kiongozi mwenye tutapata awe ni wakiwango kipi tutamuapisha. Kwa hivyo ile kiapo yenye tutatumia kumuapisha pia tumeweka kwenye Katiba ili ifuatane kila pahali. Na mwisho wake tuna jambo lenye bado tutazungumziwa na ndugu zetu za kitaifa. Wakati huo tumeweka siku mbili, tumeweka 1st June siku ya Madaraka na pia tumeweka 12th December, Jamhuri. Na tumependekeza kuwa kutakuwa siku ya Katiba. Watu wengi wanatuuliza sababu gani tumetoa siku ya Kenyatta day, na mumeondolea siku ya Moi day. Tumekubaliana kuwa kwenye hii Katiba wananchi wametuambia kuwa wagetaka Rais akae kwenye muda gani? Urambo ngapi?

**Audience:** miwili

**Com. Salome Muigai:** Miwira miwili kila mmoja miaka migapi?

**Audience:** mi tano

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo kukifanyika hivyo katika siasa arubaine ingine ijazo tutakuwa tumekuwa Rais wangapi?

**Audience:** wanne

**Com. Salome Muigai:** Wanne, akiwa atamaliza miwira miwili. Munajua mwaweza kuwa na kura mmoja akakosa kuchaguliwa kwa hivyo uenda ikakuwa wainne ama wawe wangapi?

**Audience:** wanane

**Com. Salome Muigai:** Wanane, Mungu akitujalia tukiwa na historia ndefu kama America walio na historia ya miaka mia mbili tutakuwa tumekuwa na Rais wangapi?

**Audience:** Ishirini

**Com. Salome Muigai:** Ishirini ama ngapi?

**Audience:** aubaini

**Com. Salome Muigai:** Ama arubaini. Kilia mmoja tukimpa siku yake tutakuwa tukifanya kazi siku ngapi basi watu wa

Kenya. Tutakuwa tungoja tu holiday moja baada ya nyingine. Lakini ni jambo la kufikiriwa sio kusema tumeangalia hivi na tukasema basi ndiyo hiyo. Tumesema lakini bado hatujaandika na mawe. Kwa hivyo tunaweza kufuta. Lakini tunataka wananchi wafikirie hii habari kwa that ilikuwa ni their identification za kila Rais wetu siku yake. Sasa hiyo tumemaliza sura ya pili tuende kwa sura ya tatu.

Malengo ya Taifa na Madhiri ya Kanuni. Our principles, our National goal, Value and Principles. Na hiyo ina mambo mengi yenye tumeleta. Tunasema kuwa malengo ya Taifa na madhiri na kanuni zilizoko katika sura hii zinahusu mamlaka ya nchi, bunge, mahakama, tawala za wilayani, na vyombo vingine vya Serikali na viongozi. Raia na viongozi na miungano ya kibinafsi pale aambapo chombo kimoja wapo kwanza au kinatumia na kuifafanua Katiba au Sheria zinginezo.

Pili, kinatumia, kinaunda au kinatekeleza mauruthi ya feather, policy. Jamhuri itakuza umoja wa kitaifa na kuendeleza haki ya kujitolea kuangalia wake wauzito wa Utaifa. Yani this value, sometimes Kiswahili inakuwa ngumu kuliko Kingereza, sivo? Sisi wengine tuaelewa goal, value na principles kuliko vile tunaelewa malengo, madili ya kanuni na zera, sivo? Nitakuwa nikitumia kingereza na kiswahili mchanganyiko.

What we are saying here is this, that whatever organization whether it is the Parliament, whether it is the Institute Government, whichever organization is going to be in a position to interpret the Constitution they must follow this values, they must follow this National goals, they must recognise this values. Do we understand that?

Tunasema kuwa hizi thamana zetu, sijui thamana tunaziita nini kwa Kiswahili, kitamaduni cha kiafrica. Hii malengo yetu, pahali Kenya inataka kwenda, pahali tumelenga, thamana zetu ni kitu chenye unaweka kanuni. Thamana ni kitu cha muhimu sivyo? Si thamana ni kitu chenye tunawekelea mtu muhimu? Kila mtu mwenye atakuwa kiongozi kama ni kiongozi wa bunge, kama ni kiongozi wa wilaya, kama ni uokozi wa kikundi cha watu binafsi nina jua awekee mananai haya majirio, haya matumaini yetu.

Na la kwanza ni kusema kuwa, Jamhuri itakuza umoja wa kila nyumbani. Yani sisi kama wanakenya tutakuwa Mataifa mangapi?

**Audience:**

**Com. Salome Muigai:** Tutakuwa Taifa moja ndiyo thamana yetu ya kwanza. We are one people as a Nation. We are one Nation. Pia Jamhuri itatambua wengi wa tafauti za wananchi wake na kukuza tamaduni za jamii zake. Ingawa tu Taifa moja, pia tunatambua kuwa sisi ni makabila tafauti. Sisi tuna dini tafauti, sisi tunauwezo tafauti, wengine wanaulemavu, wengine hawana, wengine ni wake wengine ni wanaume. Lakini baado tutachagua vitu tofauti na tuwe zaidi ya kuwa ni sisi tunaishi tafauti pia sisi ni watu wa Taifa moja. Tunaelewa hivi?We are one Nation but we recognize our diversity. Hizo ni thamana zetu.

Ya inne inasema Jamhuri imejengwa katika misingi ya kanuni za kidemokrasia na itaendelesha ushirika wa wananchi katika

maswala ya kitaifa na kufanikisha ugawaji na ugusaji na utangazaji wa madaraka. Kuwa mutakubali ni Taifa moja, tunakubali makabila na vitu vingine tofauti pia tunakubali kuwa ugawanyaji wa maendeleo na kila kitu utafanywa kisawa. Bali na tafauti zetu tutagawanyiwa usawa kinachotuhusu. Hayo mathamana ni nyingi, zimeendelea mpaka mktasari kumi na nane. Na sitazisoma zote lakini nigetaka kila mtu aweze kuzisoma. Lakini kabla sijamaliza kusoma ningetaka kusoma ya kumi na moja.

Jamhuri itahakikisha kushiriki kikamilifu, kwa wanawake, walemavu. Jamii zilizowekwa pembeni na sekta ya jamii katika maisha ya nchi katika mikasa ya kijamii na kiuchumi. We are bond as a Republic to take on board everybody. Tutahakikisha kuwa kina mama wahusishwa, watu waliona ulemavu wamehusishwa, wale jamii kama dorobo wenye tusema Ibrania …. Wao dorobo, Ogiek, huu ni wakati wetu wa kutafuta kuwa. Jamii zetu wako wapi? Nani alisahaulika jana? Na kama alisahaulika jana tutaweka bimu gani ili wakati huu afanye nini asisahaulike? Kwa hivyo niwako mpya.

Na ya kumi na mbili, Serikali itatekeleza kanuni kuwa ugumvi moja ya wanachama wa vyombo vyote vinavyo fanyiwa uchaguzi na uteuzi ni kina nani?

**Audience: (inaudible)**

**Com. Salome Muigai:** Ni wanawake, 1/3 ya kila pahali penye kutakuwa na uchaguzi, ukiwa wewe uko kanisani na unafanya kwa ofisi ya Katiba na nyingi ni Wakenya lazima mtakubaliana na Katiba ya nini? Ya Kenya. Na mtatafuta kiwango kipi cha kina mama kuhusika?

**Audience: (inaudible)**

**Com. Salome Muigai:** 1/3, hiyo ni nyingi sana? Kina mama ni wangapi kwa nchi?

**Audience: (inaudible)**

**Com. Salome Muigai:** 51%, kwa hivyo ni zaidi ya nusu. Na hao kina mama wanauliza wawekewe kiti yao. Wanauliza hiyo nusu? Wanaomba nini? 1/3, si kina mama ata hao wemejinyima? Nitasoma kipengele kingine kimoja juu ya hii mjadala wetu halafu nitaendelea kwa jambo lingine.

Number kumi na tatu, ina sema hivi, Jamhuri itatambua majikumu maalum ambayo taifa, jamii na wazazi wajao kwa watoto wetu, na itahakikisha kuwatingizia mahitaji yao ya nini? Mahitaji ya nini? Ya hali na mali. Mahitaji ya kina nani hiyo yenye tunazungumzia wakati huu?

**Audience: (inaudible)**

**Com. Salome Muigai:** Mahitaji ya watoto. Tutahakikisha kuwa tumetimiza mahitaji ya watoto ya hali na mali. Haitoshelezi kuwa tutapatia watoto kitu fulani kama tumewapa chakula, tume wapa elimu, tumewapa mavazi, itatuhitaji pia kuhakikisha kuwa haki yao ni hali yenye inaletea manani na pahali mzuri yakukua. That is one of our values, that is one of our principles.

That is one of one of our National, National what? Goal. Sasa tunazungumzia hali ya hiyo kwenye gazetti tafathali tafuta nafasi ukasome mwenyewe ukiwa na swali turudie.

Tutazungumzia pia wajibu wa Raia. Kama wewe ni mraia wa Kenya je unawajibu wowote? Na kitengele cha kumi na tano, page 5, kinatueleza jukumu za raia. Wewe ukiwa ni raia wa Kenya unajukumu fulani. Na kanuni za jukumu hizi ni kusema kila mwanakenya anahaki sawa ya kupata haki za zile kawaida ya uraia. Ukiwa wewe ni Mwanakenya una haki sawa na yule mwingine yeyote kupata nini? Sorry mimerudia tena kwa uraia kwanza.

Ili kutimiza malengo ya kitaifa yenye tumefikiria na madiri na kanuni, raia wote wanawajibu fulani. Wajibu wa kwanza kuna jamii. Wajibu wa kwanza wako kama raia wa Kenya ni kujifahamisha kuhusu masharti ya Katiba na kudumisha mathiri ya malego yake. Wewe mwenyewe unajuhudi ya kufanya nini? Ya kujifahamisha na zaidi ya kujifahamisha ufanye nini?
**Audience:** udumishe

**Com. Salome Muigai:** Udumishe. You have a duty to do what? Look at page 5, you don't need to remember just read it. Page 5 number 15.
**Audience:** (**inaudible)**

**Com. Salome Muigai:** But we don't start by propagating. We don't proper gate what we don't know. You start by doing what? You start by acquinting yourself. Lazima ujifundishe kwanza na ujue ndiyo uweze kufanya nini? Kufundisha mwingine.

Inasema aje kwa kingereza. Uphold and protect. Lazima wewe mwenyewe uidumishe baada ya kuidumisha lazima ufanye nini, uitetee. Uitetee Katiba yako. Leo asubuhi mahali nilikuwa nikikaa, mtu moja simu yake ya mkono ililia, na mahali tulikuwa hatukubalishwi kuzungumza kwa simu ya mkono. Akambiwa, there are many people with that sasa kwa nini unatuwekea mambo hapa kwenye board na ugonjwa wa mambo tumesikia. At least wawili waone mmoja…..**interjection**

**Borr:** Tafadthali tuchukue watu wawili wawili mmoja. Gazetti moja kwa watu wawili maana hatuna ya kuzunguka kwa kila mtu. Tafadhali peana kwa watu wawili wawili.

**Com. Salome Muigai:** Tafadhali mupe huyo mama moja angalie kama atapata affirmative action. Mama mwenye ashika mtoto na ku… shuka ya kushika mtoto. Okay can we go back to our meeting, tungerudia mkutano wetu tafadhali. Asante. Nilikuwa nikieleza juu ya kisa niliona. Niliona mtu ameambiwa mahali tuko asizugumze na simu ya mkono. Simu yake ikalia akazugumza kama dakika sita. Halafu akambiwa tafdhali hapa hatukubalishi kuzungumza kwa simu, akaendelea tu kama mwenye hakusikia. Akamaliza mjumbe akafikiwa, walikuwa watu fulani. Alipoamka kuzungumza mimi nilisikia nimehudumishwa na hiyo habari, I was angry**.** Nilimwangalia tu kwa macho, halafu akaondoka yeye mwenyewe akaenda

kuzungumzia nje. Lakini kumaliza kuja aliendа tukamuwambia huyu wa pili hatufalishanga kwa uliamka ukenda kuzungumzia nje halafu urudi. kwani wakati munavunja sheria zetu. Wakati munavunja sheria zetu na pia umenuvuwa sheria zangu mimi mwenyewe. mukija kwa nchi yetu ya kuvunja sheria zetu na mujue umevunja sheria zako wewe mwenyewe. Kwa hivyo ni sheria za nani?

**Audience:** zetu

**Com. Salome Muigai:** zetu, sheria za zangu. Sikumzungumzia yule mwenye alikataa lakini the message was very very clear, akawa ameanza kuabika na kuangalia chini. Munafikiria kesho atazungumza ni hizo kitu kwa public, no, kwani nilitetea nini? Sheria zetu. Kwa hivyo kila mmoja wetu ni lazima tufikirie kutetea Katiba yetu.

Ya pili, kutekeleza haki yao ya kidemokrasia kwa kupiga kura na kushiriki katika namna ingine ya shuguli za siasa. Kwa hivyo ni wajibu wa kila Mkenya kupiga kura. Unaelewa? It is not only a right it is also a responsibility kwa kila Mkenya kupiga kura. Na pia kufundisha vilivyo kwenye namna mbali mbali za siasa. Kwani siasa uleta nini? Politics bring what? It is politics that brings what? Polisies isn't it? Our polisies come from the politics. Is there anybody who is not touched by polisies. Polisies ni kama nini? Kuna wizara ya nini? Kuna wizara ya kilimo, politics and Agriculture, na nini?

**Audience:** ya elimu

**Com. Salome Muigai:** Kuna zera ya elimu, we support education policy people. Kuna wizara ya afya tumepewa usiano kati ya siasa na zira, the relationship between policy and politics. Is there anybody who is not touched by a policy of one sought or the other? Is there anybody who is not touched by the policy of agriculture? Ata mimi mwenye sio mkulima mimi ni nini? Kama mimi ni silimi ninahusishwa vipi na zera ya kilimo?

**Audience: silent**

**Com. Salome Muigai:** mimi nakula, sivyo?

**Audience:** ndiyo

**Com. Salome Muigai:** Mkulima asiokuwa na zera nzuri za kuwezesha kutayarisha chakula. Mimi nitapata wapi chakula? Sinimekosa? Kwa hivyo zera ya kilimo inatuhusu nini? Na pesa ya kilimo inatoka wapi?

**Audience:** kwa siasa

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo kila mkulima usiomkulima wewe ni mwanasiasa. Ukiwa mtu mwenye kuza wewe pia ni mwenye siasa. Hakuna siasa kubwa kuliko ya tumbo. Kitu muhimu sio vile tumeelewa siasa ya tumbo katika nchi yetu. Kwa hivyo ni vizuri kuona ushirikiano ulioko katika siasa na feather. The relationship between politics and polisies. Kwa hivyo tukiwa na siasa nzuri tutakuwa na kura zipi?

**Audience:** nzuri

**Com. Salome Muigai:** kura nzuri. Na sisi kila moja lazima ajishuhusishe ili tuweze kuona wizara zenye tumepata ni nzuri na zinatusaidia kila moja.

Jambo legine la jukumu ya Mwanakenya ni kushiriki katika kazi. Kila Mwanakenya ana jukumu ya kufanya nini?

**Audience:**

**Com. Salome Muigai:** ya kufanya kazi. Kazi yote ata kazi ya kufanya jamii. Pia watakuwa wameichagua kama kazi. Lakini kila mmoja lazima ajishuhulishe kwenye kazi ili aweze kuhudumia nini? Yeye mwenyewe, na nani mwingine?

**Audience:**

**Com. Salome Muigai:** familia yake, na nani mwingine?

**Audience:** Jamii

**Com. Salome Muigai:** na mwishowe ni nini?

**Audience:**

**Com. Salome Muigai:**

**Audience:**

**Com. Salome Muigai:** Taifa nzima. Msipofanya kazi, watu wa Jamhuri ya Kenya tutakuwa na shida za kibinafsi. Hiyo shida itaingia kwenye familia zetu. Itatuletea pia Jamii, community na mwishowe itakuwa inatupea nini?

**Audience:** silent

**Com. Salome Muigai:** ya taifa nzima. Kwa hivyo hizi ni jukumu letu, nyingi sitajengea moja kwa jingine lakini nimewapa mfano tu na pia ukienda nyumbani tafathali tazama gazetti lako uweze kuyasoma

Wasikazi wenye kamwone kaya kama Mkenya. Tafadhali mkitaka chekpot … akalia zaidi na tunasema haki zaka. Lakini nigetaka kuwaomba wenye simu za mkono, tuzifunge tafadhali. Na ningetaka kuanza na yangu. Basi tuendelee na sura nne.

Sura ya inne inazungumzia uraia. Huwezi kuwa na malengo ya Kenya ukiwa pengine wewe sio Mkenya. Kwa hivyo tuangalie nani atakuwa Mkenya. Tunaagalia kanuni za kujiunga kuhusu uraia. Pia tunaagalia kudumisha uraia ulioko, ukiwa wewe tayari ni raia wa Kenya. Itabidi ufanye nini ili kudumisha huyo uraia. Tunagalia pia vile unaweza kupata uraia, ukiwa wewe sio raia tayari. Tunasema kuna uraia wa nini? No. 19 kuna uraia wa nini?

**Audience:** (**inaudible)**

**Com. Salome Muigai:** wakuzaliwa. Kuna uraia wa ndoa. Hiyo ya ndoa nigetaka kueleza kidogo. Katika Katiba tulioko nayo hapa wakati huu. Saa zingine mimi nikiwa na ndugu na dada, Fami aende aoe muhindi ama aoe mschana kutoka hapa Uganda. Huyo bibi anathibitishwa uraia wa Kenya na Fami. Amempatia uraia. Mimi nikienda niolewe na Muhindi ama Mganda ama Mrwanda katiba ilioko sasa haikubalishi kumpatia bwana yangu uraia wa Kenya. Hii Katiba mpya inasema kila mtu mwenye kuoa ama kuolewa na Mkenya ana haki ya kuwa Mkenya, kwa hivyo kuna hiyo tafauti. Pia zaidi ya hayo watoto wa Fami akiowa mgeni, wanakubalishwa kuwa Wakenya. Lakini watoto wa bibi mwenye aliolewa na mtu asio wa hapa walikuwa hawafanywi kuwa Wakenya. Mzee mmoja alitupatia mfano tukiwa, nafkiri tulikuwa Meru ama Nyeri. Alituambia kuwa siku moja alikuwa mgonjwa sana amelala Kenyatta National Hospital na watoto wake mmoja alikuwa ameolewa wingereza na kijana wake yuko America na ameowa Mamerica. Wakaitwa waje wamuone baba huaja akafa. Wakifika airport yule kijana mwenye aliotoka America akakubalishwa akuje na bibi yake na watoto wake. Lakini yule mschana mwenye alikuwa ameolewa wigereza alikubalishwa kuja kufika airport, yeye akaingia lakini watoto wake wakafungiwa kule airport, wakaambiwa hao sio Wakenya. Je mungetaka hii iendelee ama ibadilike?

**Audience:** ibadilike

**Com. Salome Muigai:** Ama iendelee? Mukitaka kusema iendelee sema tu. Kuna uhuru wa maoni. Basi hii Katiba inapendekeza kuwa mtoto yoyote wa Kenya aweze kumpa uraia kwa watoto wake na pia bwana ama bibi yake. Tunaelewa hiyo?

**Speaker:** Are we supposed to react?

**Com. Salome Muigai:** No, not during this time. Utaleta maswali nyuma. Kwani tukianza kureact wakati huu na tuko kwa tune ya nne katambo tufike sura ya ishirini na mbili kutakuwa usiku. Weka swali lako, liandike usisahao halafu utauliza. Tumeandika pia kila mtu anaweza kuwa raia kujiandikisha na pia kuna jambo lingine no. 22 lenye linasema kuwa mtoto yoyote akiokotwa Kenya, akipatikana Kenya hajulikani wazazi wake, upelelezi ufanywe akose kabisa kujulikana alitoka wapi? Ama alikuja aje hapa? Awe anaonekana kama ana miaka nane basi atapatiwa uraia wa Kenya. Sababu gani? Nasema, watoto wote ni lazima wawe shuleni. Na kwani hadi miaka nane mtoto hakuenda shuleni, tutachukua huyo mtoto, na tutamulazimisha kwenda shule. Basi tutakuona kama Mkenya. Tunaelewa hapo? Kwa nini tumechagua miaka nane? Kwa sababu miaka nane bado ni wakati wa kwenda shuleni. Mtu akiwa na miaka kumi au miaka kumi na tano ataweza kujieleza yeye ni nani.

Pia No. 23, makabila ya Kikenya yanayo ishi karibu na mipaka, sana sana wanatueleza kuwa hawa wakitaka kuwa raia wa Kenya na wawe raia wa inchi nyingine. Sana sana tulielezewa haya na Wasomali wenye kukaa katika mipaka ya Somali na Kenya na Ethipia na Kenya. Wanatuambia wakati wa kiangazi tunapeleka mifugo yetu inchi zingine. That is how we save our economy. Ushuru wetu ni wanyama wetu kwa hivyo tukiwapeleka nchi zingine wakati kuna mvua na kuwarundisha inchini ndiyo tunaweza kuzileta sisi wenyewe. Tuliambiwa hivi na wasomali na kabila zingine kama Maasai, Kajiado na Arusha, Wateso, Wasamia, Bukusu na Wagisu., Mt Elgon. Basi tukafikiria kwenye hii Katiba mpya tumekubalisha kuwa mtu anaweza

kuwa raia wa nchi mbili. Mradi tu pawe na maelewano kati ya Kenya na nchi hiyo ingine ya pili. Isio ni nchi tu ya Kenya.

Kuna raia wazazi kufa kabla ya mtu kuzaliwa. Kwa mfano baba anaweza kuwa ameowa ama hajaowa lakini wameanzisha mtoto lakini kabla huyo mtoto azaliwe baba afe. Unasema huyo mtoto akizaliwa baado ana haki ya kuwa nini?
**Audience:** Mkenya.

**Com. Salome Muigai:** Kuna haki ya makao. Tunasema Mkenya anaweza kukaa mahali popote. Kuna haki ya uwezo wa Bunge. Tumewambia wabunge vile inaweza kufanya na uraia. Na pia kikomo cha Bunge, pahali gani hauwezi kugusa uraia wa mtu.. Na pia tumeweka kwenye Katiba hii mpya hal mashauri yenye itaweza kumtajiri uraia. There will be a special committee that will deal with citizenship. Itaajiri watu kama wewe kuwa raia na itakuwa kamati mpya.

Halafu sasa tuende sura ya tano. Hii ni sheria ya Haki. Haki za binadam. Hii ndiyo mambo nyingi tumesikia kutoka wananchi wote, ili kuwa juu ya haki yao. Lakini nasema pia tumeweka wajibu wa Kenya kabla ya haki ya nani?
**Audience:** Mkenya

**Com. Salome Muigai:** It is by design, kuwa wajibu unakuja mbele ya haki. Tuna haki lakini zaidi ya haki kuna nini?
**Audience:** wajibu

**Com. Salome Muigai:** Kuna wajibu. Tumezungumza juu ya haki za kimsingi na uhuru. Tumezungumzia pia juu ya wajibu wa serikali kuendeleza uhuru wa watu, tumeweka mipaka kwenye haki. Hakuna haki isio na nini? Na mpaka. Tulipokuwa tukizungumza na Bwana Tororei pale inje aliendelea kuzungusha hiyo macho yake, unajua hii macho ya Tororei ni marefu kuliko ya kila mtu. Aliendelea kuzungusha kila pahali. Nikamwambia hii macho yako unaizungusha kila mahali unaweza kugonga mtu nayo. Na afikapo zinakomea pahali zangu zinaanza. Munaelewa? Nina haki zote lakini zina nini? Zina kikovo, zinakoma mahali zingine zina anza. Kwa hivyo nikisema kila mtu ana haki ya shamba, huwezi kuja kuchukua langu kwa sababu wewe hunahaki. Wewe una haki na mimi nina nini? Tutaangalia haki yako ya shamba itatupeleka wapi ndiyo nikukatie shamba lakini huwezi kuja kunyakua yangu, haki zako zinakomea pahali haki zako zinaanza. Kwa hivyo haki zote zina mikopo na mipaka ya hizo haki zimezungumziwa kwa urefu kwenye kitengele cha 31.

Kitengele cha 32 kina zungumzia habari ya haki ya kuishi. The right to life. Haki ya uhai. Tumesema kwamba haki ya uhaia hupatiwi na mtu. Kwa hivyo hakuna mtu anaweza kupokonya. The right to life is not given so it cannot be removed. Na kwa hivyo kwenye hii Katiba ya leo ama hii Katiba mpya tumekanusha adhabu ya kifo. Tulipotembelea jamii mbali mbali za Kenya mimi mwenyewe nilijifunza mengi sana lakini ile ya kwanza nilijifunza ni kuwa hakuna katika Kenya lenye limesema mtu akimua mwingine naye auwawe. Ilikuwa mtu akimuua mwingine analipa nizaa, compensation kwa jamii ya wale mtu wao ameuwawa. Akikosa nidaa anatengwa na jamii……

Kama pastor moja alituambia alikuwa ni mwanaume. Wote ni wanaume wenye walikuwa wanauwa zamani. Siku hizi sijui kama bado kuko hivyo. Sana akiwa ni mwanaume alikuwa hapatiwi bibi. Kwa hivyo ukoo wake ulisha na nani? Na yeye mwenyewe. Hakuweza kuzalisha ukoo wake.

Watu wengine pia walituambia mtu kama angekuwa ameua na akose pesa ya kulipa ridaa na watu wote wakose tulimfukuza kwenye jamii. Basi hakuwa mmoja wa hiyo jamii. Lakini hakuna mmoja lieye tuambia sisi tulimua ama tunayo. Jamii ya kinandi ilikuwa ikifanya nini mtu akiuwa?

**Audience:** ana lipa ngombe

**Com. Salome Muigai:** Analipa ngombe, okay. Ana kuwa cleansed, anatakaswa. Kwa hivyo sasa tumesema adhabu ya kifo haitkuwa kwenye Katiba yetu mpya. Tumezungumzia sana usawa, equality.

Tumesema kuwa equality does not mean same. Kuwa tuna usawa wa kihaki haisemi sisi wote ni sawa sawa. Kwa mfano, tukisema watu wa ulemabu wana equality na wale watu wengine. Sio kusema tukienda kwenye freedom from hunger walk, lazima pia hao wafanye hivyo. Waende wataweza?

**Audience:** Laa

**Com. Salome Muigai:** Lakini tunasema kuwa wapewe ile yenye wangeweza kufanya wapewe nafasi sawa. Tunaelewana?

**Audience:** Ndiyo

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo tukisema kuna usawa kati ya wanaume na wanawake hatusemi wanaume na wanawake wamefanana. awafanani, wangefanana kungekuwa na castrostophi yani kungekuwa na generation ngapi? Hii moja halafu ishie. Kwa hivyo wanawake na wanaume hawafanani tafadhali. Vile tunasema ni wana haki sawa. Ingawa hawafanani bado wana haki sawa. Watoto wanahaki sawa na watu wazima. Hiyo sikusema wanafanana. Nikusema mataka yao lazima iwekewe manani kama yale ya watu wazima. Ndiyo tukiwa na hospitali tunakuwa na upande wakina mama, tunakuwa na upande wa kina baba, tunakuwa pia na upande wa watoto. Hiyo ndiyo maana ya usawa. Equality does not mean the same it means kila mtu apatiwe equity. Equity inakuja baada ya equality ndiyo tunasema tukiwa tuna watu ni sawa na tumekubali hayo basi tukiwatutaondoka hapa, twende maili ishirini pengine Salome atahitaji kubebwa na boda boda. Hapa kuna boda boda? Zile baiskeli

**Audience:** ndio

**Com. Salome Muigai:** Ndio aweze kuandamana na nini? Na wengine. Those are the kind of things we are talking about the differences between equality, equity and being the same. We need to understand this values very clearly. Because when we do not understand them zinatishatisha. When we say that the Kikuyu’s and the Kalenjin’s are equal, do you think they are the same?

**Audience:** No

**Com. Salome Muigai:** No, they have different, what differences do they have?

**Audience:** culture

**Com. Salome Muigai:** different culture, language, customs but we are saying in the eyes of the Lord they are equal. So, equal and same do not mean the same thing. Tukisema kila mtu anahaki ya kulishwa vizuri na tunamchukulia manane tafauti zetu ni lazima Mkalenjin tutampa nini?

**Audience:** Kimiet

**Com. Salome Muigai:** na nini?

**Audience:** maziwa

**Com. Salome Muigai:** na maziwa ama na?

**Audience:** mursik

**Com. Salome Muigai:** Lazima tumpatie Mkikuyu nini?

**Audience:** Githeri

**Com. Salome Muigai:** Githeri ndiyo asikie amelishwa.

**Audience:**

**Com. Salome Muigai:** Ikiwa kati yetu kuna Muhindi tumpatie nini?

**Audience:**

**Com. Salome Muigai:** Chapati na wali, sivo. Kukiwa kati yetu kuna Mwislaamu na tulikuwa tumechinja nguruwe lazima tumtafutie ngombe. You see. Hiyo ni kuhisi kila mtu yeye ana equality. Lakini katikati ya hiyo equality tunaangalia masilahi yake iliyo tafauti. Is that clear?

**Audience:** Yes

**Com. Salome Muigai:** Pia nitapeyana mfano moja kuwa hii ili kuwa jambo kuu sana wakati nilikuwa mtoto mdogo. Lazima tufikirie mtoto wetu aliyenaulemavu, na yule asio naulemavu hao wote wako na equality. Tukifikiria hivyo ndio tutafikiria yule mwenye ulemavu tutamsaidia vipi ili aweza kupata masomo sawa na yule mwenye hana nini?

**Audience:**

**Com. Salome Muigai:** Hana ulemavu. Wakati huo ndiyo tunasema Township School lazima wakuwe na unit ya blind. Tumecheleweshа kwenda karani wa County Council na furahia uko hapa, kuwa kwa nini Township hata ingawa miaka hii yote,

you see we don't have unit of the blind of the deaf; Watoto wetu wale ambao hawasikii na hawaoni wako wapi? Twasema pia wachanganike na watu wengine. Kwani asiyejua kunena mswahili asema afanye nini? Asiyejua hakubaligi. Kwa hivyo ni lazima watoto wetu wasome pamoja ndiyo wajuane na wapate kufanya nini?

**Audience:** kuthaminiana

**Com. Salome Muigai:** Kuthaminiana. These are things of equality, equity are not the same. Haki ingine ya No. 34, ni uhuru kutokana na ubaguzi. It says freedom or life noquity is not to be discriminated at all. Mtu hawezi kubaguliwa kwa kuwa yeye ni mwanaume ama ni mwanamke, ama ni kabla fulani, ama ni mrefu ama ni mfupi, ama ana ulemavu. Mtu hakuwe hatakufanya nini? Mtu asibaguliwe, if you are a Kenyan you should not be discriminated against And if we are freed of discrimination, then we are free to be able to participate fully, aren't we?

Kama umepatiwa uhuru ubaguliwe basi unaweza kurudishwa kwa kila jambo vile uwezavyo wewe mwenyewe.

35, ni haki za wanawake. Tulizungumzia kuwa thamana yetu moja ni kuhakikisha kuwa wanawake wanahusishwa kwenye nini? Uongozi. Sasa ndiyo haki zao tumepatiwa zaidi. Tumesema hawawezi kubaguliwa, tumesema jambo lengine twataka sasa kwenye hii jamii ya Kalenjin na jamii ya Wakikuyu walituambia kuwa, mtoto asibaguliwe kwa urithi kwa jili yeye ni mwanamke ama ni mvulana. Jamii ya kutoka Nyanza ilikuwa na shida sana na hiyo. Wengine mtaniambia maoni yenu mwishoni.

Pia tuna haki za wazee. Kwa muda mrefu wazee wetu wamekuwa hawatambuliki kazi yenye walifanyia hii nchi. Atakama mtu alieba kutoka kijabe huyo naye amefanya kazi, kama ameiba hii miaka hii yote na hajashikwa, ata yeye amejaribu sivyo?

**Audience: laughter**

**Com. Salome Muigai:** Lakini sana sana tunafikiria kazi yenye wazee wetu wakongwe wamefanyia inchi. Kama mtu amekuwa mchugaji, kama amekuwa mkulima, amekuwa mtunzaji amaelea watoto wake. Amefanya kazi kubwa si afadhali na omba tuwe na mkutono mmoja. Nitawapa nafasi ya kuzungumzia mwishoe. Munataka kuitambua kazi yenye wazee wetu wameifanyia nini? Hii ni Taifa na twasema hivi, wazee ingawa wamekuwa wazee, wakati wa kujivaa na heshima zao zimekomaa. Wapatiwe nafasi ya kuhusishwa kwenye uongozi na mambo mengi yenye imefanyika katika kijiji, katika jamii na katika Taifa nzima. Tunasema pia watu wakuangalia maisha ya mzee ni yake yeye mwenyewe. Aweke mali yake yaweze kujiangalia na kujitunza akiwa mzee. Lakini akikosa kujiweza akiwa mzee basi tutawajulisha Taifa kumchunga nani? Kumtunza mzee ili tuwetuna mpa chakula cha kutosha, mahali pa kukaa, hapati matibabu wakati anapokuwa mgonjwa. Hizo ni haki za wazee mtazisoma kwa urefu.

Tunasema pia kuna haki za watoto, watoto wana haki zao. Walimu wametulalamikia sana kwa sababu tumesema watoto wasipigwe. Watoto tumesema wasipoangaliwa na kila mtu hawawezi wenyewe kujitunza kwa hivyo ni wajibu wa kila mtu kutunza watoto. Tumesema mtoto ana haki, ya kulindwa na kulewa na baba na mama wawe wako katika ndoa ama wako inje

ya ndoa. Hao watoto wenyewe hawakujua hiyo mambo yote. Hiyo ilikuwa katikati ya nani?

**Audience:** ya wazazi

**Com. Salome Muigai:** Lakini mtoto akishazaliwa huyo mtoto ni Mkenya sivyo? Kwa hivyo huyo mtoto asipotetewa na baba yake na mama yake lazima atetewe na nani?

**Audience:** na Taifa

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo tumesema mtoto yoyote anahaki yakulindwa na kulelewa na baba na mama. Pia kwa masilahi ya watoto tumesema mtoto anahaki ya kwenda shule. Kwa hivyo tumesema masomo kutokea nursery mpaka form four yatakuwa ya bure na ya lazima. Every child must be in school. Watu wengi wanafikiria masomo ikiwa ya bure kila mtoto ataenda shuleni. Hii ni ukweli? Laa. Kuna watoto wenye hawataenda shule. Watoto wenye wako kwa mitaa yetu ikiwa elimu sio ya lazma watatoka mijini waende shuleni? Laa. Watoto wengine tutawatoa kwenye shule kwa miaka miwili na kuwaoza nje wakaanza kuwa mama wakiwa na miaka kumi na nne. Au tu watakaa kwa shule? Laa. Kwa hivyo tumependekeza kuwa watoto wawe shuleni. Shule iwe ya bure na pia iwe ya lazima. Kwa hivyo mzazi utaulizwa na Taifa kwa nini mtoto wako hayuko shuleni?

Kuna pia haki za familia, kuna pia haki za walemavu katika hii haki tumesema majengo yote kama hii lazima itakubalisha kila mmoja wa wanakenya kuweza kuingia bila hitilafu yoyote. Kwa hivyo watu waende wangalie hii mijengo ili kila mmoja aweze kuingia. Na pia tumesema kwa lugha zote
zinatambulika Kenya hata kwenye bunge. Pia mikutano ya mijadala lazima tukubaliane lugha ya ishara. Na maadishi ya kweli ita tafsiriwa pia. Tumezugumzia kwa kirefu habari ya heshima za kibinadam, yani personal dignity ya kila mmoja ya Wakenya. Tumezungumzia uhuru na usalama ya kila mtu. Mwanakenya mwenye atakubalishwa kuwa mtumwa wala kufanya kazi bila kulipwa. Amakufanyishwa kazi ya lazma.

Faraza: faraza maana yake ni privacy. Wewe ukiwa nyumbani mwako Katiba inakulinda ili mambo yako isiingiliwe tu ovyo ovyo. Kukiwa kunamtu anataka kuingia kwa nyumba yako ama askari anataka kuja kutoa kitu chochote kwa nyumba yako ni lazima itambidi apate kipande cha koti. So that we protect your privacy.

Tumefikiria pia uhuru wa dini ni mbali na maoni. Watu wengi sana walituuliza kama Katiba hii mpya itakubali tu abudu Mungu na si kuabudu nini?

**Audience:** shetani.

**Com. Salome Muigai:** Lakini nayo Katiba inakiko chake. Ukieleza kuwa watu wasiabudu shetani ama wakiambiwa waabudu Mungu peke yake kwa kisheria ni lazima utafsiri kuwa Mungu ni kusema nini? Na shetani ni kusema nini? Tulikuwa na shida kubwa sana kutafsiri Mungu na kutafsiri shetani. How do you interpret devil worship? Utasema devil worship ni nini?

Ukiulizwa. Na ukifika mahakamani ni lazima ujieleze. Yule anabudu shetani kwa hivyo alifanya nini? Sasa vile tumesema tutaweka hii uhuru ya kuabudu kwenye Katiba lakini tutauliza bunge itengeneze sheria zingine za kusema huwezi kuzui mtoto akawa safana. Hatutaki dini zenye kufanya A,B,C,D unaelewa. Ile utekelezaji, nafasi ya utekelezaji lakini kunanafasi ya Katiba nitaiachia hapo. Tumesema tuna uhuru wa maoni, na kuna uhuru wa kuchapisha maoni yako. Kuna uhuru wa kufikiwa na habari. Kuna uhuru wa kuomba habari. Ukitaka kujua habari yoyote iliyo katika ofisi ya Serikali hii Katiba ama kwa ofisi nyingine inakukubalisha kuuliza kuhusu hiyo habari. Kuna uhuru wa kushirikiana, wa mikutano, wa maandamano, wa kuchochea mugomo yani unaweza kugoma. Na uhuru wa malalamiko. Ukitaka kulalamika watu wakitaka kujiunga pamoja wakaweka sahihi zao wakafanya petition kwa wizara yoyote ama jambo lolote la Serikali ama la public wamekubalishwa katika hii Katiba mpya. Una haki ya kisiasa, you have a right to political right, una haki, uhuru wa kwenda utakapo na kukaa utakapo. Kupitia hii hewa ya Eldoret hakufai hivi na ungetaka kwenda kukaa mandera unahaki ya kufanya nini?

**Audience:**

**Com. Salome Muigai:** Yakwenda huko. Ukitaka kwenda Kanyen, umpende mungu wa karibu mount Elgon anankufaa ni afathali mungu wa Mount Kenya pengine atakusikia zaidi una haki ya kufanya nini ya kwenda huko na pia una haki ya kukaa huko. Kuna haki pia ya wakimbizi na watafuta hifathi (refugees) watu wenye wanakimbilia inchi hii wana haki zao na zimehifathiwa katika Katiba yetu.

Pia, una uhuru wa biashara, kazi na ujuzi. Kila mtu ana uhuru wa kufanya biashara zake na kufanyia profession yake na kuiendesha. Tafadhali tungefungua madirisha, kumekuwa na joto sana. una uhuru wakuwa na mali. Mkenya yoyote ana uhuru wakuwa na mali. Una uhuru wa usiasa wa kikazi. Una uhuru wa usalama wa kijamii. Usalama wako wewe mwenyewe na usalama wa jamii yako. Una haki ya afya, una haki ya kutaka kukaa kwa afya mzuri. Ukiangalia hapo utaona vile Serikali ina husishwa kuhakikisha kuwa kila mtu anaweza kupata uhifathi wa afya yake. Una haki ya elimu, nilikuwa nimeizugumzia, kuna haki ya kuwa na pahali pakukaa kama nyumba, kuna haki ya kuwa na chakula chakutosha na kinachofaa. Kuna haki ya kuwa na maji masafi na yakukusaidia. Kuna haki ya usafi ya kutokuwa na ….. Tulisema haki yako inatokea wapi? Mahali haki ya mwingine inaanza. Kwa hivyo mimi ingawa nina haki ya kuzungumza kikikuyu siwezi kuitia hii haki yangu halafu nitanza kuzungumzia kila mtu kikuyu naniko kwa mkutano wa hadara. Igawa hiyo ni haki yangu inamalizikia pahali, nani mwenye haelewi kikuyu hapa? Inua mkono kama huelewi kikuyu. Basi pahali haki yake inapoanza ndiyo haki yangu nayo inafanya nini? Inakomea. Kwani yeye ana haki ya kuelewa vile ninasema, sivyo, basi tuna haki za lugha na kitamaduni lakini ni lazima zikubalishe kila mtu kuwa na nafasi yake. Tuna haki ya wateja consumer right. Tuna haki ya kuziwa bithaa zilizo nzuri na ikiwa sio nzuri tuna haki zetu za kuweza kutetea haki hizo.

Kuna haki za utawala wa haki. We have a right for proper administration. Tuna haki za kutawaliwa vilivyo bora na kuhudumiwa. Kwa hivyo mimi nikienda kwa hudumu wa Serikali nisikie sijahudumiwa viliyo. Na sikia haki yangu kufanya nini?

**Audience:** kuvunjwa

**Com. Salome Muigai:** Imevunjwa, imekeukwa sivyo. Kwa hivyo tutawaeleza pahali gani tumeweka nini kwenye hii Katiba ya kuweza kutusaidia kwa mambo kama hayo. Tuna haki ya kutofuata maagizo ya sio halali. Kwa mfano mimi nikiwa sipendi rangi ya majano, ikiwa sipendi yellow, nikakuambia kwani mimi sipendi yellow, nkaambia Paul kila mtu mwenye amevaa hiyo rangi yenye sipendi simkubalishi kwenye mkutano. Paul ana haki ya kutotii amri yangu ingawa pengine mimi ni mwajiri wake. Tunelewa?

**Audience:** ndiyo

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo tuna haki ya kutotii amri zilizo halali. Hii imekuja zaidi kwa jili ya janda lililo pata Rwanda. Wengi wa watu waliopelekwa Kotini walisema mimi nilikuwa nikifuata amri. Na amri ya kwambiwa umthuru mtu mwingine na unakubali kumthuru mtu mwingine ukijua uthulumu wa mtu mwingine ukijua kuthulumu mtu mwingine sio halali. Basi hii Katiba inasema una haki ya kukataa kufuata amri zisizo halali. Na ukizifuata basi wakati utakuja kuhukumiwa huwezi kujitetea kwa kusema nilikuwa nikifuata nini?

**Audience:** amri

**Com. Salome Muigai:** amri ambaye vile niliambiwa nifanye. Una haki ya kusikia mahakama, kila mmoja wetu ni lazima apatiwe nafasi ya kuingia kwenye mahakama ya kustaki case yake na case yake kusikika kwa wakati unao fanya nini?

**Audience:** unaofaa

**Com. Salome Muigai:** unaofaa, sivyo? Ukiwa wewe unatoka tarbo kuna Kosa? Hapana hii ni South. Ukiwaunatoka burnt forest, burnt forest si bado ni this Constituency?

**Audience:** silence

**Com. Salome Muigai:** ukiwa unatoka burnt forest kila siku kuja casi pengine una leta mashahidi ishirini. Casi yako ikose kusikizwa mwezi mmoja, ihairishwe muezi mmoja, ihairishwe miezi tatu, inne, tano, maika tano. Utaweza kuendelea kufanya hivyo?

**Audience:** silence

**Com. Salome Muigai:** pengine alikuwa ameiba ngombe yako mmoja, sasa kukuja mara hiyo yote siitakubidi kuuza wale watono wenye walibaki?

**Audience:** ndiyo

**Com. Salome Muigai:** Ndiyo uweze kufatilia huyo mmoja. Kwa hivyo ndiyo hii Katiba inasema kila mwananchi ana haki ya kutia mahakama na kuyatia kwa wakati ufaao ili asikuwe kufuatana na mahakama inakuwa kazi ya kumthurumu mwananchi kwa mara ya pili. Tayari amethulumiwa kwa ile njambo yenye amekuja kuleta kwenye mahakama. Mahakama pia isionekane

kama imefanya nini? Inamthulumu zaidi. Kuna haki ya watu wenye wameshikwa waliotiwa nguvuni. Una haki zako kwa hivyo hii Katiba ukiangalia inasema mtu akishikwa ni lazima kufikia wakati fulani fulani awe amefikishwa cotini naye kasi ziwe zimetatuliwa kufuatia muda fulani.

Mungetaka kikomo cha miaka mbili?
**Audience:** silence

**Com. Salome Muigai:** Would you like a break for two minutes, muzungumze hapo kidogo? Ama tuendelea? Mungetaka nini?
**Audience:** tuendelee

**Com. Salome Muigai:** Okay. Pia tunasema kuna haki ya walio kizuizini. There are prisoners rights. Kama wewe umeshikwa na umezuiliwa una haki zako. Tafadhali atoke uangalie zimesema nini? Hizi haki zote wakati wa hali wa hatari zinasimamishwa. Kwa hivyo zimesema mambo fulani zimependekeza mambo fulani kuhusu hali ya hatari ili haki za wananchi zisisimamishwe kwa muda mrefu zaidi ya vile inavyo hitajika. Tumesema kuwa kuna haki ya matumizi ya sheria ya haki. Yani ukiwa na haki hizi zote ukiwa huwezi kujitetea kwenye sheria hazikusaidie. Lakini tumeweka sheria zenye zitakuwezesha kutetea haki zako. Tumesema kuwa tutaweka tume ya haki ya binadam na haki za kitawala ili kuweza kuchunguza wakati wakati hujapatiwa haki zako. Kwa hivyo ukiwa unamalalamishi kutakuwa na hili tume litawekwa na litawekwa kwa Katiba. Tumeeleza nani anaweza kuwa mwana tume kwenye hili tume. Halafu huku ukipeleka ulalamishi wako itakuwa kazi ya hiyo tume kuchuguza na kuhakikisha kuwa umerudishiwa haki zako. Pia tumeiwekea jukumu mahakama kuweza kutekeleza haki za kibinadam. Yani kuenda kwenye koti ukiwa pia haki zako zimeupigwa utaweza kusaidiwa. Hiyo ndiyo mwisho wa sura la tano, na nimeisomea kwa kirefu kwa jili hii ni mambo yenye kila mtu alikuwa na shida kubwa sana na hii hali.

Sura ya sita inazungumzia uwakilishi wa watu katika sehemu mbali mbali. Sehemu ya kwanza ni utaratibu wa upigaji wa kura. Tumesema kuna kanuni za jumla juu ya haki ya kupiga kura. Tumezungumzia uchaguzi mwenyewe. Katika uchaguzi tumefanya mabadiliko kidogo. Wakati huu mtu mwenye anachaguliwa kusimamia mwingine ama kuwakilisha yule mtu aliyepata kura nyingi zaidi katika kikao cha bunge ama kikao cha udiwani, sivyo? Sasa tumesema uchaguzi mwingine wenye utafanywa katika hii Katiba kutakuwa na kura mbili za wakilishaji. Wewe ukienda kupiga kura mwenye unataka mbunge wako kwa mfano, pia utapigia chama. Utakuwa na kura ngapi?

**Audience:** mbili

**Com. Salome Muigai:** mbili, moja ya nani?
**Audience: (inaudible)**

**Com. Salome Muigai:** Moja ya mbunge na moja ya chama. Sasa hizi kura za chama, umhimu wake ni nini?

**Audience:**

**Com. Salome Muigai:** Ni kuwa chama chenye kitakuwa.. Ngoja kwanza niwambie kwa nini tulifika hapo. Tulipokuja kwenye kikao cheye kina watu wengi kama iwasingishu tuliambiwa kuwa ni mipaka ya vikao vya bunge ya wakilishao bunge vinatakiwa kupatwa kulingana na nini? Munafikiri watu huwasia kulingana na nini?

**Audience:** wingi wa watu

**Com. Salome Muigai:** Na wingi wa watu. Kwa kila pahali penye tulienda Central Province, yote nikianzia hivyo Western Province na mahali fulani fulani katika Rift Valley tuliambiwa hivi na Nyanza pia tumeambiwa hivyo. Lakini tulikwenda mahali pengine hapa katika Rift Valley kama mimi mwenyewe nilipoenda Arong Marakwet, tuliambiwa kuwa ukifanya mipaka ya Constituency tafathali mufikirie mazingara ya watu. Kuna pahali pengine hapa unakuta mtu mmoja hapa kutetea kufikia pahali mambo mengi yalipo inakuwa ubali mkubwa zaidi. Kwa hivyo mfikirie kuburatia wakati wakufikiria nini?

**Audience:**

**Com. Salome Muigai:** Vikao vya wakilishaji. Tulipoenda Mandela, na North Eastern yote tuliambiwa musifikirie witu wa watu kamwe. Fikirieni geoghraphia peke yake. Kwani hapa kwetu wakati mwingine ukitaka kwenda pahali mbunge wako ana mkutano inakubidi kutembea amakufikia maili mia mbili, maili mia tano. Kwa hivyo hii habari ya wingi wa watu musahau, mfikirie tu habari ya umbali. Sasa hao watu wenye walituambia tufikirie umbali walikuwa watu wa kutoka wapi? Kenya. Na watu wakituambia tusifikirie wingi wa watu walikuwa wanatoka wapi? Kenya. Sasa ndiyo tumefikiria tuje na hali yenye itashugulikia shida za hao watu wote.

Tuna sema hivi, ukipiga kura ya mbunge na upige ya chama, mbunge mwenye atapata kura nyingi zaidi ataingia lakini pia chama chake kitapasa kupatiwa vitu via ziada ikiwa na watu wengi. Hizi viti vya ziada tumesama zitalinganishwa na chama kilichopata. Lakini hizi kura za ziada kama ni hapa Eldoret ndiyo pahali ikiwa mbunge ametoka kwa jamii moja, ndiyo pahali wanafikiria yule jamii mdogo. For example ikiwa hapa mbunge mwenye anaingia ni Major Muigai, ni wanani hivi vyama vingine, warudi wapatiwe viti zingine kumi hapo ndiyo watafikiria habari ya kabila zile ndogo. Kabila ndogo hapa ni kina nani?

**Audience:**

**Com. Salome Muigai :** Turkana, Ogiek, kwanza tuanzie na Ogiek kwani Turkana pengine watakuwa wamepata mbunge kwao Lodwar sivyo? Lakini Ogiek atawakikaa miaka ishirini watamwingiza mjumbe kwa kura?

**Audience:** Laa

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo pengine hiyo itakuwa priority ya kwanza hapa. Pia tunasema sana sana wale watu wenye kusimama habari ya siasa pengine wengine wao sio watana, sivyo? Ama pengine ni watana? Pengine tu saa zile tumemuingisha

mbunge wetu hapa sisi kama watu wa kikao hiki cha Eldoret South. Lakini pia sisi kazi yetu ile kubwa hapa ya usafishaji wa mali ni nini?

**Audience:** ukulima

**Com. Salome Muigai:** Ni ukulima. Sindiyo tungefikiria tungepeleka mjamaa mmoja wapi? Mbunge ndiyo aweze kutuletea masilahi ya nini? Ya wakulima. Kwa hivyo hizi viti vya siada zitahakikisha moja waliopata ni mkulima. Na mambo kama hayo, kila nafasi ya wafishaji wa bunge itakuwa na matakwa tafauti na upande ule mwingine. Pengine tukienda Wajir watasema lazima tupate mtu mwenye Ngamia. Kwani ndiyo mwenye atajua shida za Ngamia zetu. Kwa hivyo itakuwa tafauti lakini itawaleta watu wengi kwenye utawala wenye kutetea masilahi mbali mbali. Hizo ndivyo zile vitu unasikia zikiambia ziko between tisaini. Na watu wanasema hao watu watakuwa hawajachaguliwa. La hasa watakuwa wamechaguliwa kutoka kwa ile nafasi, Constituency kutetea masilahi fulani. Nusu yao kama hapa chama kiliko na watu wengi ni kipi?

**Audience:** Kanu

**Com. Salome Muigai:** Kanu, kwa hivyo kazi ikiwa na viti vingine via zihada kumi itawabidi mpee hizo viti tano kwenda kwa kina mama. Mtu anaweza kuwa mama na akawa mkulima sivyo? Anaweza kuwa mama na akawa mtaalam kwa mambo fulani. Kwa hivyo nusu yake itaenda kwa kina mama. Nusu yenye itabaki itaenda kwa watu wenye nilikuwa nimeseama, makabila yenye haiwezi kupata nafasi ya kupeleka mtu bunge kwa wingi wao, vijana, watu kama walemavu wenye wanashida fulani, na pia wataalam wa namna moja ama ile nyingine. Tunaelewa hii? Kwani hii ni jambo tafauti kwa hivyo itahitajika kueleweka sababu gani tumeweka. Now kwa siasa itakuwa mara nyingi imewatoanisha watu kwa wingi na kwa geographia, sindiyo? Wale watu wengi watapata vitu vingi zaidi kwa ajili ya wengi wao si ni kweli? Na wale watu wenye geographia tafauti bado watapata vitu vyao. Kwa sababu tuliona kama tukisema kila kikao cha bunge lazima kiwe na watu thelatini. Kulikuwa na watu wengi walituambia kuwe na wapiga kura 30,000 elfu.

Ukienda kama pahali kama North Eastern, kama Madera, kama Wajir, kuwapata watu 30,000 elfu utakuwa umeenda karibu kuzunguka Wasingishu na Transzoia na Nazi na Marakwet na Keiyo. Wilaya kama tano ndiyo upate watu 30,000 elfu wapigaji kura. Sasa huyo mtu mmoja ukimwambia awe mjumbe wa hao watu wote umewasaidia, wamesaidika? La. Kwa hivyo ilikuwa kazi yetu kubwa ni kujaribu kuagalia matako ya kila watu. Tuone watu wenye miji wamesaidika kama hapa Wasingishu, lakini pia watu wakutoka ijara wenye ni wachache pia wamefanya nini? Wemesaidika. Huyo ni habari ya uchaguzi.

Tumeweka haki ya kupiga kura, hata kwa watu wenye ulemavu tumesema ni jukumu ya wenye kuendesha uchaguzi kuhakikisha kuwa wamepata usaidizi wa kutosha kuwawezesha kufika na kupiga kura zao. Tumesema pia wafungwa wanahaki ya kupiga kura, pia hao ni Wanakenya. Tumesema mahitaji ya mtu ili aweze kusajiriwa kupiga kura. Tumezungumzia habari ya kutostahili kuajiriwa kupiga kura. Tumezugumzia habari ya kupiga kura kwenyewe, ndiyo yenyewe. Na tumezungumzia habari ya wagombeaji bila kupingwa. Hiyo pia ningetaka kueleza kidodo.

Kwa mwajibu wa Katiba iliko sasa hukiwa hujapingwa mara nyingi kwenye kikao chako cha bunge hatufai tena tupigi kura, ni kweli? Tunajitangaza tu kuwa umeshapita. Lakini sasa kwa ajili ya hivyo kuwa chama chako kitahitaji zile kura, hizo zenye umepigiwa wewe mwenyewe na pia zenye umepigiwa chama chako, atakukiwa mtu hana mtu mwenye kumpinga ni lazima kupigwe nini? Kura.

Njambo la pili lingine lenye ningefanya kupiga kura nitalieleza tukija kwenye viama vya siasa. Sehemu ya pili ya huduma ya uchaguzi. Tumezungumzia vile hii tume ya uchaguzi itakavyo undwa, tumezungumzia habari ya majikumu ya tume uchaguzi. Tumeiongeza jukumu lingine moja. Tumesema tume la uchaguzi ndiyo itakuwa na wajibu wa jusajiri vyama vya kisiasa. Kwani hao ndiyo wenye kuhusiana na vyama vya kisiasa wakati wakupiga.?

**Audience: silence**

**Com. Salome Muigai:** Wakupiga kura. Hao ndiyo wenye wanajua vyama vipi zinakuwa na fujo. Vyama vipi zinavyo fanya vizuri ama zisipofanya vizuri. Sasa badala ya hao kuenda kuwambia tume lingine kuwa chama hiki kimefanya hivi ama vile wakati wa kura watakuwa wenyewe ndiyo wenye kusajirisha ama kutosajirisha nini? Vyama vya kisiasa. Tumesema pia kuwa hii tume itapunguzwa, itakuwa na watu wasiopunguwa watu nane lakini pia watu wasiozidi watu kumi kwenye hiyo tume ya upigaji wa kura.

Tuemsema pia tume ya uchaguzi ukienda kwenye uchaguzi wa kwanza tuataenda na tuma yenye itakuwako kabla haijabadilishwa lakini baada ya siku tisaine itawahitaji kuwa wamekamilisha habari ya hiyo uchaguzi na wakati huo itakuwa nafasi tosha ya kwenda tume pia kwenye makao yake. Tumeeleza nani atakaye kuwa mfanyi kazi wa tume ya uchaguzi na pia tumeeleza habari ya mipaka ya maeneo ya bunge.

Sehemu ya tatu ni vyama via kisiasa. Tumesema kuna haki ya kuunda chama cha kisiasa. Kila mtu ana haki ya kuunda chama cha kisiasa. Tumesema habari ya wajibu na majikumu ya vyama vya kisiasa. Kuwa vyama vya kisiasa mbali na kuendeleza maoni yao wenyewe pia itakuwa kuwaunganisha wananchi. Tumesema pia nani atakayeweza kusajiri vyama vya kisiasa na tumesema utahitaji kuhitimu vipi ili uweze kuchaguliwa kama chama cha kisiasa. Tumesema kuwa chama cha kisiasa pia kitakuwa na hali ya kuwa shirika. Na tumezungumzia hali ya utajiri na ukutwaji za kutupiliwa mbali ya hivi vyama. Tumezungumzia pia zile vyama vya kisiasa vitakavyo pata fedha zao. Tumetekeleza kuwa ama tumependekeza, (kiswahili cha weza kuisha mtu akichoka) vile vyama zitakachopata pesa zoa na tumesema kuwa vyama vyenye kufuata condition, condition ni nini?

**Audience:** masharti

**Com. Salome Muigai:** Masharti fulani, zitapatiwa pesa za uma, ili tuwe na kiwanja kilicho fanya nini? Kilicho sawa kwa kila mtu, kupiga huu mpira. Wakati huu tunaona tuliambiwa na watu wengi kuwa inaonekana kama hiki kiwanja kimeinuka sana

upande mmoja. Kwa hivyo yule mwenye kimeinukia upande wake akipiga mpira kutoka upande huo unaenda moja kwa moja kwa goal ya mwingine. Fiti zingine kubwa sana. Kwa hivyo sasa tungetaka kuufanya huo uwanja kuwa sawa. Na tumesema kwa kufanya hivi lazima vyama vya siasa vipatiwe pesa za uma. Lakini tumesema kuna mashariti fulani. Sharti la kwanza ni lazima kiwe ni chama cha kitaifa. Tutahakikisha ni chama cha kitaifa vipi? Kisha kuwa na jamii zote ama jamii zenye ziko Kenya, na pia kikuwe kimepigiwa kura ya 3% ya tatu kwa mia. Kwa hivyo vyama tulivyo nazo sasa zenye ni ngapi?

**Audience: (inaudible)**

**Com. Salome Muigai:** Tunavyama zaidi hamsini sasa zenye zimehajiriwa, nyingi zake zitaangushwa na mtihani wakuwa na 3% ya nini? Ya kura. Kwa hivyo zikitaka pesa za uma ni lazima zifanye bidii kutafuta nini? Wafuasi wake, ama zinungane na vyama vingine. Tumezungumzia pia habari ya mathumumi ya hizi pesa na tena zingine za siasa via kisiasa tumesema watu ngapi watakubaliwa kuchangia vyama na watakubalishwa pesa ngapi ili chama kisikuwe ni mali ya kibinafsi na inaweza kumuuzia mwingine kule sokoni. Tumezungumzia sana ni ngapi ya chama na usimamizi wa chama wa hivi vyama. Tumesema ni lazima vyama zionyeshe demokrasia katika chama chenyewe. Hii inamaana gani? Kuwa ni lazima tuone kuwa wale wenye kusimamia vyama ni watu wiofanya nini? Waliojichagua hao wenyewe tu? Waiofanya nini? Waliochaguliwa na watu. Demokrasia lazima iazishe kwenye chama. Chama kisipokuwa na Demokrasia kiazishe Serikali hiyo Serikali itakuwa na Demokrasia? Watakuwa wamejifunza wapi demokrasia, na kabila huanza wapi? Kabila huanza wapi? Charity starts at home.

**Audience:** home

**Com. Salome Muigai:** Na home ya Serikali ni wapi?

**Audience:** ni chama

**Com. Salome Muigai:** Ni vyama vya siasa. Kwa hivyo ni lazima tuagalie vyama vya siasa na kuhakikisha kuwa zinaundwa kwa yale maadili yetu. You remember our malengo yetu yenye tulizugumzia ya kidemokrasia. Lazima pia vyama nazo ziwe zinafuatia hayo maongozi. Tumezungumzia kuwa vyama hazitakubaliwa kutumia mali ya uma kuendeleza mambo yao ama kufanya campaign zao. Na hiyo sehemu ya tatu ya sura ya sita tafathali soma vizuri utaona sheria zenye tumeweka.

Sura ya saba inazungumzia habari ya sheria, sehemu ya kwanza ni bunge. Tutaunda bunge yenye inawajibu fulani, nitazungumzia. Tutazunmzia pia kuelimishwa kwa uteuti wa bunge na tutazungumzia pia ithini ya matumizi ya fedha na bunge. Jambo moja tu ningetaka kugusia kwenye habari ya bunge ni kuwa tutakuwa na bunge yenye vikao viwili. Bunge ya kawaida kama vile tunavyo ielewa leo, lakini pia tutakuwa na bunge/kikao cha Taifa, lenye litawahusisha mtu mmoja kutoka kwa kila wilaya. Wakati hii tuna wilaya ngapi?

**Audience: (inaudible)**

**Com. Salome Muigai:** 72, basi hiyo nabari na zaidi ya hiyo kutakuwa na watu mia moja kwa hivyo tutakuwa na kina mama

30 kwenye hiyo kikao cha pili cha baraza ya Taifa. Watu wengi wanauliza kwa nini munataka kuwa na kikao kingine. Tuliambiwa kila mahali tulienda watu walitaka kikao cha baraza ya kitaifa. Walitaka kikao cha pili cha bunge. Lakini zaidi ya hiyo bunge iliyoko sasa hii yenye tunaielewa tumeipa kazi nyingi sana. Kama kuangalia watu wenye wameteuliwa kufanya kazi bali bali. Tumesema lazima bunge ihithimishe nini? Hao watu. Lakini mbunge yenyewe pia isipopata mtu wakuiangalia si pia itasahao kuwa na uwangalifu. Kwa hivyo hili ni baraza la Taifa kazi ingine yake itakuwa kuikalia macho nini? Bunge. Nayo bunge isizidi sana. Kwa hivyo itakuwa hii ni moja ya checks and balances, ya kuangalia tumempa mamlaka kubwa hii bunge lakini pia nayo ina mtu mwenye kuitazamia kusema kwamba hii mumefanya ni mazuri lakini hiyo tafadhali chunguzeni tena.

Sehemu ya pili ni muda ya wanachama wa bunge. Tumezungumzie habari ya muda wa bunge, wanachama wa baraza la Taifa, ndiyo nimezungumzia. Wanachama wa Baraza la Wabunge, Wanachama kushiriki kusahili na kutosahili kuchaguliwa kuwasilikisha kina mama ama wanawake kwenye bunge. Kuchaguliwa kwa wabunge na waamu ya bunge afisini, na vile mwana bunge anaweza kufutwa. Mambo mawili tu ningetaka kuwekea mkazo kwenye haya.

Tumesema kuwa mulituambia katika kila pahali yenye tualienda kuwa tunataka mbunge mwenye kuelewa. Kwa hivyo kwa hii Katiba mpya imesema kuwa mbunge atakuwa na masomo fulani. Na atakuwa na masomo yakufikia kidatu cha inne. Lakini pia mulituambia hiyo haitoshi. Tunataka kujua mbunge amehitimu kwa masomo na mtaalama lakini mbali na hiyo pia tunataka akuwe mwenye tabia nzuri. Kwa hivyo kutakuwa na kikao maalum chenye kitachunguza kila mtu mwenye atakaye takakuwa mbunge.

Jambo la pili, tulieleza kuwa kuajiri mtu tangu miaka tano awe anatakiwa mshahara akiwa anafanya kazi ama hafanyi ni mda mrefu sana. Kwa hivyo Katiba hii mpya imependekeza kuwa kuwe na namna ya kumuajiri mbunge na nani wenye kumuajiri mbunge? Ni nyiyi, basi na nyinyi mpatiwe pia mbinu za kumfuta huyu mbunge asipofanya kazi yake kabla ya miaka tano. Kwa hivyo mukisoma hiyo sura mutaona mapendekezo yetu kuhusu kumfuta kazi mbunge ao kumrudisha nyumbani.

Step ya tatu inazungumzia juu ya maafisa wasimamizi na watenda kazi wengine, yani speaker wa hizi nyumba bili za mbunge. Na ufajizaji juu ya baraza la wabunge, usimamizi juu ya Baraza la Taifa na mambo mengine yenye kuhusu usimamizi wa bunge zote mbili.

Sehemu ya inne inazungumzia sheria na utaratibu wa bunge. Matumizi wa uwezo wa kisheria, idini ya Rais na kurejelewa yani vipi mbunge linaweza kuwa na vote of no confidence kwa Rais wa siku hiyo. Maoni mengine ya mjadala zaidi na kujadiliwa na ufundi mmoja na mwingine yani uhusiano kati ya hizo nyumba mbili za mbunge mtazikuta kwenye sura ya nne. Sehemu ya nne katika sura ya saba.

Sehemu ya tano ni juu ya kikao taratiba za mbunge, wengi wenu mulieleza kuwa mungetaka mbunge lijisimamie lenyewe kufikiria caledar yao na vile watakavyo fanya kazi zoa. Tafathali angalia hiyo sehemu uone mambo gani tumependekeza. Na

pia mengineo juu ya hiyo ni uhuru wa kuzumgumza na majadiliano katika mbunge, uwezo, na kabila na kinga. Yani protection of the MP's na pia vile sisi kama wananchi ata nyiyi kama uma mutashirikishwa kwenye utawala. Na pia tumeangalia habari ya tume ya huduma za bunge yani Commission and Parliamental Service Commission.

Sura ya nane, inazungumza habari ya mamlaka ya nchi. Sehemu ya kwanza ni kanuni na mfano ya mamlaka ya Taifa. Inazungumzia juu ya kanuni za uwezo ya mamlaka ya nchi na pia mundo wa mamlaka ya Taifa.

Sehemu ya pili ni Rais na Makamu wa Rais. Inazungumzia kuhusu mamlaka ya Rais. Ningependa kukueleza kuwa Katiba hii baado imewacha mamlaka ya Rais mengi sana. Rais ndiyo atakuwa mkuu, ndiyo atakuwa mwajilishi wa bunge. Ndiyo mwenye atatambua waziri mkuu. Rais pia ndiyo atakuwa amri jeshi mkuu. Ndiyo mwenye atakuwa mwana chama, mwenye kiti wa tume ya usalaam ya Taifa. Waziri ndiyo mwenye atakaye chagua mabalozi wetu na kukubali mabalozi wengine wakuje inchini mwetu. Ile jambo moja ingine yenye tumeongeza ni kuwa Rais atawasiliana na watu mbali mbali kuhusu uteuzi mbali mbali. Kwa mfano akiwa anateuwa mahakini ni lazima atawasiliana na tume ya kuwajiri mahakimu. Ikiwa ana teuwa mawaziri watawasiliana na Waziri Mkuu. Na akiwa ni ubalozi, watashauriana na wizara inayofanya hii kazi, tekelezi ya hii kazi. Lakini jikumu la taji za Rais zimebaki zikiwa nyingi na zikiwa bado kamilifu. Jambo lingine lenye tumesema ni kuwa mtu atakeye simama kuwa Rais atasimama na mwenzake yani running mate. Na huyu running mate wakichaguliwa wote wawili huyu running mate ama mwenzake atakuwa Makamu wake aliyechaguliwa moja kwa moja na wananchi. Rais akiwa hayuko ama akiwa na shida fulani huyu makamu wake atasimamia Serikali. Na pia tumesema Rais ndiyo mwenye atakuwa ishara ya mmoja wetu kama Taifa. Pia tumesema Rais atailinda Katiba. Atahakikisha kuwa hii Katiba italindwa vilivyo. Ndiyo ukitaka kuona kazi zingine zote ni za Rais tafathali soma sehemu ya pili ya sura ya nane.

Sehemu ya Tatu ni Waziri Mkuu na Baraza la Mawaziri. Tumesema kuwa Waziri Mkuu atachaguliwa na Rais kutoka kwa chama nacho kitakuwa na wanabunge wengi zaidi katika bunge. Lakini pia tuliambiwa na wananchi kua wakitaka waziri aliye mtaalam. Hawataki kuona mwalimu anapatiwa wizara ya kilimo, askari anapatiwa wizara ya elimu, na daktari anapatiwa wizara ya majeshi. Kwa hivyo pia wananchi walitueleza hivi, mbunge akichaguliwa kuwa waziri hatumuoni mbunge wetu tena mpaka siku ile Rais anakuja kwenye kikao chetu cha bunge ndiyo tutamuona mbunge wetu akiwa yeye ni nani? Ni waziri.

Jambo lingine Wanakenya walituambia ni kuwa mtu mmoja afanye kazi moja. Kuna Wakenya wengi wenye hawana kazi, kwa hivyo mtu mmoja akipata kazi moja, yengine yasiyo nayo Mkenya mwingine. Na kwa jili ya hayo mambo mengi yenye tulielezwa na Wakenya tulionelea na tumependekeza kuwa Waziri Mkuu na manaibu wake wawili watolewe bunge. Lakini hawa mataalam wengine Mawaziri watolewe inje ya mbunge. Na Mbunge akichaguliwa kuwa Waziri ni lazima afanye nini? Ajuhudhuru. Lazima achague kazi moja. Tunaelewa hapo? Hatukuelewa? Wanasiasa wana shida kubwa sana kuwa hawatakuwa Mawaziri na wakuwe Mabunge.

Shida ingine yenye wananchi walitueleza juu ya Mawaziri kutolewa Mbungeni, wanatuambia saa ingine ikiwa jambo lenye

mbunge, akiwa kuna jambo tungetaka atutetee kwa zaki sana kwa Serikali ilioko na Mbunge wetu apate fununu kwamba pengine angechaguliwa kuwa Waziri ananyamaza kimia, hatusimamie tena kama wananchi. Baado anagoja kufanya nini? Kuteuliwa waziri ama waziri msaidizi. Kwa hivyo akiwa huko hatutetei vilivyo kwani yeye anangoja nafasi akiteuliwa Waziri. Kwa hivyo tungetaka Wabunge wachague kama wanataka kuwatetea wananchi ama wanataka kuwa waziri. Ndiyo hii maana tumesema Waziri wote watolewe inje ya Mbunge. Na hiyo pia inatuwezesha kutenganisha mamlaka. Kuna mamlaka ya Executive na nini tena? Legislative, na Judiciary, yani mahakama, bunge, na tawala. Kwa hivyo mtu akiwa tayari yeye ni Mbunge na yule ni Waziri sasa tunaweza kuchanganyisha amekuwa mguu moja uko hapa na ule mwingine uko pahali pengine. Kwa hivyo unakuwa na shida ya kazi gani**.** penye atattea zaidi na mushikaji mawili waswahili husema afanya nini?

**Audience: (inaudible)**

**Com. Salome Muigai:** Sasa ndiyo nataka muelewa kwa nini tunapendekeza Waziri asiwe Mbunge. Ndiyo hii mamlaka mawili ya weze kutengnishwa vilivyo. Na Wabunge waweze kumkazia macho nani? Waziri. Kwani hapo umewacha nafasi ya kuwa Waziri kesho na wakiwa basi wataondoka kwenye Mbunge.

Sasa tunaagalia sura ya Tisa. Hiyo bado ni kuna chapter nzima. Tafadhali soma pole pole nyumbani uweze kuelewa zaidi. Sura ya tisa ni mvumo wa Mahakama na sheria. Sehemu ya kwanza ni mtumo wa mahakama. Tumezungumzia habari ya uwezo wa mahakama, tumezungumzia habari ya Msote wa Mahakama yani viwango mbali mbali, tumezungumzia habari ya uhuru we Mahakama. Tumezungumzia habari ya Mahakama ya juu, yani Supreme Court. Mulitueleza kuwa mungetaka hii nchi ikuwe na Surpeme Court na hiyo tumefanya mapendekezo ya kuiyanzisha. Tumezungumzia mamlaka ya kisheria ya usimamizi wa Mahakama ya juu. Yani Supreme Court itasimamiwa na nani? Mahakama ya Rufani, yani Court of Appeal. Mamlaka ya kisheria ya Mahakama ya Rufari. Mahakama Kuu, ndiyo High Court. Mahakama ya Juu ni Supreme Court. Uteuzi wa majudge tumezugumzia, sifa ya anayestahili kuteuliwa kuwa Judge. Awamu ya Majudge ya ofisini yani Court of Conduct. Kuondolewa ofisini kwa Majudge kutatekelezwa vipi? Mahakama ya kazi tuliozungumzie kuwa tumeipa Mahakama kwa different levels. Hiyo ni kiwango tafauti. Zamani imekuwa ni moja tu sasa tumewapa Mahakama ya viwango tafauti. Tumezungumzea habari ya Utauzi wa makasi, sifa yanayo stahili kuteuliwa makasi na kamati ya maongozi ya korti ya kazi. Majukumu ya tume ya huduma ya uma, tumeizungumzia pia hapo. Na pia tumezumzia tume ya huduma ya mahakama yani Judicial Service Commission. Tumezungumzia pia uteuzi na kuwaondoa maafisa fulani wa Mahakama na pia tumezungumzia mishahara na rusuku za staafu. Jambo moja ningetaka kuzumzia juu ya mishara, tumesema tumeweka tume yenye kushugulikia na kupunguza mishahara ya wafanyi kazi wote wa uma kutokea kwa Rais mpaka kwa yule ili tusipate watu wengi wenye kupata mishara kubwa zaidi. Mtu anapata millioni tano na mwingine anapata shilingi mia tano. Na wakienda Uchumi wanuziwa unga wa jogoo bei gani?

**Audience:** moja

**Com. Salome Muigai:** Bei moja. Sehemu ya pili ni hukumu ya sheria. Tunazungumzia habari ya mwana sheria mkuu na

tunazungumzia habari ya mkurugenzi wa mashtaka ya uma, kwa hivyo tumebadilisha ofisi ya Attoney General zikawa ofisi mbili. Ofisi moja ni yule mkrugenzi mwana sheira Mkuu ambaye ni advisor, advicer ni nani?

**Audience:** Mshaur

**Com. Salome Muigai:** Mshauri Mkuu wa Serikali. Halafu tumekuwa sasa na Judge Mkuu. Kwani wakati mwingine kunakuwa na shida wakati wewe unataka kuistaki Serikali na lazima yule Mshauri Mkuu akuwe ndiyo mwenye atakupa idini ya kustaki mteja wake. Muelewa? Kwa hivyo kuna kuwa na conflict of interest. Tungetaka sasa kuwe na Mshataki Mkuu na pia kuwe na Mwanasheria Mkuu. Pia tungetaka kuwe na Wakili wa Uma ambaye kazi yake ni kutetea mwanchi wa kawaida. Tumezungumzia pia uwezo wa kuhurumia utakuwa mkononi mwanani? Akishuriana na nani?

**Audience:**

**Com. Salome Muigai:** Jambo kuu pengine ni kuwaeleza kuwa …..

Na kukoma kwa wingi ukiwa wewe unakikundi chako mnakutana iwe ni kazini iwe ni kanisani iwe ni kwenye ukoo. Tafadhali ningependa kuwaomba wenye munjua kusoma, kusoma na kuwaelza wale wengine ili kuweza, kuanzisha debate, ili tuoe maoni tafauti. Ukipata maoni tafauti tafaadhali tumekueleza delegates zenu uwaone na ueleze ile mabadiliko yenye tafadhali mungetaka kuyaona.

Lakini kabla ya hapo tuende kwa sehemu ya tatu, yenye inazunbumzia taluma ya Serikali. Hiyo inazungumzia kwenye Public Service Commision. Sura ya kumi inazungumzia upunguzaji na utambazaji wa madaraka. Sehemu ya kwanza ni kanuni na malengo ya ukuzaji na utambazaji wa madaraka, yani Centralization ili utawala na madaraka ya wafikie wananchi pale wanapokaa. Na sehemu ya pili inazungumza juu ya kanuni za jumla. Sehemu ya pili inazungumzia utaratibu wa kupungunza na kutapanza madaraka, kanuni za Serikali iliyo takazwa na madaraka yani devolution. Tunataka mulitueleza kwa wingi kuwa mungetaka Serikali ya Nairobi iletwe karibu nanyi, yani Serikali iwe tu ni kule Nairobi lakini Serikali ije karibu na nyinyi. Kwa hivyo tumeweka viwango vya Serikali kutakuwa na Serikali ya kijiji, kutakuwa na Serikali ya kasha yani Location. Kutakuwa na Serikali ya Wilaya, na pia Serikali ya mkoa. Ningetaka kuzungumzia kidogo kuhusu Serikali ya Wilaya. Kila Wilaya itakuwa na Serikali yake. Itakuwa na bunge ndogo hapo na hiyo bunge ama hiyo Serikali itakuwa na haki ya kufanya mambo mawili. Ya kufunya Sheria zenye muhimu kwenye hiyo Wilaya. Pia itakuwa na uwezo wa kutosha ushuru wa kuweza kuendeleza mambo yake katika Wilaya. Kitu moja kina tafauti kidogo imetuongezea na siada na vile tulivyoambiwa na wananchi ni kuwa wangetaka kuona linkeage, linkeage ni nini?

**Audience:** uhusiano

**Com. Salome Muigai:** Uhusiano. Kati ya utoaji wa ushuru na huduma zenye wanataka. Kwa hivyo wananchi watosha ushuru wange taka kuona uhusiano kati ya huo ushuru na ile huduma yenye inafanya nini? Wapewa. Na hii pia itawapa uwezo wa kuweza kulinganisha.

Sehemu za tatu, ni uwezo wa Serikali, zilipochapaziwa madaraka na mahusiano ya Serikali. Kwanza ni uwezo wa Serikali ya Wilaya itakuwa na uwezo gani? Nimeeleza kwa kifupi fupi juu ya hiyo. Kutakuwa na zaidi kutosha. Na pia majukumu ya utawala wa mkoa. Jukumu kubwa ya utawala ya mkoa utakuwa ni co-ordination. Co-ordination ni nini? Kushirikisha. Kushirikisha Wilaya zake. Yani kwa mfano, kama Rift Valley itakuwa bado ni mkoa mmoja watu wa Uwasingishu watakuwa na mahindi zaidi ya yale wanaweza kutumia sivyo? Ukienda mahali kama Kajiado watakuwa hawana pengine chakula yakuwatekeleza, sivyo? Itakuwa kazi ya Serikali ya mkoa kupata kutafutia watu wa mkoa ya Uwasingishu, soko katika Wilaya gani? Wilaya ya Kajiado. Na pia watu wa Kajiado wakiwa pia nao wananyama za ziada watatafutia watu wa Kajiado soko katika Wilaya ya Uwasingishu yani that co-ordination. Kutakuwa katika hiyo mamlaka ya kuwezesha wilaya tofauti kuwasiliana vilivyo. Pia tumezungumzia habari ya Serikali za District kama mitaa, County Council, na part yake itakuwa ipi na itakuwa na uhusiano gani na Serikali za Wilaya. Tungezungumzia pia habari ya pataji katika mamlaka yaliosababiwa madaraka. Pia tumezungumzia kifalme ya fedha. Fedha gani zitatoka wapi za kutumiwa kwenye kiwango kipi cha utawala. Tumezungumzia pia habari ya tume ya fedha na Serikali ya masinani na ugawaji wa raslimali za Taifa. Yani uhusiano kati ya Serikali ya Taifa na Serikali za mkoa na pia kuendelea tu mpaka Wilayani na vijijini na kata. Sana sana nikweleweke kuwa mambo yote ya Wilaya itakuja moja kwa moja kwa Wilaya. Hiyo ni jambo lenye ninge ni vizuri kuielewa vilivyo. Kuelewa Wilaya itakuwa na jukumu lipi na siku gani itatakikana kwenye hii Serikali yenye itakuwa kwa kiwango hicho.

Tunzungumzia pia masharti ya kisheria ya kizazi wa utangazaji wa madaraka na hiyo sura inamalizia kwa ufafanuni kwa hayo mambo yote.

Sura ya kumi na moja inazungumzia habari ya Arhi na mali**.** Mwanzo inasema mkumbo wa fedha ina afya, yani land quality. Pia inazungumzia juu ya umiliki wa arthi. Tutamiliki vipi arthi zetu. Inazungumzia pia habari ya uamulishaji wa arthi na awani wa arthi. The situation of land ownership and the tenure. Ulinzi wa mali katika arthi pia umezungumziawa na pia kuanzisha tume ya Kitaifa ya Arithi. Kwa nini tumefikiria kuanzisha tume la arthi, ni kwa sababu maswala ya arthi katika hii inch ni maswala mengi na magumu. Tuliangalia kama tume tukaona wakati mfupi tuliyo nao hatungeweza kuufikiria haya maswali na kuyatatua. Kwa hivyo vile tumefanya ni kuweka kwenye Katiba kuwa kutakuwa na Tume ya Taifa itakayoangalia maswala ya arhti kwa muda mrefu na kujaribu kuyaelewa na kujaribu kuyatatua ili kila mwananchi wa Kenya askie kuwa haki yake imestabiwa na imelindwa. Jambo moja tu hii Katiba mpya inasema ni kuwa haitasimamia na haitalinda arthi yenye haikupatikana kihalali. Katiba ni sheria sivyo? Kwa hivyo Katiba haiwezi kuplani mambo inayofanyika ki nini?

**Audience:** kinyume

**Com. Salome Muigai:** kihalali. Kama mambo imefanyika kinyume cha sheria Katiba haitaweza kusimamia.

Sura ya kumi na mbili, nyinyi mlisema hamtaki break, mimi naomba break ya dakika moja nikunyue maji na nipumzishe koo. Re-act kwa mwenzako. Uliza kidogo kwa dakika chache, Nimekubali ndiyo nipumzishe sauti kidogo halafu tutaendelea.

**Speaker:** Naan yani nathani karibuni katika utumbuizaji hii leo hapa kuna mtangazaji na pia kuna mtu ambaye ataweza kuongea kama Rais lakini aki support Katiba.

**Com. Salome Muigai**: Excuse me, because this are two venue to handicap process let me not allow that. Let us continue with our meeting. Tuendelee na mkutano wetu. Excuse me can we go on with our meeting, tafadhali. Tuanze mkutano tena, I would like to call to watch this, watu wengine wangetak kutumbuizwe lakini nimeona kuwa afadhali tuendelee na mkutano wetu tukimaliza ikiwa bado tunawakati tunaweza kuwapa watu wenye kutumbuiza. Kwani tuko sura ya kumi na mbili na bado tunaendelea mpaka sura ishirini.

Sura ya kumi na mbili, inazungumzia mazingira na majasili. Tafadhali muniambie mukiwa tayari.

**Audience:** Tuko tayari

**Com. Salome Muigai:** Asante. Ninasema kuwa sura ya kumi na mbili inazungumzia mazingara na majasili. Inazungumzia ulinzi wa mazingara na pia kuwa tutakuwa na tume ya kitaifa ya usimamizi ya mazingara. Tunaangalia pia juu ya utekelezaji wa haki za mazingira. Na pia sheria za mazingira. Jambo moja yenye ningetaka kuelezea hapa ni kuwa tume itakuwa na watu tafauti na jamii tafuti kuwa wenyewe walikuwa na utamadini wao kuangalia mazingira na sasa tungetaka kuendelea haya. Hii utamaduni kwenye Katiba ili watu na jamii iweze kuagalia mazingira yao.

Sura ya kumi na tatu, inazungumza juu ya fedha za uma na usimamizi wa mapato. Ina anzia kwa kuzungumzia kanuni na malengo ya pesa za uma na usimamizi wa mapato. Inaendelea kuzungumzia juu ya utoaji. Tafadhali utakapo kuwa tayari unielezee. Inazungumzia habari ya utoaji wa kodi, inazungumzia juu ya mkoa mkuu wa fedha za uma. Na inazungumzia juu ya utoawaji wa pesa kutoka huko ukoo wa pesa za uma. Inazungumzia juu ya mfuko wa zarura, yani Constituency and how constituency with money. Kutoshwa kwa mfuko wa fedha za Serikali na pia sheria za matumizi ya hizo fedha. Inazungumzia juu ya uwezo wa Serikali kuomba ama kukopa. Wakati huu tunarudisha bunge kufikiria fedha gani zinahitaji kukopwa kutoka nje. Kwani mbunge akizungumza anazungumzia kumuakilisha nani?

**Audience:** mwananchi

**Com. Salome Muigai:** Mwananchi nini? Pesa zikikopwa zinalipwa na nani? Na mwananchi kwa hivyo tunataka mwananchi akuwe na sauti kwenye ukopaji wa hizo pesa. Tunataka pia kufikiria habari ya deni la uma na habari ya Banki Kuu ya Kenya. Tunaweka kwenye Katiba wajibu wa Benki Kuu na pia uchaguzi wa budgeti na Katibu Mkuu. Mkaguzi wa budgeti na Katibu Mkuu hii ilikuwa ofisi moja ya auditor general lakini wananchi wanatuambia auditor general anafanya kazi nzuri sana lakini kitambo afunge boma inakuwa ngombe ameshafanya nini?

**Audience: (inaudible)**

**Com. Salome Muigai:** Ameshafunguliwa na akaenda. Boma ishafunguliwa ngombe anondoka. Nyuma yake ndiyo Katibu

Mkuu anakuja anatwambia munajua fulani alifungua boma, ndiyo ngombe akafanya nini? Akatoka. Sasa tunataka mkaguzi wa budgeti, mwenye atatuambia boma karibu ifunguliwe ili tumwambie, kubali ama usikubali ifunguliwe. Yani akuwe kuangalia mambo kabla haijaharibika. Halafu, Muhasibu Mkuu atueleze matumizi ya pesa ilifikia wapi mwishowe. Nataka pia kujua habari ya kuondolewa ofisini ya hawa wawili na hesabu na ukagusi wa hesabu. Tunataka pia kuanzisha Baraza la uchumi wa jamii yani committee or economic and social cultural yenye itasimamia itatueleza kabla hatujafika taabani, itaujulisha tukiendelea kufanya A, B,C tutaharibikiwa na mambo. Hatuekewi kabla hatujafanya nini? Hatujafika kule. Kwani wakati huu tunajua tuko tabaani wakati tayari tumefikia huko. Tunataka Economic Council that will warn us that we are getting into problems before we get there. Na pia nimeeleza kuwa kwa mara ya kwanza hii Katiba inasema wewe mwananchi una haki ya kulinganisha kodi yako na huduma zenye unapata. Sura ya kumi na nne inazungumzia huduma za uma.

Sehemu ya kwanza inazungumza juu ya ufamizi wa uma. Inazungumzia habari ya tume ya huduma ya uma, Public Service Commision. Inazungumzia mamlaka ya wajibu wake. Inazungumzia vile hii afisi atakapoanzishwa. Inazungumza juu ya uteuzi wa maafisi wa uma. Watu watateuliwa aje kufanya kazi tafauti. Watateuliwa na nani? Na itawabidi kuwa na umri mgani ndiyo wateuliwe. Inazungumza juu ya ulinzi wa maafisa wa uma na ndiyo sehemu ya pili inazungumza juu ya huduma ya polisi wa Kenya. Kila pahali yenye tulienda wananchi walilalamika kuwa polisi wanapokuja juwajiri watu watakao ungana na idara ya polisi. Watoto wenu watakimbia, wanafua nguo, wanafanyishwa hivi na vile lakini mwishowe hatukuoni wakiajiliwa. Kwa hivyo leo tumeweka huduma ya polisi ili hii huduma itaieleza bunge umeajiri polisi wangapi na imewajiri kutoka wapi katika Kenya. Tumezungumzia juu za kanuni za hii nchi na wajibu za hili shirika kuazishwa kwa huduma ya polisi wa Kenya na uteuzi wa Commissioner wa huduma ya polisi ya Kenya. Hii sasa imekuwa ni ofisi yenye itakuwa ya Kikatiba.

Sehemu ya tatu, nimezungumzia juu ya huduma ya Kenya ya kurekebisha tabia, yani freedom. Inazungumzia kanuni na malengo na kuhakikisha huduma ya Kenya ya kurekebisha tabia. Inazungumzia pia uteuzi wa ujenzi wa wakulima wa Kenya na kurekebisha tabia na sehemu ya inne inazunzumzia habari ya ufafanuzi ya mambo yote ya hiyo sura.

Sura ya kumi na tano, inazungumzia kikosi cha ulinzi na usalama wa Taifa. Inazunmzia kanuni na majikumu ya ulinzi wa mktaba wa Taifa kuanzisha baraza la ulinzi wa Taifa. Majikumu ya Baraza na Usalama ya Kitaifa na kikosi vya ulinzi wa usalaama wa Taifa. Inazungumzia pia makamandos. Makamanda wa ulinzi wa Taifa.

Sura ya kumi na sita, inazungumza juu ya uongozaji na uwaminifu. Wananchi wengi walituambia tumezungumzia mbeleni kuwa watueleza haitoshi kuwa mtu ana elimu. Haitoshi kuwa mtu ana mali, hiyo haimfanyi kuwa kiongozi. Tungetaka ya ziada. Na kwa njia hii tumekuwa na kutumika kwa tumeelezea juu ya uongozi na uwaminifu na kutumika kwa hii sura majukumu ya ulinzi yenye itaanzishwa na hii sura.

Sura ya kumi na saba, ni tume ya Katiba na afisi za Katiba, yani Constitutional offices and High Commission. Ya kwanza ni kanuni zitakazo tumika na tume zote, yani tumezote zenye zitaanzishwa kwa Kikatiba zitakuwa tume zitakuwa za namna gani.

Halafu malengo ya uhuru wa hizi tume kushirikiswa kwa hizi tume kwa viombo kwenye hiyo tume ama hizo tume. Majukumu ya jumla ya hizi tume. Na kumbu-kumbu za hizi tume. Vile watu wataondolewa kutoka kwa cheo za hizi tume na mifuko ya fedha ya hizi tume. Tarifa za kwanza na linginezo yani kila tume yenye imechaguliwa na Katiba lazima itaweza kutoa tarifa ya mwaka kwa bunge kueleza kazi yetu hii imefikishwa hapa, hapa ndiyo hatujafika, na tuja settle hizi, na tuna matarajio ya kuwa tukifika pahali fulani tumekuwa tumefikisha hii kazi wapi. Sababu hii ni kwa sababu watu wengi kila mahali tulienda walilalamika kuwa tume nyingi zinateuliwa zinatumia mali ya uma lakini mwishowe matokeo ya hizo tume haitumikani kwa wananchi. Kwa hivyo tumesema hizi tume zikitoa matokea yao kwenye bunge tutayasikia na wanafunzi wetu watasikia na sisi pia kwani tumesema kwenye Katiba hii pia kuwa habari zote zenye zitafanyika kwenye bunge zitaletwa na vyombo vya habari moja kwa moja kwa wananchi. Kwa hivyo wakati hii habari inapopatiwa bunge na vipi wananchi twaweza kuyasikia moja kwa moja.

Tutakuwa na tume ya haki na binadam na haki za kitawala niliwaeleza kazi yake nyingi itakuwa kuangalia haki za binadamu ama haki za wananchi. Itakuwa ikiangalia sana habari ya sura ya tatu. Sura ya tatu ndiyo yenye haki. Angalia tuone, zilikuwa sura ngapi zenyewe.

**Audience:** Ya tano

**Com. Salome Muigai:** kwa hivyo kazi kubwa ya hiyo tume itakuwa kuandalia habari ya sura ya tano. Kutakuwa pia na tume za uadhilifu na uwaminifu. Hii ndiyo tume yenye itachunguza viongozi wote katika viwango vyote. Kuagalia kuwa ni wapi kwenye uwathilifu mwema. Tume ya mshahara na malipo nimeelze kazi yake, itakuwa kuangalia kila mtu amepatiwa mshahara mwenye kumuezesha kukaa maisha yenye nini? Nyinyi mnataka kuishi maisha yenye nini?

**Audience:** furaha, heshima

**Com. Salome Muigai:** Na pia kutakuwa na tume ya huduma kwa walimu. Hiyo tumeiweka kwenye Katiba. Hiyo ni Teachers Service Commission. Na pia kutakuwa na Tume ya Katiba. Hii tume itafanya kazi kwa miaka mitano tu halafu tunaifungia. Katika hiyo miaka mitano ni kazi yake kuagalia kuona sheria za bunge zimegeuzwa kuambatana na Katiba mpya. Na pia kuangalia sehemu zote zitakazo tuwezesha kueneza hii Katiba mpya. Pia tutakuwa na ofisi ya Kikatiba, afisi za Kikatiba na pia hizo zimeshugulikia kwenye hii sura ya kumi ya na saba.

Sura ya kumi na nane, kubadilisha Katiba. Ile mambo yenye itatuwezesha kubadilisha Katiba bila pengu yani transition. Kutoka kwa Katiba ile iliyoko sasa kwenda kwa Katiba mpya. Hii imeweka mbinu tofauti zenye zitawezesha smooth transition, hiyo ni nini? Mabadiliko yenye nini? Rahisi na yalio nini?

**Audience:** (**inaudible)**

**Com. Salome Muigai:** Mabadiliko kwa urahisi. Babadiliko bila pengo. Tukimalizia pingu hii kwa jina imesema tumalize na kumbe tayari hatujaweka nini? Kitu kile kipya kwa mfano tume ya uchaguzi, tumesema tume ya uchaguzi yenye itakuweko

tumesema ni lazima ipeleke, tupeleke kwa uchaguzi wa kwanza wa Katiba ile mpya. Kwani tukisema hivyo tume imemaliza kazi yake kwa hii tume mpya tutakuwa na nini? Na pengo. There will be a gap, okay. We are looking for a way that will give us a peaceful and harmonious transition from one section to the other. Another example is for example tumesema kwenye Urais ikwa watu hawataki Rais aliye na zaidi ya miaka sabini. Lakini tumesema tayari kuna watu wenye wako kwenye hiyo process ya uchaguzi wenye wako na miaka zaidi ya sabini. Kwa hivyo tungefanya uchaguzi wa kwanza na hawa watu lakini uchaguzi wa pili kwenye hii Katiba mpya haitakuwa na watu wenye zaidi ya miaka sabini. So that we have a smooth transition. Kuna mambo mengi ile ya kuwekewa manani kwenye hiyo sura, tafathali yatazame huenda ikawa tayari yamezungumzia ile mambo yenye unaona ugumu wake kwenye hii Katiba. That is a useful section to look at. Tumezungumza juu ya mabadiliko ya Katiba, mabadilisho ya Bunge na haki ya utiifu.

Sura ya kumi na tisa inazungumzia juu ya ufafanuzi yani translation (madam ukipeyana gazetti kila moja unachukua unapeleka nje, tutamaliziwa na gazetti na zitakuwa zikienda na watu wenye baado wako kwenye mkutano wetu hawana. Ningetaka kukuomba hiyo iwe ya mwisho). If you keep on giving the people who are not ready to come to the meeting, you are stopping them from coming to our meeting.

Sorry ya ishirini ndiyo yenye utaratibu wa transition ya mabadiliko. Sura ya kumi na nane. Ni badiliko ya Katiba. Amendment to the Constitution ndiyo sura ya kumi na nane. Ya ishirini ndiyo yenye Transition calling base ama kitendo zile kanuni za mpito au matokeo ili tuweze kusikia kutoka kwa Katiba moja kwenda kwa ingine. Na kwa hayo mengi sana ningetaka kuwa shukuru kwa kusikiliza kwa makini na kwa utulivu. Na sasa ningetaka tuende kwa kiwango kingine cha mkutano huu. Na hiki kiwango ni cha kuuliza maswali. Tutachukua maswali kama kumi hivi, kuanzia hapa watu kumi ili na mimi nipate nafasi ya kupumzika kama baado munaandika maswali chini halafu mutayajibu pamaoja. Kuna maswali mawili ningetaka tujibu kabla hamjauliza.

Swali la kwanza ni kuwa je bunge ikivunjwa kutakuwa vipi? Kazi ya tume nikutengeneza Katiba, kazi ya kuvunja bunge ni kazi ya Rais. Kwa hivyo mimi kazi yangu ni kuzungumzia habari ya Katiba leo. Swali hilo lingine nalo litaulizwa kwa mtu ambaye ataweza kulijibu. Lakini jambo moja tu ningelitaka kusema. Tukimaliza hapa, hatua ya pili kutoka hapa ni kuwa tunaenda mkutano wa kitaifa ama kikao cha kitaifa cha kuzungumzia Katiba. Hiki kikao tutakuwa na wabunge wote, pia na washirika watu kutoka kwa kila Wilaya. Leo tumeona washirika wawili kutoka hapa na nyinyi mnabahati kubwa Uwasingishu kwani baadala ya kuwa na wahsirika watutu munawashirika wa tano. Kuna washirika watatu walioteuliwa kutoka kwa County Council na kuna washirika wengine wawili wameteuliwa na Civil Socieity, yani Vikundi via raia. Kwa hivyo mkoo na watano, ukiwa una jambo lenye unasikia unatafuti kubwa na hii Katiba. Tafathali watafute delegate wako umweleze na umzungumzie mukubaliane kuwa hii ni maoni ya Uwasingishu. Ningetaka kusema hivi, hawaji kujishirikisha hao wenyewe. Wanakuja kuwashirikisha nani?

**Audience:** Wilaya

**Com. Salome Muigai:** Yani hao wanawashirikisha nyinyi. Wilaya sio boundary sio miti ya Uwashingishu ama nyumba ni nini? Ni watu. Kwa hivyo lazima mukubaliane kama mna vikundi muwaulize pake mutakutana waje wasikize maoni yenu ama muandikie ndiyo wajue matakwa ya Uwasingishu ni gani. Ndiyo walete hayo matako. Ninahuzunika kuona wote hawako hapa, lakini kitambo mimi nitembee kwenye zile vikao vingine viwili vy bunge na fikiri nitakuwa nimekutana na wote. Ili kuwaelza kuwa wanaenda kuwakilisha wananchi kwa hivyo ni lazima wasikilize watu wa Uwashingishu wanataka nini? Nitaachia hayo ili muulize maswali.

Jambo lingine nigetaka kueleza leo siku si siku ya maoni. Tulikuja kutoa maoni na tukamaliza. Leo ni wakati wa kuuliza swali ya mambo ile hujaelewa kwenye hii mswaada wa Katiba. Ile yenye ungetaka tupinduwe utaeleza delegate wenu ama utaandika utampa Peter Borr na atatuletea lakini kwa wakati huu ingekuwa vigumu sana mimi kuanza kuchukua maoni ya kubadilisha Mswaada huu kwenye kikao hiki. Munaelewa?

**Audience:** ndiyo

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo muulize maswali yenye itawawezesha kuelewa zaidi huu mswaada ili na nyinyi mkiondoka hapa tafathali mwaeleze wengi wenye hawakuweza kufika hapa. Mukiwa ni daktari, ikiwa ni chama cha walemavu , chama cha wafanyi kazi ikiwa ni chama cha mtaa popote utakapo shiriki na watu hata jamii yako uwaeleze kuhusu hii Katiba ili waweze kutoa maoni yenu. Basi kikao cha Mataifa sisi tunakitarajia kuanzia tarehe ishirini na nane na tunakitarajia kumaliza mwezi mzima lakini Wakenya wakikubaliana kabala ya hayo basi tutamaliza wakati wowote tutakapokubali tumekubaliana. Tukitoka kwa kikao cha Taifa ile mambo yote tutakubaliana yatapelekwa kwa Parliament ili ikiwe Katiba mpya. Bunge ama Parliament inaweza kufanya mambo mawili. Inaweza kukubali huo mswaada amainaweza kukataa. Haijakubalishwa kubadilisha. Ikiwa wabunge wamekuwa katika Constituency Committee, ikiwa wamekuwa ndani katika kikao hiki cha Taifa. Siwamesema yenye walikuwa wakitakata kusema. Basi wakienda kujifungia Parliament ni jambo mawili wakubali yote ama wakatae yote. Wakikubali yote hiyo itakuwa ndiyo Katiba yetu. Wakikataa tutaanza mwanzo tena. Kwa hivyo sisi tunajukumu ya kumuonna Mbunge wetu kabla ya tarehe ishirini na nane na kumueleza tukiwa tumekubaliana na hii mswaada basi tumtume. Tumtume akahakikishe kama ni maoni yetu. Si ni kweli? Sisi wenyewe tukikataana nayo pia tutamtafuta mjumbe wetu tumwambie afanye nini? Aikatae. Kwa hivyo tunajukumu ya kuwa tumemuona mjumbe wetu kwani mjumbe wetu ni mfanyi kazi wa nani? wetu tu sisi wenyewe. Sasa nitachukua maswali na maswali yangu itakuwa ya kuwaeleza ili muelewe tafathali sio ya kubadilishs. Nitampa Bwana Juma akuwe mwenye kiti wa sehemu hii ya mkutano wetu Bwana Juma.

**Bwana Juma**: Vile amesema mtauliza maswali na kabla hujauliza utakuja hapa mbele na kuweka jina lako katika kitabu hiki na address na sahihi. Tutachukua kwanza watu kumi. Kwa vile Commissioner atachukua maswali kumi kwanza na kuchukua wasia zake na kuchukua watu kumi tena. Kwa hivyo utakuja hapa. Kina mama wako wapi?

**Com. Salome Muigai:** Ni nani kutoka upande hii, ni nani? 1,2,3,4,5 wapi mama mwenye alikuwa na polo hapo nyumba. Basi njoni hapa mbele nyinyi. 7,8,9,10.

**Unita Rop:** Mimi ni Unita Rop. Swali langu la kwanza linahusu haki za walemauu. Haki za walemavu hujafafanua vizuri kwa upande wa employment. Hawaja kuwa clear sana kusema kama mtu ame qualify ama ako na ujuzi ya kuingia pale. Jambo lingine mambo ya exemption from the tax pay, sijaona hapo ndani. Jambo la tatu ni sign language iko lakini nilikuwa nataka iwekwe ya kwamba iwe official language tuseme ati hii wapi, kotini wapi, iwe kila mtu. Yangu ni hayo. Na education tulikuwa tumeonelea ya kwamba tulikuwa tumeongelea mambo ya free education na baado hatujaona pale.

**Daniel Simotwo:** Asante sana madam Commissioner jina langu ni Daniel Simotwo. Mimi ningesema tu refer kwa ile article ambaye inazungumzia mambo ya devolution hiyo ni Act 22 ambapo imesma hi District Government halafu ikasema katika ile subsection clause 2 ya kwamba District and municipalities have the status of district. Halafu katika ile schedule 2 ime list yale madistrict ambazo zinatakikana kuease the district. Kwa hivyo naona kama tuna contradiction hapo kwa sababu kwanza imekubali ya kwamba Municipality should be halafu at the same time imetoa nusu ya districts katika ile second schedule. Kwa hivyo na fikiri, na hii Katiba hajasema kama kuna mambo inaitwa mayor ama nini haijatambua kama kuna Local Authority sijui hapo itakuwa aje?

Jambo lingine ningekuliza ni kama ilie ya Act 266. Ambavyo inaongea juu ya Police Commissioners. Sasa hapo sijui kama ni typing error lakini imesema ya kwamba Commissioner anachaguliwa a term of 10 years. Mimi naona kama ni ukweli ya kwamba ni 10 years. Ningependelea ikuwe shorter than that kama four years or less. Kwa sababu mtu akienda 10 years ni mtu ambaye hajiwezi kwa kazi. Utabaki na mtu for ten years hiyo ni muda mrefu sana.

Jambo lingine ambayo igawaji haijatajwa vizuri ni hii ambayo unasema mawaziri watolewe kutoka nje ya mbunge. Katiba haijasema hawa watu watakuwa ni wanasiasa ama ni watu wanainagaini na wako na job security ya aina gani. Kwa sababu kama hawana job security kuna hatari ya hao kuwa sycophant. Kwa sababu kama umesaidiwa na mtu kuwa Minister utakuwa ukimmwimbia wimbo namna hiyo. Lakini yule mtu amechaguliwa ata anaweza akawacha hiyo kazi na baado anakula mshahara. Kwa hivyo kuna hiyo hatari ya kuweka Cabinet Minister akiwe sycophant.

Jambo la mwisho ningetajia ni kuhusu mahakana. Naona ya kwamba Katiba imetoa institution kama tatu katika Serikali Kuu. Sasa iko Supreme Court, tuko na Court of Appeal na High Court. Nafikiria hii yote sababu gani inakuwa yote inarundishwa katika Serikali Kuu. Ingekuwa vyema kama High Court kungekuwa na devolution ya High Court ili tuweze kupata High Court katika provinces. Hiyo ingesaidia sana kuleta justice karibu na watu.

Halafu ya mwisho madam Commissioner kama vile umetueleza ya kwamba tunajua kweli hii Katiba tunaitaka tufanye uchaguzi katika Katiba mpya lakini jambo ambalo sijui ni kwamba mbunge ikivunjwa hatutakuwa na watu wakwenda kupitisha hii Katiba kwa hivyo kama vile madam Commissioner anasema hiyo sio kazi yao. Sasa ni sisi wananchi tuone ya kwamba Wabunge wetu wasikubali bunge ivunjwe ili tuweze kumaliza hii kazi. Na mimi kama mmoja wao ambao watagombea kiti ninakuhakikishia ya

kwamba atakama Bunge itavunjwa bora tu muongezewe muda mpaka April huko. Sababu wenye watachaguliwa kama itakuwa ni mimi mmoja wao nitakuja kudefend hii Katiba. Asanti sana Madam Commissioner.

**Mwangi Githogo:** Madam Commissioner na wale watu wako hapa jina langu ni moja sina mbili, jina langu ni Mwangi Githogo. Uligusia maneno ya mschana kuolewa, akiolewa na Muhindi, akiolewa na Mzungu anahaki ku

**Speaker:** Katiba mumeweka, utafinya mwafrika maanake sisi kabila yetu waafrika wote. Jana sijatoka nyumba yangu napata akijenga nyumba yake huko, angalitakiwa kujenga nyumba huko. Wote mnamuweka, mimi shule ambao alikuo arudi kwangu, tuwe kukiishi na yeye, hapo haitakuwa nzuri. ***(Clapping)***

Iile lingine, ni vile ulisema maneno ya mipanga ya Bunge, hatujuii kwamba ile ilikwa immeweka tutakuwa tukifanya kazi, I hope utabadilisha, tukiwa tukapata vile ilikuwa zamani, na nilipata ile iliwekwa nyuma, ziliwekwa mingi, na mwananchi inashindwa ni kuchuwa ni wapi atapigia kura, hata wengine watakata kupiga kura maanake anasukumwa pande ingine, bila kujua. Kwa hivyo mngetuhakikishia na kututangazia, constituency fulani inafika mahali fulani, mimi mwananchi, hawezi kupiga kura, lakini sasa mwananchi anakuwa labda ange kaa nyumbani, angekuwa pande hii anarudi pande hii. Saa ya mkubwa hata kama haijakubali kwa mfano moja iko town hii.

Bibi ya councilor, inaweza kuwa nakatwa kidogo kidogo, sasa imerudi councilor mmoja imeweka dunia nzima, na mahali alikuwa akipigia kura, ndio sijiu alitoka wapi? Kwa hivyo hapo mtuelezee ili tueleze mapama, maanake kama hapa town, town yetu ndani, town ya Eldoret hii, tuseme town Eldoret, mimi ni mkaaji wa Eldoret tangu mwaka wa arobanne na sita. Hatuna uwezo wa kuchaguwa mjumbe, maanake tuliambiwa watu inaingishwa kutoka huko wanaingia mpaka town. Ingine inatoka pande ile, inaingia town, mwingine anatoka huko anaingia town, kabila ya mia saba. Sasa tukienda kwa kupiga kura tena ninashindwa, maanake nikifanyi hii, hata mpaka sikuonyeshwa, hiyo nayo itakusumbua sana, Madam Commissioner, uwende ueleze watu wanu maneno ya mipaka, wajaribu kueleza watu kwa kinaga naga na kuandika kwa gazeti ile tujuwe tutaenda wapi. Tuko na mipaka mingi, mimi naona mnataka kufuza wajumbe, ama kuongezwa.

Lile lingine ya mwisho, katika nchi yetu, mjumbe mmoja, anaongoza watu elfu mbili mia tano na tatu, na mwingine, anaongoza watu elfu mia moja, anajuwa kazi mingi hata …..(Inaudible) inakuwa ngumu. Hapo muende mfikirie, maneno kuenda hivyo, kama ni mahali pa watu wengi, mgawa kidogo, huyu anaongoza kidogo na mwingine anoangoza kidogo. Maanake mwingine ata, vile nilisema nilisema vizuri. Wengine ambao walijaza contract na siwajui, hata ningeona wakikuja karibu na sisi, kwa hivyo hiyo Madam, mlifanya vizuri kuongea hivyo. Maanake wengine hatufahamu, asante, sina mengine ni hayo tu.

**Mr. Nicholas Mwendwa:** Jina langu ni Nicholas Mwendwa. Swali langu ni kuhusu devolution chapter 10, hiyo iliulizwa na mwenzangu Eric Chogo, na 222, about municipality, being in the same as district. Or hakusema kwa vitu maandishi, ama yule atachaguliwa, kuongoza serikali ya municipality, atakuwa administrator au mayor the same question kama yangu. Na ile ingine nilikwa nataka kuuliza, ni kama iko pahali tunaweza pata si chaos abit more, about the civic election. Kwa sababu detail ile iko, hapa ni, kidogo sana. Hatuwezi juwa how they are going to be elected and in which manner?

My other point ilikuwa ya constituency, sijui kwa nini Tume iliona ni vizuri kuacha 272 constituencies, na kuko na constituencies zingine kubwa sana, at the moment. Tulifikiria labda hizo zitawanywe halafu viti ya 90 ile istaongezwa kwa kura hii ya chama iwe, ipunguzwe kidogo, maybe 75 or something like that na 15 iwekwe kwa new constituency, that is my question. Thank you.

**Mr. Isaack Kibenei:** Mimi ninaitwa Bwana Isaack Kibenei, kutoka hapa lenges market. Swali yangu mkuwe ni moja. Ya kwanza, ni kuelewa hali hii ya wa mama kutukana wa mama na 30%, lakini tumesema ya kwamba kuna ile report tumeenda through review. Kwa nini kama mama, umepewa equality na wa mama, kama mimi tuseme nataka ya bibi ya …….(Inaudible), si yeye haja ya kumpatia ………(Inaudible) na kung'ang'ania tuone nani ame ngoja tunakubaliana.

Na ingine, mmetuambia ya kwamba, tuende kwa mjumbe wa Parliament, aende aandikishe hii, na dereva yake mwenyewe wa huyo mbunge amesema hii sheria hajaona. Hako kuna possibility kweli? Hii kitu iende kuliwa na huyu Mjumbe wangu ambaye sasa inasemekana, unaona kama hii, kitu si yetu ya wananchi wa Kenya, kutokubaliana, walitupea, na haki yao kuenda ku-withdraw in the Parliament. Maana tuliletewa hapa, tukaongea, kutakubaliana, kwa maoni yetu, kwa hivyo

hatungekubaliana na raia, kama kuna vitu ndogo ndogo, tutaenda wote delegates huko. Sijui katiri refugee waende tu watuletee lakini nahakika ndani ya roho yangu, wale wajumbe wenu, mimi siongee, ………….(Inaudible) kwa wengine wataweza kusikia mimi nimesema mimi napiganga hawa, hapana.

Haya ingine, kama wenzangu wamesema, kwa hivyo wacha hata mimi niseme kidogo. Hii ni haki yetu Katiba ya Kenya, imesemakana wilaya, municipality na kuna kati ya hapa tunataka, itakuwa ni risky sana, ikisemekana, hawa centre iwe kama district, halafu ile watu wengi over district kule, ambayo hatuaja-indicate, Katiba ya nchi yetu mimi, itakuja kuwa na small portion watuchukuwa hiyo district kuwa maana na watakuwa na say, halafu wale wako district hawatakuwa na say. District kama nni wilaya ya Uasin Gishu, hiyo wilaya ya Uasin Gishu iwe kama ni urban council iko town, ichaguliwe na raia wote kama ni mtu, sasa tuseme kama ni mayor, kwa mfano tuseme elders, kwa kama ni mkubwa ata simamia district, katika municipality. Raia wana views, what is wachaguwe huyo mtu mmoja yule atakaekaa napiga mayor, siyo watu wachache watachaguwa. Nafikiri natakiwa nyinyi muende Nairobi, muende mfikirie hii sheria mpya, iwe ya mwananchi wa Kenya, kwa mara ya kwanza it has …..(Inaudible) fourth years kando baada ya Kenya.

**Mr. Robert Mathethe:** Asante sana kwa huu mkutano, mimi kwa majina ni Robert Mathethe, na ningependa, kukuuliza swali moja, na kabla niulize, ningependa kusikia Commissioner wetu hapa kuwa aliuliza, kiwa ni watu hao wameandika hii draft na saa zile Parliament ivunjwa kesho, watafanya nini, mimi nilikuwa naona si vizuri, kwa sababu hii constituency haitakuwa inafanya njia hii vile iko saa hii ndani yake, hii ndiyo sheria ambayo itakuwa ya Parliament, na Parliament itafanya ambayo itakuwa inakuja. Kwa hivyo nyinyi muendelee na kazi yenu hapa hata kama hamjamaliza muangalie. Maoni yangu ilikuwa tu ya friendship, ambayo yule mzee alikuja, kama anakaa akaolewa na yule mwanaume ambaye ameoa na yule na mwanaume ambaye amaoa yeye, akuwe citizen. Hiyo mimi sikuona kwamba inaingia ………..(Inaudible) hii italeta shida kwa sababu huyu sasa akikuja hapa tena, atakuja kuchukua some of our land, ………(Inaudible) hata kama yule mwenye analeta yeye anakuja kununua shamba, akuwe citizen wa hapa, atakuwa anakuja kulumiza wanainchi ……….(Inaudible) hapa.

Ingine ilikuwa juu ya mahari, dakika hii, draft ………….(Inaudible) mumeweka ibakishiwe right ya mwanamke, right ya watoto, right ya watu walemavu, lakini sijui kama mli-assume right ya wanaume, kujua na bahati ………..(Laughter from the

audience). Kwa hivyo naomba pia mimi ni nataka kujuwa kama tuko na right……….(Inaudible) zaidi ya hapo, Katiba, rights of worship and opinion, mlisema kuwa mtu tuwe na uhuru, ……..(Inaudible). Lakini imefika mahali kuna watu ambao hawaoni mambo hawo watoto wake, anaenda ana-practice withcraft, then withcraft anaenda ana practice mpaka anaenda ………..(Inaudible) mwingine. Na sasa mwingine anaemba kuumia na wale wako, na huyu mtu tukipeleka kortini, hakuna sheria inamshitaki, hata kama ungechukuwa hiyo angeku…..(Inaudible) hata mtu anaingia ………..(Inaudible) takaumie, hakuna sheria inatungoja, nikuchukuwa for example, chairmana alipigwa kule Kisii, akapatikana na ile kitu yake, kupelekwa kortini, hakuna sheria ambayo……(Inaudible). Inasemekana ikipatikana na hawo tu kupiga …………..(Inaudible) **Laughter .** Madam Commissioner I may discuss, kwa hivyo hapo pia niliona kuwa, mungeenda kwa kama huyu kuwa tashikwa na …………..(Inaudible). Kwa hivyo ana practice hiyo right yake ………(Inaudible) awe na njia ya kutatua na hata amengojewa. Yangu ni hayo tu. **Clapping.**

**Mr. Zakaria Sifuna:** Basi kwa majina naitwa Zakaria Sifuna. Maswali yangu, itahusu upande wa uchaguzi. Sasa kutokea wakati wa multiparty, kumekuwa na mambo ya kusema swearing, labda area fulani itakuwa ni ya chama fulani. Na hapa katika hii draft, naona ya kwamba, pia tutakuwa tunapitia vyama kura. Sijui kama itapunguza hiyo zoning …………..(Inaudible) na hiyo zining ………..(Inaudible) wakati huo ilikuwa na madhara yake. Kwa hivyo hilo ni swali nimekuwa nalo wasi wasi, moja.

Swala lingine, ni kwamba vyama, pia tutaweza kupata watu wakuwa, kulingana na wingi wa kura zile vyama vimepata, pia tutakuwa na nafasi ya kuchaguwa watu. Kwa hivyo swali langu ni kwamba, hawa watu pia wataenda kwa Bunge la kawaida, ama wanaenda national council ya chini …………..(Inaudible).

Swala lingine, ni kwamba tumeongea juu ya usawa na akina mama, na tunaona ya kwamba, wana nafasi ya one third, kwa hivyo ningependa pia kupata ufafanusi kwamba, hizi nafasi za one third, kwa hivyo ningependa pia kupata ufafanusi kwamba hizi nafasi za one third, watakuwa wanategewa hapa, wanaenda kwa uchaguzi peke yao, ama watakuwa wanafanya, wanaenda kwa uchaguzi hata na wanaume. Asanteni

**Mr. Tonny Kirwa:** Kwa majina naitwa Tonny Kirwa. Kwanza ningetaka kusema ninawapongeza kwa vile mmfanya kazi

ngumu wakati ambao ulikuwa si rahisi kupata draft ambayo imekwisha. Nawapongeza commission kwa kufanya kazi kama hiyo. Kama watu wamekuwa unasema tumeuliza maswali lakini naona kama tunatoa maoni. Kwa hivyo I also agree like the rest. Nataka kuuliza hivi, hamkuona kuwa wimbo wa taifa ni ya maana sana na ni lazima mueke katika katiba.

Swali la pili, ni juu ya Kadhis courts. Je, hamuoni kuwa mkikubali Kadhis courts, ziwekwa katika Katiba, you will open a ponderacle, kwa vile watu ambao ni wa matenebu mengine kama wa Kristo, wahindi, wahindu na wale wanaobudu kienyeji. Wanasema pia tunataka korti zetu katika Katiba.

Jambo la tatu, je, kama mnakubali, two thirds of office, kwa raia, kwa nini msikubali kuwa wajumbe pia wapate two thirds kwa ………..(Inaudible).

Jambo lingine ni kuwa, wakati tunapo piga kura, tunasema mtu akiwa na miaka kuna na nane, anaweza kupiga kura. Lakini wakati mtu anataka kuchaguliwa kuwa Mbunge, mnaanza kubadilisha miaka tena mnasema ni ishirini na moja, ama nina naweza kupiga kura nikiwa na miaka kumi na nane, ni kipindi gani kitafanyika tena siwe nikupigiwa kura tena nikiwa na miaka kumi na nane.

Ukiona Katiba ambao itakuja sasa hivi, ni jambo, naogopa kuwa huenda tukapata Katiba ambayo inafanana na ile, Katiba ile ya ancestic (zamani). Sura yake inafanana na hapo Parliament. Na wakati nilikuwa hapo nikitoa maoni hiyo ni kuwa, ingekuwa vizuri kama tungeweza kurembesha, Katiba yetu. Ndio itabaki kama ile ya zamani ile haina sura. Mtu ili ukiona ina-act upande saa zingine zinafanana. Ama mtajaribu kurembesha kidogo, afanane ndio vizuri. Na nikiwa hapo pia nitasema ile organization ya content ya Katiba, kidogo inaleta shida, kwa sababu unaposoma, unasikia dini ya kwanza ni chapter one. Ukishika zile act of Parliament, tena unasikia ni chapter one of the citizens of legislation. Je, hamuoni kuwa wakati wa raia watakushika Katiba, na kushika zile zeria zingine,

Act of Parliament, watakuwa na shida. Kwa sababu hiyo ni Act Chapter three, Katiba inasema Chapter one of the Constitution of Kenya, sasa mtu anaweza akafikiria, ile chapter one ya constitution ya Kenya, ni ile act chapter one ya Act of Parliament. Asante.

**Ms. Grace Mugo:** Madam Commissioner na wengine wanzangu, hamjombo ni

**Speaker:** …………….(Inaudible)

**Ms. Grace Mugo:** Kwa majina ni Grace Mugo na ningependa kuuliza maswali matatu. Hasa ya kwanza ningeanza na ile chapter 5 ya hii constitution mpya, imesemekana ya kuwa, every person has denied the right to live in the republic. Therefore, for my case ni hii, still bado wanakuwa na wandikia mambo ya passport isipokuwa ndio tumekuwa tunachukuliwa sana.

Ya pili, imetokea kuwa tutakuwa tunafanya uchaguzi mara mbili, ya MP na maybe ya party. Now, I wanted to know kwa hiyo party, watakuwa wana elect people or they be nominated. Na at what percentage will women be elected or appointed sawa?

Sasa nilikuwa ninataka kusema kwa hiyo kwa hiyo pia nilikuwa nataka kujuwa registering of votes, We take as the event of the day. We have seen that this voting is

**Speaker:** ………………(**Inaudible). (intersection)**

**Ms. Grace Mugo:** Yaah, yaah, it is between the votes in the polling station in the Constituency who are taking this vote?. Now, what have you done to that point? First you have said the constitution protect cancer, it protects celebral cancer.. Mimi nimewahi kusikia that having that, or yaani, hakutaja.

**Mr. William Serem:** Mimi kwa majina ni William Serem. Ninayo maswali machache hapa, ambayo Madam Commissioner will be able. Swali la kwanza linahusu, ulisema ya kwamba kwa Katiba, tusema kwa Katiba, imetajwa ya kwamba, President anapo wania udhasafa huo wa presidency, yeye hatakikani kuwa mwana chama wa chama chochote, lakini katika uteuzi wake, kuwa nominated, itaandikwa ya kwamba, awe anapendekezwa ama anakuwa nominated na chama fulani. Je, hiyo huoni kuwa italeta shida kwa sababu mtu huyu alichaguliwa na chama fulani, atakuwa na raia upande ule, ambako alichaguliwa.

Ya pili,

**Com. Salome Waigai:** …………..(Inaudible).

**Mr. William Serem:** Asante, la pili ni kuhusu uchaguzi ambao ni imeandikwa ya kwamba, imekuwa proportional system. Je, huoni kuwa hii proportional system ya kugawana madaraka kama jinsi vile those za wananchi MP, na hawo wanawake Mp, kuwa utaleta unyanyasaji kwa njia fulani, kwa maana watakuwa wakiakilisha masilahi ya watu binafsi ama uchaguzi fulani. Ilihali katika uchaguzi, umechaguwa mtu ambaye anaenda kuakilisha maslahi ya vikundi vyote.

**Com. Salome Waigai:** ……………(Inaudible).

**Mr. William Serem:** Haya swali lingine linahusu mahakama. Nimegusia, nimegusiwa ya kwamba, kutakuwa na continue ya kardhi. Ilhali, sheria hii ambayo tumesomea hapa imesema ya kwamba, nchi hii ya Kenya, haitakuwa nchi ya ama state religion. Nchi ya hii, lakini tunapojuwa ya kwamba korti ya waislamu, inawekwa, inaonekana ya kwamba, kwa njia ingine, nchi yetu imewekwa kama nchi ya dini, ambayo inakalia sana ni ya dini ya waislamu ilhali tunaye dini aina mbali mbali, hata wakristo, sisi wakristo tunakuwa na shida aina mbali mbali, na huwa na hata sisi tunapenda kwa kortini ambayo wataweza kuwa wanasikiza mambo yetu, kwa wananfunzi vile tunapenda.

Mengine inahusu mtu ambaye anasomea cheti fulani, tumesomea kuhusu that formation of elections, kweli ni vizuri, lakini, haijasema sana kuhusu hali ya mtu binafsi, ambao anasomea nyasifa huo, maana kuna watu wengi ambao wanayo tabia mbaya. Watu ambao hawastahili kuongoza watu, mradi unakuta wakiongoza watu. Hii ni lack of information, kwa nini hawangeele kifungu cha kuchunguza haki ya mwana damu huyu. Hali yake ya binafsi, pengine kama mwanamke kwa mfano wanawake wengine wakichaguliwa, wanaedna wanawacha ma bwana zao, wanafanya mambo ingine kadhaa, kwa nini hamngeweka kiwango fulani ambacho mtu akitaka kuwania nyatifa fulani, aangaliwe kabisa, aonekane ni mtu ambaye atakuwa role model ya kuvaa. Ni hayo tu.

**Com. Salome Waigai:** Asante sana kwa maswali ninataka kuanza kuwatibu kwanza ama bado nasikia kutia mahali mnataka kususha kwa vile mtaendelea kuuliza zingine. Nitajaribu kwa uwezo wangu wote. Ni lazima kua mmoja wetu ni lazima kuwachunga hio katiba, tumezungumzia kuwa lazima wafundushwe kuwa ni kazi ambazo wanaweza kufanya. Kwa hivyo pia sitaja mengi kwa hiyo vile tumesema pia kuwa itakuwa ni ya serikali, kuwa facilitate. Kununua vifaa vinavyo weza kuwasaidia. Ingetaka kusema jambo moja juu ya Katiba. Katiba ni mwelekezo wa sheria, siyo sheria zote. Katiba and the main principles, the broad principles of a country's legal dissemination. It is not everything that has gone to the constitution. Constitution inatupa mwelekeo, kwa hivyo tukisema ati, Katiba ni lazama iwarembeshe walemavu kuleta vipaa vitakavyo wasaidia. Katiba sisi hatuwezi kusema ati ni lazima tuwapatie kodi, kwani tukisema hivyo kwa Katiba, ile yenye tumeacha hatujasema, basi hatuwezi kuenda kwa korti kuwa ni kusaidiwa. Nisema, hiyo ……..(Inaudible) haikuzungumziwa kwenye Katiba, kwa hivyo ni kinyume cha Katiba. Na ikiwa kinyume cha Katiba, haiwezi kutengenezwa na mahakama. Kwa hivyo constitution inajaribu kuleta broad principels za, kwa hivyo tukisema kuwa walemavu waisaidiwa kupata vifaa vinavyo wazesha kushiriki kwenye maisha yao. Basi iwe ni kazi sasa ya Bunge kuunda sheria tekelezi. Zenye sasa tutasema hawatalipishwa kodi, na watakuwa kuwa hivi na hivi, mnaelewa?

Pia, kuna sehemu nyingine pia zaidi ya hapo, Bunge ikshafanya sheria tekelezi, itawabidid tena kwenda another step ya kuwa na national policy on people with disabilities. Tena ni ya watu walemavu, hiyo nayo inatakiwa moja tatu. Kw hivyo tafadhali, tuelewane kuwa, Katiba haiweze kusema kila jambo. Inaalekeza mwelekeo, naye Bunge inaleta sheria na zingine zake, nayo ni sasa inaanza, inakuja na zera za utekelezaji.

Sign language tumeifanya kuwa lugha ya kitaifa. Tumesema tuna lugha, ingawa tulifanya kuwa lugha tatu, tumesema lugha yenu itakuwa na lugha tatu. Itakuwa na lugha ya kiswahili, kiingereza na lugha ya ishara, maanalewa? Ikiwa kuna haja ya kuwa na watu wenye nia hizo, pia maandishi yatakuwa kwenye press, lakini pia hatutaki kusema kama tuna mtu mwenye kuitaji lugha ama la bado itakuwa hapo. Mnatuelewa? Kwa hivyo tafadhali elewa na kadiri ya Katiba, na kikomo chake, tutaweza kufanya nini, haiwezi kufanya jambo hili.

Free education tutasema pia education kwa mtoto wa Kenya, kutokea nursery mpaka form four. Sasa, tungetaka kufanya nini

na watu walemavu? Tusema pia watoto walemavu, tukisema mtoto mkenya tumetaja watoto wote,

**Speaker:** ……………(Inaudible).

**Com. Salome Waigia:** Kwani hujasoma kutoka nakala mwisho kwa mwisho?

Ungeangalia tu pale watoto wa mlemavu. Hakika haki za watoto, tume elekeza pia kuwa, watoto walemavu lazima wapatiwe kile cha ziada chenye wanahitaji waweze kusaidika. Daniel, anauliza juu ya serikali za wilaya, serikali za municipalities, zitapata mtu mwenye kuangalia hiyo, kuangalia kama mambo yote yameangaliwa kama kuna jambo na kuna kingine kinatakikana kuangaliwa cha ziada na kingaliwa. Lakini tuelewe kuwa hii Katiba ni a daft which is working, working centre, kwa hivyo haijamalika sisi wenyewe tujuwe tulitoa saa nane ya usiku, tukaenda nyumbani, tukawaambia yule mwenye anaenda, kuweza kutengeneza atengeneze, kufikia saa tatu, tulikuwa tunataka kuinua kwa public, ilikuwa iko tayari ilikuwa ya saa nane.

So, it is something that still be defined. Tutaangalia hayo mambo nikitekeleza. Ukikuwa na mambo hoping proposals, tafadhali tuandikieni, tupatieni Paul na tuta zipata kwenye office yetu. Na hiyo pia ni habari ya municipalities na mayor na hiyo inatakiwa kuangaliwa…………..(Inaudible)

Political missionary, ten years, tumesema kwa muda mrefu, lakini kila wateja walipatia Kenya, mtu Kenya, tuliwapatia mlango wa kuingilia, na tutamfungulia, kufungua tu tukisema ndio huwo mlango wafanya nini? Wa kutunga Utaingia, na unakaa kwa wakati wenu wenye tunakushughulikia vile tunavyotaka kufanya nini? Kuhudumiwa. Usipotuhudumia pia kuna mbinu za kusema, Kubali vile tulikuambia, tafadhali mpe mtu mwingine nafasi ajaribu kufanya hiyo. Kufanya nini? Kuhudumia wananchi. Kwa hivyo sisi hushinda miaka kumi, akienda miaka ishrini, hapati vile watu wanataka, hata onelea upande mwingine. Tumepatiana vile takavyo chaguliwa, na vile atakavyo achishwa kazi, pia iko, mpango huo uko kwenye kuna Katiba.

Ministers wakiwa wataalam na Bunge, kati ya wataalma huwa watakuwa duni, hata iko upande, sasa huyo minister atakuwa na nafasi zake zakuchaguliwa. Atakuwa kwanza kwa kuwa yeye ni mtaalam. Na ikiwa tunataka minister mmoja wa masomo, na vile tuna waalimu wengi, competition itakuwa very high. Na nani mwenye atachaguliwa kuwa nini? Minister. Hayo majina yote

yataletwa waziri mkuu, lazima ipelekwe Bunge, yaah, lazima Bunge ikubaliane kuwa, Salome Wairimu Muigai, ndiye mwalimu shujaa zaidi na ndie mwenye anatakiwa kupatiwa nini? Ministry, wanaweza kataa waseme kwa nini umemleta Salome, walikuwa wanasoma na Paul, na Paul alikuwa mtu wa juu.

**Speaker:** ……………(Inaudible).

**Com. Salome Muigai:** Mwalimu mzuri, angekuwa mwalimu mkuu, amekuwa, alikuwa katiba katika wilaya ya, na wizara ya elimu na mambo mengi. Kwa siyo tumngoje mwenye kumchaguwa mtu, akiwa wakienda huko, utaenda tu kum-select, kumpenda mwenye kuchaguwa. Tumefanya mbinu, tumefanya utaratibu wa kuchaguwa watu ili mtu asisikie anamtumikia mtu mmoja. Na asipofanya kazi yake, pia tumeweka mlango wa kutoka.

Judiciary, codes zake, siyo lazima tuwe tumekaa Nairobi, la, kuna zingine zenye zitakuwa sehemu zingine, na zingine zitakuwa kutembe kutoka mwezi mmoja hadi mwingine kufanya kazi huko, lakini siyo korti yetu ndio zitakuwa Nairobi.

Uraia na wananwake, kuwa mwanamke asikubaliwe kulipisha bwana wake, uraia, lakini mwana mwanaume akubaliwe. Kwa nini tutasema, sawa sawa mbele ya sheria, kati ya mwanaume na mwanamke, lakini tukija kwa mbinu zenye zitaonekana kuwa kutekeleza huwa usawa, unakuwa na shida.

Mtu wa dini kama mwana Kenya na mwalimu, atakuwa kulipa kodi ile ile kwenye ndugu yangu analipa kwani ikiwa na mwalimu, ama tukiwa wana shule mimi nina ndugu yangu, tutatatishwa, tutatoa kodi ile ile ya mapato kwa ajili ya wasichana wangu kama Bwana Tonny, kwani kitu hiko kwa haki zangu za kifundisha bwana wangu uraia, tunaona shida? Lazima niwe na haki zangu na nikuwe na jukumu langu. Wakati wa jukumu la waalimu, mnalipa waalimu wa kutosha kama ule, lakini wakati wa faida, ninatengwa. Kama inaitwaje, ile kwenye, kama mambo angekuwa hapa angeulizaje? Hata nyumbani mwetu angalieni, leo kama babangu akitka kununua shamba, mtu wa kwanza kupigia simu atakuwa nani? Atakuwa msichana wake mwenye uko kwa dume kwani ndiye mwenye nini? Ndiye mwenye pesa sivyo? Halafu wakati wa kupeana hii mshanga, kuakuwa baado mimi kwani mimi ni mwanamke. Wakati wa kutoa, mimi ni mtoto wa nani? Wa baba, wakati wa kubaitika mimi nimeonewa, je,

jiulizeni nyinyi wenyewe, je nini,

**Speaker:** …………..(Inaudible)

**Com. Salome Waigai:** He , mambo walifanya huu ulifanya ni kuuliza. Unajuwa uzuri wa Katiba, Katiba ni sheria, na Katiba ni kitu cha haki, na haki ikipitia karibu na mimi, nitapita vile, nitapita karibu na jumba, wakati mwingine ni wadhukuma wastahili kutoka kwa hiyio haki, wakati mwingine ni mimi nastahili kwa hiyo haki. Na akina mama wame jitetea kwa muda mrefu, kuwa wanabaguliwa, siyo kwamba wafenye kazi, siyo kwamba hawafanyi bidii, siyo kwamba wanafanya baadaye, lakini kwa kuwa tu hawo ni nini? Ni wanawake. Lazima mtu mmoja mwenye alisema wakati huo, wa zamani sana kuhusu kina mama na kina baba. Yeye mwenyewe, alikuwa Bwana technologia mkubwa sana, na akafanya technologia kwenye ya watu, ni ya ajabu, akamuumba mwanaume, na yeye mwenyewe siku moja akaendelea, akaendelea akaja wakati mwingine akangalia huyo mwana ume na akasema hiyo basi mwanaume kuwa ni kuwa peke. Lakini hakuweka watu wakusema akuwe pekee kwa Bunge alikini akisema tu one thing, one sentence. It is not right for man to a leader. Je, tunatakaana na huyu mwenye wa kitechnologia, unamjua?

**Audience:** Yes,

**Com. Salome Muigai:** Alikuwa ni nani?

**Audience:** ……………..(Inaudible).

**Com. Salome Waigai:** Haya, kama mungu mwenyewe, alikubali kuwa kulikuwa na makosa hapa na aka-correct, kwa nini sisi tuna nia na makosa ya kuishikilia? Mungu aliposema hivyo hakuwa na mwanamke pekee yake, alifanya nini? Aliumba mwanamke, alileta mwanamke, kwa Mungu ndiye mwenye alikuwa wa kwanza kutenganisha wanaume na nini? Na wanawake, lakini alipoangalia kwa ratili, akaona kweli pengine alikuwa, alikuwa nini

**Audience:** ……………………(inaudible)

**Com. Salome Muigai:** Sawa na yeye akafanya nini?

**Audience:** ……………………….(Inaudible)

**Com. Salome Muigai:** Akapewa wasichana na akarekebisha, sijui kwani sisi tuliyo umbwa kwa maumbile ya wazi wa kitechnologia, wa mkuu, kwa nini kuna shida kubwa hivyo? Najuwa utamaduni wetu unashida nyingi na kuna swali nyenye mama mwingine aliuliza pale kwenye, nitaangalia pale, lakini Katiba, ni Katiba ya kidemocrasia, ni Katiba ya haki, ndio vile tumesema, na maana zetu ni nini? Ni haki, democrasia na uhuru wa kweli. Tulisema uhuru kwa wanaume si peke yao, ni kwa uhuru kwa akina nani? Kwa hivyo tafadhali ndio mnajuwa wabunge, mkubali Katiba yote ama mpigie nje, yote, kwani itawapa kila mtu uhuru wake na nafasi yake. Mzee na yule hafanyi unapo muona, lakini wacha nimalizie hayo maneno kwanza.

**Speaker:** ……………………(Inaudible)

**Com. Salome Waigai:** Hiyo mzee, hata tukizungumza huenda tukakosa kuelewana wakati huu lakini, mimi na wewe tungeketi tuzungumzie kwa ziada. Vikao vya watu chache vya Bunge. Tumesema kuwa Tume ya uchaguzi, kila miaka kumi tukishafanya censors, wanaangalia vikao vya Bunge wakilinganisha na matokeo ya censors. Kwa hivyo hiyo ni kazi yenye Tume haingeweza kufanya kwa kura, kwa kura, hukumbuki tumeimba hiyo kazi kwa Tume ya uchaguzi. Kwa hivyo constituencies zitakuwa reviewed, zitaangaliwa tena kila baada ya miaka kumi. Tumeelezwa kazi ya 2500 voters wenye wanakikoa na watu wenyewe, 100,000 voters. Hawa wakichaguwa elfu mbili, wakileta wabunge wao, na hawo wapigaji kura, elfu mia moja, wakipiga kura wote, na wafikie chama chao ama kiwe kimoja, watakipenda sana. Hata vikiwa nyingi, watalipa nafasi vyama vyao, kupata viti katika ile ziada.

Pia ni shada, watapata viti vya ziada, wakili wingi, wao, lakini bali yule mwenye pia ana 2500, pia yeye angetaka mjumbe wake. Kwa hivyo yule atataka wake, na hawo kwa ajili ya wingi wao, watapata pengine viti vingine viwili, ama vitatu vya ziada.

Mumeelewa hapo? Tumejaribu kutumikia kila mmoja, badala ya kusema huyu ni mdogo sana hajalalwe, tunamsema wewe wacha asikie tu ndoto yenye iko ndani, tuacha tuangalie vile tutawasaidia wenye viwete zaidi ili wapate zaidi, lakini siyo kunyang 'aya yule aliye nayo kidogo tule,

Nicholas, amezungumzia upande wa devolution, amezungumzia habai ya municipality na districts, tusikia hiyo part tutangalia zaidi, pasiwe conflict, halafu kulikuwa na swali pia kuuzu implemantion to constitution, na hapo ndio mahali nitasema kuwa, hapo nitasema kuwa, Katiba imeweza kukubaliana na mwenyewe tendo, haina difference, the constitution does not have difference on how to implement. The implementation as we know are the act of Parliament under in the pollings state, kwa hivyo mambo mengi hayawezi kueleweka kama yakawezeshwa kwenye Katiba, lakini watu wengi wamenipendekeza kuwa constituency isiwe nyingi zaidi kwa upande zingine kumi na tano, na kwa hivyo tujadiliana vibaki tu sabini na tano. Hiyo ni proposals, hiyo ni pendekezo, tafadhali ibakie kwenye delegates wenye watakuja kwenye mkutano kitenge anazunguonizia kuhuzu equality ya akina mama, atakubalishwa kupeana uraia, kwa Bwana Sau, kuna mtu mwenye ana shida ya mwanaume kukubalishwa kupatia uraia kwa bibi yake mgeni? Kuna mtu mwenye ana shida na hiyo? Basi tu, wanaume mna shida na hiyo? La, okay, ndio huyu, mtu mwingine alituuliza tunasikia habari ya Africa wana wake, Africa walemavu, Africa kila mtu mwingine, kwa nini Africa hawatoki, kwani saa zote iko, wanaume hawapiki haki zao, ndiyo? hawapiki haki zao, kwa nini kila mtu ameniambia, madam tungetaka tukioa bibi wa kutoka nje wakao hawo wenyewe na …..(Inaudible). Nyinyi mumeharibu haki zenu, ndio hamna haki za kupeleka haki za wanaume, kwani mkileta haki za wanaume, tuseme watu wakishikwa wakakue na still busy, kwa nini wamenyamaza, kwani ni haki zao. Shida tu, ni mtu ampe mwingine haki zake.

Kwa hivyo hakuna haja ya kuzungumzia haki ya wanaume, sisi sote ni wanakenya, wananume wanatuchukulia wenyewe kwamba mamlaka yao na kwa wengi wao, na sauti zao kubwa zenye kunguruma na zinasikika.

Siyoni shida kubwa juu ya municipality na wilaya, ingawa bado niko, nafikiri nitakuwa na mtu mwenye pendekezo, anaweza kunipa, kwanza kuwa wakati huu, tuna wilaya, tuna county council, na tuna municipality. Hivyo, hizo zote ziko karibu wilaya moja, karibu mahali pamoja, na hamna msongomano, mamlaka, kati ya District. Kwa hivyo tunaweza kuwa na serikali mbali mbali ama kutawala mbali mbali, na tuweze kukaa pamoja. Ni vile tu we should make sure that we defiled hii document tuweze

kueneza kila mtu jukumu lake la inaende wapi, inaenda lingine linakuishia watu.

Robert anasema kuwa, hamna shida hasa nyinyi, hata hii Bunge tulikuwa tunafikisha hii, katika Katiba, sisi tungetaka kusema hivi, mamalka ya Tume inamalizika tarehe tatu January, kwa hivyo hii isipokuwa iko kubaliwa wakati huu, tutatengeneza Katiba ingine iwe itakuwa na …**$$$$$$$$$$$$$$$$ End of side A**

Nafikiri tulikuwa na shida ya kuwa na wenye kupatiwa haki za kuwa wa raia watakuja kuchukuwa mashamba yetu, pia wanaume, wakati utasema hataki, mimi bwanangu akija hana sharti kuenda kuchukua shamba la baba Kamkunji, atakuja kuchukua shamba langu hata mimi ni mununuaji wa shamba. Sijui mnafikiria, mnafikiriria akina mama vipi? Ni dada zenu, wakati mlikuwa mkinunua mashamba, na sisi tupia tunafanya nini? Tuna nunua mashamba. Na tukirudisha mashamba, kila mtu apate nafasi yake, ya kuleta wake bwana. Kwa nini unataka kuleta mdada mwenzako, na mimi mwizi nitakaa nini wakati wa kuleta Mrwanda. Kwani mnasema shamba yetu. Shamba tulisema shamba lake Kenya ni nini? ni za Mkenya, kwa nini unafikiria lakini basi ni wanaume, Mkenya ni nani? Ni mwanaume na nani? Na mwanamke, na ndiyo kwa preamble yetu tumesema, wacha tuangalie, kwa preamble tumesema, nilisema, recognizing, can you make this clearly. Recognizing the aspiration of our work, na tuanza na akina nani? Recognizing the aspiration for our women and men for a better state of on the essential values of freedom. Tumeelewana? Freedom ni ya nani? Ni ya nani na nani? Ni ya mwanamke na mwanaume. Demokrasi ni ya nani?

**Audience:** ………………(Inaudible).

**Com. Salome Waigai:** Tuende kusema wote, kwani wakati mwingine tukisema wote, watu wengine nafikiri wote ni wao peke yao. Ikiwa kuzuru nafikiri wote ni wakikuyu, ukiwa mkalenjin unafikiri wote ni nani? Tukulu

**Audience:** ………………..(Inaudible)

**Com. Salome Waigai:** Ni nani, sasa tunataka kumueleza kiga naga au wote ni nani? Kwa hivyo tukisema hatari ya freedom

of, inabakia nani? The women and men, democracy of women and men, social justice. Social justice ni ya nani na nani?

**Audience:** ……………(Inaudible)

**Com. Salome Waigai:** Ni ya nani na nani? Women and men, and mwisho huo, tafadhali tujuwe, mwisho huo unasema nini? Rule of law, kwa hivyo tukisema ni rule ya nyumbani ama ni rule ya kanisani ma ni rule ya kitaifa, ni rule of law. Na so nitasema kuna nini? Kuna uhuru, kuna demokrasia na rule, na kuna social… sasa kama tumekubaliana hayo, nini pahali pengine tunarudia tena?

**Speaker:** (Inaudible)

**Com. Salome Muigai:** Kwanza unajua mzee ninajua wewe ni baba yangu kwa hivyo ukikuwa unakiuka ahadi zangu ukiwa wewe ni baba ya wasichana na wavulana, tutaangalia hiyo. Mzee ulikuwa na nafasi yako na sasa ni nafasi yangu ya kujibu maswali tafadhali. Kwanza tukianza debate mimi na wewe na tuanze na mwingine, kweli tutamaliza? Na yule mtu mwenye alikuwa hajapata nafasi ya kuuliza swali lake hatapata.

Robert, ni yule aliyesema haki za wanaume zilikuwa hazijatajwa na habari ya uchawi; Sasa hiyo itakuwa kwenya Act of Parliament ndiyo itakataza vitu zingine kufanyika, zenye zinawadhuru watu fulani lakini hiyo haiwezi kuja kwa Katiba kwani tukisema mtu asifanye uchawi, hayo tunaweza kuingisha kwa Katiba? La. Katiba inapeana mwelekeo halafu the Act of Parliament inaleta habari za matekelezi.

Zakayo, anazungumzia habari ya kura; tumesema kila mtu ana haki ya kukaa pahali popote. Hiyo tumekubaliana? Si hiyo iko kwenye katiba? Tumesema kila mtu ana haki za maoni yake. Tukipeana hizo haki zote, mtu atakuja akuambie hapa huwezi kusimama na chama hiki. We cannot condone such a thing in the Constitution, tunasema una haki ya kutoa maoni yako kama binadamu na yanalindwa Kikatiba kwa hivyo ukiwa popote pale ulipo unaweza kutoa maoni yako na unaweza kuwa na chama chako chenye ungetaka kuingia bila kutatizwa na mtu yeyote.

Uliuliza swali kama hii viti 90 wenye walichaguliwa wanaenda wapi; wenye walichaguliwa wanaenda kwa National Asembly.

Kulikua na swali kuhusu hizo viti thelathini; za wakina mama wenye wamechaguliwa kwenye hizo viti wanaenda kwenye baraza la taifa, yaani National Council na National Assembly.

Mwanafunzi alikuwa na shida na kama tuna wimbo wa taifa; tayari wimbo wa taifa uko kwenye ishara za jamhuri Kikatiba.

Kadhi's Court ina historia yake; Wakati Kenya ilipata uhuru, katika mwambao wa pwani kulikuwa na maikulu kutokea kwa bahari yenye ilikuwa ya Sultan. Sasa wakati Sultan walipokubaliana na serkali ya siku hiyo kuwa Kenya itakuwa nchi moja, kitu moja waliokubaliana ni kuwa Waislamu watakubalishwa koti yao ya kuangalia maslahi yao ya kibinafsi kama kuoa, kifo, kuzaliwa, talaka, kuridhi na vitu kama hizo bali ilikubalika na bado tunaipa heshima kwani ni contract yenye tulisign na hatutaki kukiuka makubaliano yaliyokuwa hapo mwanzoni.

Mbali na hivyo, bado hata sisi tunakubali koti zingine. Kama wakati wa kuoa, tumesema lazima Bunge itengeneze sheria itakayokubalisha watu kupewa certificate ya kuoa na kuona ingawa hawajaona kwenye kanisa, wenye wameoana kitamaduni, watu wanakuwa ukisha toa dowry kabla kuwa huyu ni mke wako ama huyu ni bwana wako na tunataka hiyo iangaliwe vile inaweaza kublika. Kwa hivyo hiyo kitu zenye zinaalekea maanani, inaelekea maanani ya kazi zingine. Kuenda kuolewa kwa kanisa ama kuoa kwa kanisa, pia sisi hatukubuli madaraka ya kanisa yako, sivyo? Mboni sivyo inge huhitaji lalzima uende kwa DC, ndio upate certificate ya ndoa. Kwa hivyo kuna mamlaka mingi zenye zinakubaliana. Ukiangalia kwenye tulisema sheria za Kenya zitatoka wapi? Pia tumeweka sheria za dini na sheria za utamaduni, siyo za kiislamic nafikiri. Angependa pia kuona kwa nini tumeekea saa ya President mihula miwili ya kazi kufanya kazi yake lakini si wabunge, kwa nini, kwa nini tumempatia, kila mahali kwenye tukienda wananchi walituambia tumueleke, Rais kufnaya kwa na kufanya kazi kwa mihula miwili ya miaka tano kila mmoja, lakini watu wakitofautiana juu ya wakati wa bunge. Mambo mengi inaweza kuwa ya Bunge ilikuwa, tupatie wananchi nafasi ya kunrudishe mmbunge wao ama hafanyi kile wanataka, kwa hivyo hatukuwa na haja ya kumpatia muhula kwa sababu anaweza kurudishwa na wananchi wengine.

Unataka Katiba irembeshwe, ningetaka maoni yako yenye ingefanya nini ili tusikie kuwa, Katiba yako ina urefu wa kutosha ……….(Inaudible).

Na organization of content, mpangilio wa constitution pia ningefurahia kama ungetupa mpangalio, pendekezo la mpangilio wenye ingekurudisha zaidi. Je, anauliza kuwa ma-passports lazima zitaanziwa mbali. Passport ya kuambia watu wewe ni mwenyeji wa mahali gani? Kwa hivyo ukienda America bila passport, hawajui kuwa mkenya anaingia wapi, amerika, vile tungetaka kufanya, ni kurahisisha utaratibu wa kupata passport. Visaa, hatuna visa, hatutakiwi na nchi yako haitakiwi visa. Unapatia visa na nchi nyingine, kwa hivyo ndio maamlaka ya Katiba yetu, unaelewa? Hatiwezi kulazimisha America lazima akupe visa au asikupe. Tumeona uhuru wa kuja kwetu na kuwa mwenye kwetu na nafikiri kuna, pia kuna hii chini katika yao.

Hii hatari ya …………..(Inaudible), hizo vitu za ziada, hazilikuambia, tutaweka wapi akina mama. …………….(Inaudible).

Counting at the polling stations, hiyo imekubalika, hatutachukua, kura ziende zikahesabiwe mahali pengine, zitahesabiwa pale pale, mahali zimeandikiwa.

Freedom from discrimination from HIV Aids, hiyo pia ni, tunasema aje, ninasema kuwa the sick shall go and deal direct or directly against anyone or one or more crowd, including rape, sex, pregnancy, domestic violation, ethnic of social origin, colour, and disability, religion, conscious, belief, culture, language of birth, this is not a problem. Mtu akienda kwa korti, tuseme amebaguliwa kwa ajali a Aids, inaweza kusema ni kwani wanamuona kama, amelemewa kwa ajili ya kuwa na huu ugonjwa. Kwa hivyo anaweza kukuletea hiyo hadi, that should not be an issue of discrimination.

Culture na SDA, tumesema tunakubali culture yetu, mradi tu isikuwa kinyume cha Katiba. Na Katiba imesema, mila zenye, umeangalia haki za wanawake, umeona tumesema nini juu ya kila sehemu. Ziwe huru haki za wanawake, ukiuza, tumesema kuna problem vile tunavyo kiuka haki za wanawake ama kuwaangalia wananwake kama ndio wanaKenya kamali. Hazikubatiani, haziendi pamoja na Katiba hii pia.

William Serem, President, anauliza habari ya President akiwa na as nominated by party tumekubali President anaweza kuwa amekuwa nominated by a party, ama yule Presidential candidate, anaweza kuwa Rais, vile tumesema ni kuwa akishachaguliwa Rais, basi hawezi kushukukisha na chama. Kwani na haki chama chake ni gani? Ni chama cha Kenya.

Kile kitu kingine tulivyo tengeneza ni kuwa, Rais hawezi kuwa mwana Bunge wa kituo fulani ama kikao gani, kwani Rais kikao chake cha Bunge ni kipi? Nchi nzima ya kitaifa, kwa hivyo tunajaribu kumwondoa Rais wetu kwani kwa ile kazi ndogo ndogo ndio aweze kutupatia kazi ya kitaifa.

Tumeambiwa kuwa wale watu ndio watachaguliwa kwa hii vitu ya siada, watakuwa wakingalia maslahi tofauti, mbali MP atangalia maslahi yote na tutakuuliza muzungumzaje kuhusu hizi and anaangalia maslai ya chama chake. Ni Mbunge anaangalia maslahi ya chama chake kwanza. Wakati mwingine anapiga kura ya chama, kwa hivyo hata hawa wengine wenye wataenda wataangalia maslahi ya watu wao, lakini bado watakuwa na uhuru ya kuangalia maslahi ya Kenya nzima. For example tukizungumzia habari ya mazingara, mazingara ni ya nani? Ni ya kila mtu, tukiangalia habari ya barabara. Barabara zina nani? Ni za kila mtu. Tukiangalia habari ya maji, tukiangalia habari ya masomo, lakini tukiwa na nguvu mwenye aliendа kwa matanga, ya mlemavu tukizungumzia masomo, atakumbuka kusema lakini, tukijenga shule, tuhakikishe kuwa watoto walemavu wanaweza kuingia na kusomea kwenye shule, kwa hiyo jambo la ziada, lakini tunahitaji kubaki kwa ziada, ikiwa si mahali tutafanya nini? Kitakuja, tukizungumzia habari kama ile examples nilipeana zamani, nikizungumzia habari ya maziwa, for example, watu wote watafurahia maziwa kila mtu atumie maziwa, lakini mtu anaweza kumuliza itakuwa ni jambo la miaka, kwani maziwa siyo kinywaji tu mbali kujalisaji wa umbali wa watu. Ni hiyo isirudishwe, kwa hivyo lazima tuwe na watu wenye kusaidia kila kitu, lakini pia watu wenye kuchangia maslahi tofauti kwenye Bunge. Na mtu akiingia Bunge letu, anaweza kuwa aliona vile sura ya Kenya nzima, Bunge letu ni hivyo, sasa sio sura ya Kenya nzima. Ukiingia Bunge, utaona watu wengi sana wenye wako Bungeni, kwa hivyo mtu akiingia Bunge, naoni sura ya Katiba ya Kenya tungetaka kujuwa vyenye tutaandika kwa hii Katiba, iwe sura ya Kenya.

Commission, itaangalia, itachungua kila kitu mngetaka kusimamia huo uongozi, it does matter you are a man or a woman.

Imeletwa kwanza ni lazima ichunguzwe watu kwani, masili wetu wakiaribiwa wanaweza wanaenda na mabwana wao. Kusema ukweli wanachaguliwa wanawacha mabibi. Hakuna, hakuna,

**Audience:** Noise

**Com. Salome Muigai:** Hata hawaonyeshi bibi moja nyumbani ya kuonyesha wengine ya Nairobi…………..(tape not clear) na haki zao. Unajuwa mzuri wakati ni kama mathematics, mathematics, ukisema 2+5, na mimi ndiye mwenye nakuuliza itakuwa, 2+5 itakuwa ngapi, saba, kesho ukiwa wewe ndiye mwenye unalilipa, 2+5 itabaki baado ni saba. Sasa uhaki ndio huo, ukinifaidi leo, ujuwe kesho utamfaidi mwingine, sasa nimesha muulizia maswali yote yenye niliulizwa na team ya kwanza ya watu kumi, kuna watu wengine wenye maslahi zaidi? Ama mumetosheka, kuna maswali, basi .

**Speaker:** ……………..(Inaudible)

**Com. Salome Waigai:** This is the last round, kwa hivyo ukiwa una swali tafadhali ulete hapa. One, two, three, four, five, six, seven, kuna wengine, hiyo ndio mwisho wa maswali, nyinyi ndiyo the last round. Kuna wengine, basi, anzeni nashukuru. Mzee, una swali? Anzeni na huyu mzee tafadhali. Mzee simama tu pale utaletewa vyuma vya sauti, miaka yako inakubalisha na aulize na lugha yenye anataka.

**Joseph Malakwen:** *Katinye kityo kit akenge mami lokowek, chamgei tugul*

**Com. Salome Waigai:** Ningetaka mtu wa kum-interpret vile anasema.

**Joseph Malakwen:** *Kamache anyun chito kotafsiren. Siron Kiswahili makase komie.*

**Translator:** Ningetaka mtu wakunisaidia kinitafsiria.

**Joseph Malakwen:** *Kikurenon Joseph Malakwen ne ba Cheibei*

**Translator:** Kwa majina ni Joseph Malakwen wa Cheibei.

**Com. Salome Waigai:** ………………(Inaudible) tuweze kusikiza maswali ya wale wengine.

**Joseph Malakwen:** *Ki atkinye kimi yu, kane ba oeng' niton ko kikateb kele kanyan receipt ko kikamwa kit en Katiba ini.*

**Translator:** Wakati huo mwingine tulikwa hapa, ambayo sasa ni mara ya pili tukiwa hapa, nilikuwa nimeuliza hivi kuhusu hii Katiba.

**Joseph Malakwen:** *Ko kikamwa ale oye a nyalili kongeten minginatenyun manyoru mbar.*

**Translator:** Na mzee kama yeye amekuwa na shida sana na hana shamba tangu utoto wake hadi sasa.

**Joseph Malakwen:** *Kamwau alenjin ngot ko kalel en ngalek chuton onyoiwan gat.*

**Translator:** Sasa ninaombe msamaha kama hiyo maneno mumeongea juu yake, mnisamehe.

**Joseph Malakwen:** *Ara anyun noton ne katebe mami ng'alal che chang'.*

**Translator:** Angependa kujuwa kama hiyo shuguli itafukuzwa kwa vile hana chama, kama mumeongea, then ……….(Inaudible).

**Joseph Malakwen:** *Machang' che katinye kochoton.*

**Translator:** Hana mengi, ni hiyo tu.

**Com. Salome Waigai:** Asante kwa maswali yako mzee malakwen. Asante sana kwa swali lako la watu kutokuwa na mashamba, ilikuwa jambo la na ulinieleza kila mahali katika hiyo, na

**Translator:** *Amache alechin bik ko kiking'allalen kele matinye imbarenik bik ko kiki ng'alalen keketyigei ago takeng' alalen kora.*

**Com. Salome Muigai:** Watu wenye walikuwa hawana mashamba walitulitea malalamishi yao.

**Translator:** *Bik che chang' kokiibwech malalamishi che uchoton ii,*

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo tukasema kuwa kwa akili Tume ina muda mfupi sana wakufanya mambo yenye inatakiwa kufanya,

**Translator:** *Kele amun kitinye betusiek che ng'eringen kechoben ng'alechu,*

**Com. Salome Muigai:** Hii Tume itafanya Tume ingine yenye kuchunguza hali ya mashamba.

**Translator:** *Bik che nyalu ko chop tume, kochengeng' bik alak che mache sikonyokoyai uchunguzi konai kole ngo' ne matinye imbarenik.*

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo hii Tume ya mashamba ndio itaona shamba ziko wapi, ina zinatukabithi, na zitaanza kugawanyiwa ili watu wasaidike kwa jumla.

**Translator:** *Tume inoton koamuani kole bik che matinye imbarenik kokere kole kimuche kesib oret ketaret bik che matinye imbarenik.*

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo wakati huo Tume ingine itakuja tafadhali julisheni mzee atoe ………(Inaudible) zake.

**Translator:** *Ko ingunon kobwane pichotet che ba Tume ne ba imbarenik komuch kemwaun si nyon si mwachi kole taretech kongoi boiyot.*

**Joseph Malakwen:** *Kongoi missing is.*

**Ms Beatrice Cherono:** Because I have the microphone, ningependa kusema kwamba nimefikia pia hii Katiba na nimefurahi

kama mama, kwanza,

**Com. Salome Waigai:** Sema majina yako

**Ms Beatrice Cherono:** Mimi naitwa Beatrice Cherono, Eldoret town. Na vile niliangalia hii Katiba, kwa kweli sisi akina mama tumewakilishwa vizuri na watoto kulingana na vile tulikuwa tumeongea wakati huo mwingine, tumefurahi kabisa, upande wa vita, upande wa iriithi, hata wakati utakuwa na 30%, lakini swali langu ni hivi, kweli ni vizuri na kila kitu kimewakilishwa, ningewauliza Commissioner, kuna wakati ama between now, and the period when you are going the, the period constitution inaendelee. Nina wasi wasi, wakati wowote tuliona kwamba hiki kikionekana kimechapa sana akina mama, tungependa kuwakikishia kwamba, hakuna mahali ambapo hali katika ya akina mama yataweze kuwekwa kando, mama wale ambao wanataka ku-humuliate kama women. We might not be able pass our proposals at the national conference. So, wasi wasi yetu ni kwamba, kama kutatokea kamati hiyo, sisi akina mama tunaweza kufanya Koran ingine akisema kwamba tunaweza kutetea zile haki zetu ziweze kuwekwa katika Katiba.

**Mr. Rotich:** Madam Commmissioner, ni jina langu Rotich, na niko na maswali kama nne. Ya kwanza ni kuhusu ardhi, land, tukiangalia kwa Katiba, kuna kitu ambacho kinaitwa national land commission. Kwa hiyo land nayo national land commission, itakuwa ikiangalia, unasema kuna shamba mahali, ambayo bado kutumika, itakuwa maamlaka ya hiyo land, maanake. Swali ni hili, ili kuona ya kwamba, hiyo national land inaweza kuwa vile lile system ambao iko sasa na inaweza kutoka hapa, inaenda kwa commission fulani, kwa vila kuna commission fulani huko Eldoret, Kitale ama kuna commission unikatie, na kwenye Kitale, so, kama hiyo chama kiko under national land commission, wengi itakuwa huko mpaka wao watu wa hiyo community ndio watapatiana land.

Ya pili ni mambo ya uraia, uraia ambao ni upendaji wa, kama niko na mama ng'ombe yangu msichana, unaleta Bwana kutoka Uganda ama wapi? na kwa miaka mitatu tutapatia yeye citizen, ama kuona ya kwamba, kupeana uraia kwa huio muda mfupi sana, inaweza kuleta kuwa kama mambo majabu kwa sababu kama niko na pesa chungu nzima, na mimi nataka kuwa citizen wa nchi hii, nitanunua huyu msichana akubali tuone, tuwe na duo citizen.

Ya tatu, ni mambo  ya public rally. Wakati huu, wakati ma-degree inapeyanwa, ndio President wa nchi ndiye anaenda kwa nchi kwa hiyo university. Labda ingekuwa vizuri kama tunge-delink public universities na President afanye mambo ya ngine ya nchi na kila university wana present-wa na chairman ama President yake anapeana degree, ndiyo hiyo department wanaweza kufanya kwa muda msawa, bila kuwa appointed.

Na nne ni mambo ya kilimo ya Agricultural sector. Kwa Katiba sijaona hasa kwa maonyesho vizuri zile kazi za Agriculture sector itakuwa tena kwa sababu tunatoka kwa District ambayo tunakuta maiti, uko na ng'ombe, hii inaenda kwa importation namna gani? Kwa sababu ya importation, ambayo inakuja kwa nchi hii, na sisi kama wakulima tuweze kuomba maziwa, hatuwezi fuga maziwa, hatuwezi kuza ng'ano, hatuwezi kuza mahindi.

Ya tano, ni wale watu walemavu, hata wale ambao wanatembea na wheelchair, kama wamejiriwa wafanya kazi, na pengine ile building ambayo wanafanyia kazi ya gorofa, mtu ambaye atatembea na wheel chair itaenda katika gora ya Ishirini mbili au namna gani? Mimi nafikiri, ingekuwa vizuri iwekwe kwa Katiba, any dazzling building iwe na ya walemavu. Asanteni.

**Raphael:** Kwa majina naitwa Raphael maswali yangu is about maneno ya korti, iko maneno ya korti unapata ya kwamba, unasema unastamili kuenda kwa mtu fulani  lakini mimi nimeonelea ya kwamba, tufanye nini? Hiyo kesi siyoi mbaya, ama hii kesi itapitishwa, utapata ya kwamba mbunge inakaa kwa ………..(Inaudible). Now, kuna wale members of the society, mimi nimeonelea ya kwamba, hii NSSF, inagalia watu ambao wako hapo, ambao wamekufa pekee yao, lakini wakingalia watu hii watu wengine unaona ya kwamba hii watu wengine wale ambao walikuwa.

**Mr. Edwin Baraza:** Jina langu ni Edwin Baraza Mutemi, nina wakilisha 3C CKRC Commission Elgon District ni langu la kwanza ni kama walikuwa wameuliza, lakini ningependa kulisitiza mambo kadhaa.  Ya kwanza ni kuwa ni kweli tunaweza kufanya uraia wa Kenya ukawa kama biashara na ukaleta watu labda kuwa hawastahili kuwa hapa kwa sababu gani? Miaka mitatu ni muda mfupi sana, wakuweza kujua kama mtu kweli anafaa uraia, ama hafai. Pendekezo langu ni kuwa labda tuongeze huu muda uwe wa miezi mitano, sita au saba.

Jambo lingine ni kuwe ni sheria, lazima iwe imetengenezwa kwa pande zote, kwa upande wa wanawake, na kwa pande za wanaume.

Halafu jambo la pili, ni kuhus ku-devolve government, the new government structure. Naona kuwa Katiba mpya kweli imejaribu kuleta serikali chini mpaka kwa wananchi paka kwa wananchi wote. Lakini swali langu ni kuwa sijui kama Commission nikiona inaweza ama haiwezekani, maanake kweli ni wazo nzuri lakini kama ukweli tukiwa na uwezao, wa kifedha wa kuweza kutengeneza haya mambo pia hizo ni swala lingine na nina wasi wasi hasa kwa upande wa mabaraza ya vijiji na baraza za Location pia, naona ni kama itakaramu peza nyingi sana itekelezwe Ni kama haiwezikani katika viwango hivi maanake wanahusika watakuwa ni wengi.

Halafu jambo lingine lilikuwa hawo watu walikuwa wataka kulipwa, kama waliweza kujiitolea bado inawezakana, lakini kama wataweza kulipwa, bado nafikiri nahitaji pesa nyingi sana kuweza kutengenezewa haya mambo. Yangu ni hayo mawili tu.

**Ms Helen Cheptoo:** Madam Commissioner, niko na maswali matatu, na nitazanza na swali la kwanza kuhusu hizi kesi za akina mama na, thalathini na National Council. Kwa majina Helen Chekemoi Cheptoo. Hasa ninaona ya kwamba wamependekeza binafsi napendekeza ya kwamba, tuwe na viketi vy kazini vya akina mama. Na pia wamefawanya hivi viketi hivi; kutakuwa na wa mama wanne kutoka kila province, halafu wawili watatoka Nairobi, ningependa kuelewa kwamba, kwa nini wamechaguwa wa mama wawili watoke Nairobi na pia tukielewa na kama Nairobi pia ni province.

Na naende kwa upande wa numbers, hasa wale watakuwa wachache labda wameona watuengezee kwa province, sasa wale watagawanya namna gani? Kwa sababu kama province kama Nairobi itakuwa na watumishi wale wa mama halafu pia wawe wengine wawili, sijui, hapo sikupata kueliewa vizuri.

Halafu ya pili ni kuhusu ministers ambao watakuwa professional kwa ministry wenye watasimamia Sijui kama kwa sababu zile

zitakuwa na programme ya professional, bado tutahitaji sasa necessary kwa sababu kwa kawaida ni kama permanent secretaries wanafanya reaction, professional job kwa ministry, na labda tuki ondoa mmoja kama permanent secretaries, tuwe na minister, na deputy, labda tutaokoa watu wengi na nitakata kazi ya kutaka salaries saa zile unataka kazi ifanyike katika idara.

Na labda ungenifafanulia upande wa village council, village councils kama wangeza kuwa na administrator, na itakuwa ni nani na pia labda ingewezekana tuwe na continues ya DC, ziwe, zipewe uko. Asanteni.

**Mr. Jonathan:** Kwa majina yangu ninaitwa Johnathan Kiptum mimi niko na swali moja tu. Kwa ukweli nasikia wanasema police wana Linda raia lakini mimi nasema police wa siku hizi hawalindi raia, anaumiza raia. Na ningependa itengenezwa sheria vile raia anaweza kuhepa. Kwa maana hata saa hizi, ukitaka kushitaki police, hakuna vyenye unaenda kushitaki police kwa nini. Wakati atasema hivi, kuna siku moja angetumia petroli ya gari yangu, police wakakuja usiku, wakashika kijana, basi wakaambia kijana toa kitu kidogo, kinaja hana kitu kitu. Kijana hana kitu, anapeleka kijana mpaka police station. Asubuhi ingine kuingia kijana anapelekwa mpaka kortini ana andikiwa chang’aa, kweli, police bado wanafanya kazi kwa raia? Hapa ningeomba madam Commissioner, watafute sheria yenye raia atashitaki police mahali. Asante, sina swali lingine.

**Speaker:**……………………(Inaudible) wakati huu, Tume ndio ilitengeneza report za daily nafu, za constituencies, lakini sasa tunapatiwa tu moja, sijui kama ni kwe;o ni namna gani, kwa sababu ningetaka kujuwa watu wa Eldoret walikuwa wakisema nini.

**Com. Salome Waigai:** Asante sana kwa hayo maswal kwa wole watu waliuliza. Kwa hivyoi kuuliza maswali kweli inaweza kuwa. Watu wenye wamelelewa kidogo, kwanza ningetaka kusema vile nimesema ndio, nilieleza kuwa, hakuna short cut, lazima watu wasome Katiba kabisa. Pia maswali yenye nimeulizwa bado inahusu Katiba. Watu wamenaniuliza maswali kulingana na ile mambo nilisema, ni vile walisikia mimi nikisema, lakini mimi nilikuwa nafuata hizo introductions peke yake. Na kama sikukupatia introduction kwa vile, tumekuja hapa na Bwana Juma, na Bwana Juma ni amemaliza masomo ya wakili, na ni programme officer. Sasa ukichukulia hiyo ndio mambo yote ya Juma, mtu mwingine anaanza kuniuliza lakini Juma, ni kusema ni

mjaluo amepata baba na mama wenu kweli kutueleza? Mtu yeyote akizaliwa na baba na mama ni kukuwa tu, ile yenye nilifanya kwanza, introduction, mwenye kusikia amesha nijuwa mengi zaidi, anakuja anakuuliza, ana kuuliza *jaduong' ika kanye?* Hiyo ni jambo yenye ile. Kwa hivyo hata yale mambo nimesema tafadhali angalia Katiba yenyewe, anglia mambo gani yenye bado mnatashwishi nayo, badala, baada ya kusoma, siyo badala ya kusoma. Joseph nilikuwa nimejibu yake, Beatrice, ………(Inaudible) Ama tutaendelea kuwa na nyinyi mpaka sisi wenyewe. Tumechaguwa watumishi wa namna gani wa kike? Mkiwa namna gani wa kike. Ikiwa mtachaguwa watu wenye hata zile zenu, kwanza wakuwa na ma, na interest, the first loyalty kwa akina mama.

Ya pili, akiwa mtu wa articulate kwa kuelewa mambo upesi upesi na kuweza kujieleza.

Ya tatu, akuwa mtu mwenye anaweza kunegotiate na watu wengine, ili si wewe peke yake, lakini aweze kumu-influence na Tororei na ile delegate mwingine, ni nani? Julius, na Julius atakuwa ……….(Inaudible). Kwa hivyo ni mambo, na mtu mwenye atatakiwa kuweza kuwa in the democracia, kwani hii, itakuwa ni kazi ngumu.

Pia, you must deal with your delegate kama hawajaondoka kama akina mama. Mueleze akija kutoka Nairobi, tu lakin inarudi, tatumwaambi mama wa kamba atupikie chakula wiki nzima. We will have to talk with our delegates to ensure that adhabu ya akina mama, ndio yanabaki, na kama vile unaniona kwa huu mkutano, ………(Inaudible) so, we need to choose all everything. Find out who is praying for our church also, talk with them. Wengi wa wakina mama mna kazi nzuri sana hii haijamaliza, unless of good faith siyo akina mama peke yao. Huwezi kusema unataka justice, lakini uweseme unataka justice yako peke yako. Justice haiweze kuwa ya mtu, justice ni ya ni ya jamii. Kwani leo kutetea matako yako peke yako, kesho mtoto wako atakuwa kwa ile shida. Lazima, tumesema hii Katiba tumefanya, imetupatia sisi na tumepatia akina nani? Vizazi vijavyo.$$$$$$$$$$$$$$$$$$$$$$$$4 ***End of tape 3 side B***

Wasike na vya Kirumbe. We keep on saying we Kenyans are to keep on hearing somebody saying na mashamba yetu watakuja kuchukua, yeye ni nani? sema wote bado hatuelewi kuwa wote ni akina mama na akina baba na watoto wetu si hivyo, watoto wetu pia wakike na wakiume. Ah Rotich had a question on the that of the commissional line. No we don't want

something like the like of question that we have. This national commission on land is on 237 could you please look at your 237 and look at the different between them. The person from the national land commission has two:-

1. Whole title public land in entrap for you by the people of Kenya, administer public land on behalf of the public and local authority defined and keep constently at the review the national land policy. Watu sio kukubaliana tena moja halafu kurudia sheria ya miaka tano, nikuelezea we can kagua muda kwa muda.
2. Consolidate and protect value views all those relating to land, kwa hivyo tunataka mambo yasipoendelea kuangaliwa mara kwa mara.

Expense residual land administration faction on behalf of local authorities and performs such other functions as had been entrusted to each by the law. Parliament shall enact a law to define the organization and power of the commission, so we still have time to lobby our Parliamentarian to come up with the laws that will meet our daily. You are, you get that, sio kuishi ukitupiwa Katiba tu lakini pia tuna nafasi ya kuchangia swala vile vitaenda kutekeleswa na Wanabunge ili wafanye sheria zenye zita saidia sisi.

Citizenship: kwa nini kila mtu anakubali kuwa wanawake wanasajilliwa likini sio wanaume?

**Speaker:** Hapo kuna shida?

**Com. Salome Muigai:** Kwa mpango wa kuoana na kuolewa, watu wanadanganyika zaidi?

**Speaker:** ...(?) yeyote anawedanganywa

**Com. Salome Muigai:** Yeyote wanaenda kufanya nini? Anawezadanganyua. Kwa hivyo sijui kwa nini hapa tunaona hati akina wanawake ndio watadanganyika zaidi na akina baba hawako hatarini, ikiwa ni hatari ya kibiashara, tunahitaji kuangalia pande zote mbili tena vile Jackline amesema kuwa tuangalie, ikiwa tukiangalia tukiona muda wa miaka mitatu ni mifupi sana, tunaweza kuongeza lakini tutaongeza kwa nani?

**Speaker:** Wote.

**Com. Salome Muigai:** Wote ni kina nani?

**Speaker:** Wake kwa waume.

**Com. Salome Muigai:** Wake kwa:

**Speaker:** Kwa waume.

**Com. Salome Muigai:** Waume. Sasa kuhusu habari ya Rais ya kupeana degree, moja ya kati zeny tumepatia Rais kwa Katiba mpya si ya kupeana degree. Hiyo imeondolewa kuwa watu wakipata degree iwe kati ya nani? Ya wasomi wenye kuelewa na haja gani na anafanya kazi gani. Rais wetu awe kazi yake ni kututawala sisi.

Agricultural sector: pengine Katiba haikujikuta inauwezo wa kufanya mambo ya kutosho kwenye agricultural sector na ndio nasema hivi, kila Wilaya iwe nafasi ya kutengeneza sheria zake zenye zinawezesha watu wake kusalisha amani kwa urahisi. Kwa hivyo Washingishu itategemea iwe nyingi yake ni …………..(?) za ukulima kwani ni Wilaya ya ukulima. Tukienda Nyanza ziara zake hatuwezi kukupambanisha chanzo kuwa ni ya wakilimo huenda zikawa za nini?

**Speaker:** Samaki.

**Com. Salome Muigai:** …………..(?) wa samaki, huiwazi wa samaki na mambo mengi yanahusu? Habari ya samaki na habari ya maji. Kwa hivyo hiyo habari tumerudisha kwa Wilaya ndio kila Wilaya iweze kuangazia maslahi ya watu wake pale mashinani.

…………………(?) tafadhali kusoma hi Katiba utaona kuwa kila jumba kinachoingiwa na watu wa public, watu wa nini? Ninapoingiliwa na uma lazima liwezeshe mtu kwenye ulemavu kuingia na kuna nafasi ya miaka karibu mbili hivi, baada hiyo unaweza kushtakiwa kabla kama hujarekebisha vitu zenye unatakiwa kurekebishwa kuna muda kwenye kumepeanua.

**Speaker:** ………………………………………..(Inaudible).

**Com. Salome Muigai:** Na tulipoambiwa msiingilie hili jumba nyuma, kwa sababu nataka kuingilia pahali kila mtu anaingilia, I don't want to be told shungusha gari uende uingilie kule nyuma. No, ikiwa kuna watu wanaingilia mbele kila mtu aweze kuingilia wapi? Mbele, ikiwa kuna nyuma naye akuwe na choice na pahali yenye anachagua, kwanza yeye mwenyewe ndio atakuwa kutembea kwake ni shida, ndio mnamwambia shunguka hukoo mpaka afike kule hata kama kunanyesha. Kwa hivyo lazima tuangalia maslahi ya watu wenye ulemavu.

Orango Achoki anatuambia habari ya korti and severighty tumesema kwa Katiba mpya Kenya itahitaji kuwa sovereign mtu asome kuwa kesi kazima zifanywe kwa njia ya wenzetu, wala si hivyo kuelezwe kuna shida gani? Sio kesi kukaa kwa korti kwa muda mrefu zaidi.

Habari ya wazee kuwa na kitu kama NSSF maslahi ya wazee watangaliwa mwenye hajiwezi, gosh sorry mwenye hajiwezi anatakiwa kuangaliwa na Serikali.

Tumeambiwa kuwa tukipatia uraia kwa, bibi akikubalishwa kupatia uraia bwana wake, siku ile wataachana bwana afanye nini? Arudi kwao, na bibi je?

**Speaker:** Akae.

**Com. Salome Muigai:** Akae?

**Speaker:** …………………….(?)

**Com. Salome Muigai:** Eh, sasa bibi anakaa aje na bwana wa mtu anaenda?

**Speaker:** …………………………………………(Inaudible).

**Com. Salome Muigai:** Na si tumesema kuna haki? Kuna haki wa kila mtu, kwa hivyo sasa tunakubaliana kuna haki halafu tunarudi kuuliza swali lingine nyuma. Lakini hata hilo jambo kubwa yenye sijui kama kwa uraia tumeshika, ni kuwa mimi ikiwa sina haki ya kuwa raia ama kupeana urahia, sasa watoto wangu hawana haki ya urai Wakenya? Do you get the relationship? Kuwa ikiwa mwanamka hawezi kumpatia mtu mwingine raia ni kusema hata watoto wenye watazaa watakuwa bila urai wote nchi hii. Mmh pardon?

**Speaker:** ……………………………………………..(Inaudible).

**Com. Salome Muigai:** True, lakini ikiwa mtoto amezaliwa Kenya na mtu mwenye sio Mkenya, kuna matakwa fulani, sio watu wote even in that love. Lakini mimi siwezi shinda, nina shida kubwa sana kuwa mtoto wa ndugu yako ni Mkenya na wako sio Mkenya, hata kwa kibiologia zinawaelezea kuwa kuna uhaki wa kuwa mtoto wangu ni mtoto wa Kenya kuliko… si ni kweli? Eh, scientifically yaa, my child is more Kenyan until further notice ile ingine, na sitaki kwenda step moja ama kumi ndio tuhakikishe ile ingine ni nini? Ni Mkenya. So we need to be careful about that, the man was walikuwa kitambo uwe Mfalme, lazima uwe umezaliwa na msichana wa Mmisri, sio mwanamume, ndio wahakikishe kuwa wewe kabisa ni damu ya nini? Ya Kifalme hawangehakikisha ukiwa ni kweli wewe ni mtoto wa Mfalme, lazima uwe mtoto wa Zakia ama dadake nani? Mfalme, haungempata Mfalme ukiwe wewe ni mtoto wa mwanaume Mmsiri.

Lets go back to the district lakini hii tunasungumzia habari ya sheria, haki, right before the law, equality before the law, usawa mbele ya nini? Ya sheria, ukisema wanawake na wanaume wanahaki sawa lazima wakuwe na jukumu sawa na lazima wawezeswe kupatiana uraia. Aha, amesema kuwa ukijiandikisha kama raia lazima mfanye. Lakini nina swali moja, tunakubaliana na haki za watoto? Hiyo tuna shida nazo? Sasa mtoto wangu na wa Michael wanahaki moja ya kuwa

Wakenya? Basi itakuwa aje watoto wana haki lakini mimi sina? Watoto hao watakuwa wakiume na wakike ama wanakuwa na haki wakiwa watoto lakini wakikua kidogo watapunguza haki zake. Mtoto ana haki? Huyo mtoto anahaki zake? Ndio mumesikia nikisema habari ya mtoto huyo mpya? La, wote wana nini? Ana haki zake na ninajitambua, kwanza mlikuwa mnasema watoto wana haki, mtarudi kutengana pande gani unakuwa yule mwanamke hana haki na huyu ni kijana, sisi sote mimi na my brother ni watoto wa Muigai Si ndio sasa haki zake ……………(?) zinakuwa aje kubwa kuliko zangu je?

**Speaker:** Hapo kwamba Commissioner kitu gani kinafanya msichana anatoka kwao kwenda kwa bwana anatoka kwao na bwana hawezi enda kwa msichana

**Com. Salome Muigai:** Ni kweli tumeharibu sheria za Mungu, Mungu alisema mwanaume ataacha babake na mama yake aende wapi?

**Speaker:** …………………………………………(?)

**Com. Salome Muigai:** Aende wapi?

**Speaker:** ……………………………………(?).

**Com. Salome Muigai:** Kwa mkewe, kwanini tunaharibu sheria za Mungu, na sasa tunazirudisha hivyo. Ama kweli inasema aje?

**Speaker:** Mama hana………………………………………………………………..(?)

**Com. Salome Muigai:** What does the Bible say?

**Speaker:** ………………………………….(?).

**Com. Salome Muigai:** Bibilia inasema aje?

**Speaker:** Bibilia inasema ya kwamba, mume ndio inaacha bibi.

**Com. Salome Muigai:** Bibilia inasema aje juu ya nani mwenye atatoka kwao?

**Speaker:** ……………………………..(?) mwanamke.

**Com. Salome Muigai:** Huyu mwenye anajua Bibilia ndio nataka.

**Speaker:** ………………………………(?)

**Com. Salome Muigai:** It is okay, nimchagua huyu bado sijakutambua mtoto wangu.

**Speaker:** Bibilia inasema ya kwamba wote wawili wataandamana wanaenda kukaa pamoja.

**Com. Salome Muigai:** Hivyo ndivyo Bibilia inasema ama ndio ungetaka iseme?

**Speaker:** …………….. (?) bwana inawacha….

**Interjection Com. Salome Muigai:** Nani ni Mhubiri hapa? Wapi mwenye alituombea? Wewe ni Mhubiri? Lakini Bibilia imesema aje?

**Speaker:** Mimi nataka kufahamisha hawa.

**Com. Salome Muigai:** Mimi nauliza swali moja, Bibilia inasema aje?

**Speaker:** Bibilia tangu mwanzo mume na mke, mume angeletewa mke, mwanamume.

**Com. Salome Muigai:** Lakini mimi nataka kujua …..

**Interjection Speaker:** ………………………………………(Inaudible).

**Com. Salome Muigai:** Mimi nina swali moja, nani anajua mwenye anajua vile Bibilia inasema juu ya kuo.

**Speaker:** Bwana atawacha wazazi……..(?).

**Com. Salome Muigai:** Hebu Mzee.

**Speaker:** Bwana ………..(?).

**Com. Salome Muigai:** Hebu Mzee huyu wakwanza ndio ……….(?) huyu Mzee wakwanza ………………..(?) huyu mzee wa hapa mbele.

**Speaker:** Bwana atawacha, kuwacha baba babu wake na kushikana na mkewe wanakuwa mtu moja, ni bwana ndio

atawacha.

**Com. Salome Muigai:** Bibilia inasema a man will leave his father and mother and will live with his wife and the two shall become one.

**Speaker:** Where? Where?

**Com. Salome Muigai:** In the Bible.

**Audience:** Murmuring from the audience. Wanaenda kukaa wapi?

**Com. Salome Muigai:** Wataenda kukaa wapi?

**Audience:** Yaa.

**Com. Salome Muigai:** Mnaniuliza vile Bibilia imesema wataenda kukaa?

**Audience:** Yaa.

**Com. Salome Muigai:** Mimi nakuambi vile Bibilia imesema na imesema usiongeze na usifanye nini?

**Audience:** ……………………………(Inaudible).

**Com. Salome Muigai:** Kwani ukifanya hivyo utafanywa nini?

**Audience:** ……………………………(Inaudible).

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo hatutaki kuongeza nitaachia hapo. Anyway wacha nimalize kuhusu maswali tafadhali kukiwa kuna watu wangetaka debate ya ziada tutakutana nje Pastor, nitakuwa nimefunga mkutano. Amesema kuwa mtu mwenye atajiandikisha kufanya polls kupiga kura atakubalishwa kupiga kura yeye kwa maoni.

Special seats za wanawake wanauliza ooh, wanawake tutawatoa wapi na hawajitokezi? Nilisikia kitu moja sijui alitupa hadithi moja akasema kuwa ukileta mtu mgeni nyumbani utafanya nini siku ya kwanza na ya pili? Ili asitoroke ama, hapa ni pahali ya mbugi. Pengine Wabukusu ndio wenye tulikuwa tunasungumza habari ya kuku. Tusungumze habari ya mbuzi ama mbuzi ama ng'ombe mgeni, tukimleta mgeni nyumbani, tunafanya nini siku ya kwanza na ya pili na ya tatu?

**Speaker:** ………………………..(?)

**Com. Salome Muigai:** Tuna?

**Speaker:** Tunamfunga.

**Com. Salome Muigai:** Tunamfunga. Akimaliza hapo mwezi, tunamfunga tukimfungulia atafanya nini?

**Speaker:** Amezoe.

**Com. Salome Muigai:** Amezoe. Sasa tukitaka kumfunza tena, hata tukimpiga aende huko mpaka pale atafanya nini jioni?

**Audience:** Atarudi.

**Com. Salome Muigai:** Atarudi kwa hivyo tumewafunga akina mama wakati mrefu, sasa tukiwafungulia hawajui wana uhuru bado. Tuwape nafasi kidogo ndio wazoe kuwa wana nini? Wana hii uhuru. They are in the target ukiwarecognize mimi naenda pole pole namtarget tuende pamoja, kuna mambo mawili tutafanya, haita enda pole pole ama mtakubalisha mimi kuenda nini? Mkitaka sote tufike kwa gate pamoja na nyinyi mnaweza kutembea mimi siwezi mimi nina michael. Kuna mambo mawili tunaweza kufanya. Mnaweza kutembea pole pole umakunikubalisha kufanya nini.

**Audience:** Utembee mbele.

**Com. Salome Muigai:** Mtembee mbele kwani mume mume you have recognize mumechagua kuwa mimi nimekuwa na haja fulani ya a special need eh, sivyo? Basi tumechagua akina mama wanaspecial need, kwa wakati mrefu hawakupata nafasi na hiyo affirmative action ni ya kusema wewe Salome tembea ukifika pale na sisi tutafuata. So this is affirmative action na ni haki, hata mkitaka tufike kwa gate na nyinyi mnasema hata tumeanza kila mtu na zake nyinyi mnaanza speed, nitawakuta tu kweli? Ikiwa mkutano wangu na mnaenda pale si lazima mningoje? Sasa baadaya kuningoja give people time, that is affirmative action, it is social agreed.

Schools for the disable tafadhali tanataka Katiba hii mpya ingependa sana sana watoto wenye ulemavu wasome pamoja na nani? Na watoto wenzao, mimi nilisome Township na wale marafiki tulikuwa nao Township bado ni marafiki wangu mpaka wa leo. Nilopoenda Kenya High School wale marafiki wenye tulisoma noa Kenya High School bado ni marafiki mpaka?

**Audience:** Leo.

**Com. Salome Muigai:** Mpaka leo, kwa ajili nilisoma na watu wale wengine. Kuwatenganisha watu utarudi kwa fursa kujiungana na watu tena, hiyo ni masomo mawili tofauti. Kwa hivyo ninakubali na ile msingumzaji mwenye amesema tuwape mashule, Achoki. Lakini mimi ningetaka kwenda la ziada tuseme tutengeneze shule zetu za kawaida ziweze kukubali na kuweza kusomewa na watoto wetu wote.

Edwin Baraza citizenship umesema tuongeze miaka ukuwe tano, tafadhali zungumzia delegate wa kutoka kwa Catholic Church, wana delegates wengi na nakubaliana na wewe kuwe tu ni miaka tano, miaka tano ya bwana wa kigeni na ya bibi wa kigeni.

Devolution cost: ikiwa tunataka Serikali kuja karibu na sisi, hakuna kitu yenye haina nini? Haina cost, kwa hivyo ni vile tu naweza fikiria we give our priority, ikiwa priority yetu basi lazima tuweke pesa zetu pahali priority yetu iko, kila kitu iko na cost. Ukitaka kumsomesha mtoto kuna cost wakati mwingine inaendelea mpaka unauza ng'ombe pia, sio kwamba hupendi ng' ombe, lakini ni kwamba unadhamana ya elimu yako zaidi na ya vile unadhamana ya ng'ombe. Kwa hivyo na sisi lazima kwa zile mapesa zetu tuko nazo tufikirie jambo ungetaka kufanya nalo? Na mambo gani kwetu ni priority? Ukiwa priority yetu tunakubali Serikali yetu ikija karibu na sisi, itatufaa zaidi, itatuwezesha zaidi kuzalisha kwa wenzetu basi lazima tuweke hizo pesa zenye zinatakiwa, pahali vitu zenye zitatusaidia sana.

Emmy anauliza, habari ya akina mama wa nne kwa kila province, Nairobi wawili, Nairobi ni wawili bila wale wane, kwa hivyo wamepatiwa akina mama wachache kuliko Province zile zingine.

Ministers wenye professional kama bado mtahitaji PSs, DO tunahitaji PSs, they are not professional PSs. Pahali tutakuja labo ya wataalam kwenye wizara, ni katika Director wa matibabu ni daktari, Director wa, anaitwaje Director?

**Speaker:** Mkurugenzi.

**Com. Salome Muigai:** Mkurugenzi ndio cheo chenye tunataka mataalam kwa kisasa. Kwa hivyo PS hawajakuwa wataalam

hata kidogo ni administrators PS ama Katibu Mkuu ni tawala. Village council vile tukavyoanzishwa hiyo iko kwa Katiba Emmy unaweza kufanyia mambo mengi lakini kusoma Katiba lazima kila mtu ajifanyie.

**Jonathan Kipchumba:** Jonathan Kipchumba anauliza habari ya police accountability, polisi nani mwenye atatutetea kwa polisi tumekuwa na cheo kingine kipya cha people protector, hiyo ni ombudman lakini sisi tutaendelea na ombudman na tutaendelea. eh, kwa hivyo tumemweka jina mpya ya people's protector mlinda watu na task moja yake ni kusikiza malalamizi juu ya polisi na watawala wale wengine. Na pia Kenyans ask police service pia watakuwa na dates ya kuwasikiliza malalamishi ya wananchi.

Stephen, na pia tume ya righteous administration ya haki za wanadamu pia wanasiliza malalamishi juu ya polisi.

Na Stephen anauliza kama constituency reports zenye tuliagiza ziko, Stephen unauliza kwa desturi lakini pia nina ninakuambia ulija umechalewa kuwa tiari nilikuwa memesha onyeshana kuna report ya constituency report ya kutoka hapa kikao cha bunge cha Eldoret ya kusini.

Na kwa hao mengi sana na ningetaka kuwashukuru sana mabibi na mabwana kwa kuwa watulivu kwa siku nzima leo, ningetaka pia kuwaomba muendelee kusoma hii Katiba na mwendelee kusungumza na delegates wenu na kabla sijamaliza huu mkutano ningetaka kumpa the Borr atupatie introduction ya delegates wengine wetu wenye wamefika.

**Borr:** Asante sana Madam Commissioner. Kabla hatuja introduce our delegates ningependa kutoa matangazo kwa watu wa Eldoret South. Siku ya leo ilikuwa siku ya nyinyi kupewa hiyo constitution reports na draft za bill by the commission, represented by Commissioner Salome Muigai kwa hivyo nafikiri mumepokea we hope mtaenda naye kujadiliana naye mko na akili za draft bill.

Sasa vile tumefanya katika district, tumepanga mkutano ya malocaseni ili watu wetu wengi waweze kujadiliana juu ya hiyo draft bill na waweze kuongea na wale delegates watatu kufanya lobbing na kuwapatia maneno ambao ya kupeleka Nairobi, kwani

hao delegates wanakwenda Nairobi na nafikiri wataanza mkuno wa Nairobi wa National Confrence tarehe ishirini na nane. Kwa hivyo Eldoret South kuna mikutano minne kwa sasa, tarehe 28 jumatatu ijayo watu wa location ya Kapseret Fimat, Pioneer, na Ngeria watakutana hapa kuanzia saa tatu asubuhi ili kujadiliana kwanza kujadiliana na kupanda mipango ya kujadiliana kule mashinani tarehe 21 juna tatu. Na wataongozwa na committee Member Beatrice Kimotwo na Beatrice Charono na Mika Rono. Watu wa Membo location Cheptiret, Kipchogo na Kapkoet watakutan tarehe 22 Chebetoma Catholic Church cheptiret na wataongozwa na committee members bwana Stanley Mutai na na Pastor Stephen Choge.

Tarehe 22 vile vile watu wa Kepet location Susha, Kaptulwet watakutana Murgor Primary School wakiongozwa na bwana Patrick Rotich na Jared Mvanu.

Tarehe 24 halhamisi wiki ijayo wato wa Timboroa location ………..(?) Tarakwa watakutana Koiwo Primary School Kondoo, watakuwa chini wa bwana Samwel Bitok na Robert Kiage. Na natumaini kwamba watu wakitaka location watapanga mipango ya mkutono ya kule vijijini ili watu waweze kupata kujadiliana juu ya hiyo draft bill na waweze kutoa recommendations ambao zitakwenda kwa National Confrence.

Basi nachukua nafasi sasa ya kuintroduce delegates ambaye watafika nyuma, ambaye pia alichaguliwa na county councils kuwakilisha district na pia hasa kuwakilisha akina mama, Bi Emily ukiwa tafadhali njoo mbele, usalimie Commissioner, usalimie wananchi, na uwaeleze vile pia Commissioner taja anatahitaji haki yako muhimu na jinsi wakina mama wanahitaji sana kulobby kwako uende kupeleka hao mbele kusimamia maslahi yao katika National Conference.

**Bi. Emily:** Madam Commissioner na wageni wenye wamefika Eldoret South, ningependa kutoa pole zangu kwa sababu ya kuchelewa nilikuwa katika kazi ya kujitayarisha , unajua ni lazima utayarishwe huko nyumbani kabla hujaenda safari na umeskia itakuwa ni siku thelathini ikiwa ndefu. Sasa niliona ya kwamba ni lazima nijutayarishe ndio nikienda Nairobi nawakilisha kwa moyo moja sitakuwa nikifikiria huko nyumbani nimewacha namna gani.

Na sasa nataka kuwakilishia ya kwamba sisi tukiwa madelegates kutoka Wilaya ya Washingushu jukumu letu ni kubwa na pia

nyinyi mko na jukumu. Vile Madam Commissioner ametueleza ni nyinyi mtupe kazi, tumefikishwa kwa third draft ya Katiba na nyinyi ndio mlete hizo mapendekezo, mawazo zenu na ndio tukifika huko tuwe na kazi, tuwe na la kusema.

Na kwa hayo nataka tu kuwashukuru kwa kufika na nataka kusema muende nyumbani salama na tukutane kwa mikutano eh. Asanteni.

***Clapping of hands.***

**Borr:** Asante sana Emmy, ningependa kusema kuhusu yeye itakuwa vizuri watu waelewe yeye ni nani. Yeye ni Mwalimu Katiba University ya Moi University na anafundisha kwa department ya Education. Anafundisha Waalimu wale wanafundisha Secondary, kwa hivyo nafikiri councilors walichagua mtu ambaye ataweza kwenda kusoma, akisoma na kuweza kuandika reporti ya kutosha. Vile vile delegate wenzake bwana Cheserem simama yeye pia ni mwalimu na alikuwa education officer a retire sasa, lakini yeye ni mwenyekiti ya chama cha Waalimu katika kagu 'saving and credit' katika Washingushu district, kwa hivyo ni mtu ambaye amefikia …………….(?). Makofi kwake, ***clapping of hands***. Delegates.

**Sitiene:** Mr. Borr ningetaka ya kwamba delegates ya kwamba kwa sababu tumeambiwa mungeitaji mawazo zenu na vile mnataka maoni zetu kwa hivyo nitakuwa nanyi kwa mkutano ambayo mumetangaza hapa.

**Borr:** Watatuhudhuri mikutano ambayo tumetangaza na mtapata hawa watakuweko katika mikutano moja halafu tutawapatia maoni yenu. Delegate mwingine ambaye alifika hapa lakini ilibidi aondoke wakati tulikuwa tukiendelea na Madam Commissioner, ni bwana Moses Keter yeye ni councilor kutoka (Mawalibi) amewahi kuwa chairman na yeye pia ni mkulima infact aliomba apology kwa sababu anavuna ngano anataka amalize ili wakati atakuwa kwa Conference hatakuwa anafikiria upande wa shamba lake na ngano vile iko. Kwa hivyo yeye ametuma apology.

Na mwingine tulikuwa na bwana Tororei, mumemuona? Samuel Tororei alikuwa lakini saa hii na ni mtu wainne kutoka Washingishu. Mwingine wa tano ni Hellen yego, nafikiri wewe ndio uko na fahamu ya Hellen yego ambaya anafanya kasi

katika Development Office ya County Council. Yeye pia atakuwa delegates ambaye anaakikisha civic society lakini atawakilisha.

Basi kwa sababu tunaelekeaa mwisho ningependa kutangawa kwamba tukimaliza committee members pamoja na delegates watabaki nyuma ili tufanye mkuto ya mwisho ya kupanga hizi mikutano.

Napewa shukrani kwa wote ambao mumefika na nawatuma muweze kupeleka ujumbe wa huo zile mikutano imetangazwa kwa watu kule nyumbani iliwahudhurie na waweze kujadiliana mengi kuhusu hiyo draft ya Katiba, kwa sababu vile tumeelezwa ni draft sio mwisho na maoni mengi bado yatajika kutoka kwa wananchi. Asanteni, Madam Commissioner.

**Com. Salome Muigai:** Nina chukua wakati huo tena ni kuambia watu asante na muende salama na Mungu awabariki.

**Borr:** Tunataka mtu mmoja kutoa maombi ya mwisho, bwana William Ray. Maombi ya kufanya mkutano. Ama kwa sababu ya equality mama ilifunguliwa na mwanamke. Basi mama ajitolee, tunapatia nafasi wakina mama, hatuwaoni, Hellen.

**Prayer by Hellen:** Basi tuombe. Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Mungu Baba Mwenyezi tunakushukuru kwa siku huu umetuongoza umekuwa nasi mpaka saa hii. Tunakuomba utuongoze mpaka tutakapo rudi nyumbani uwe nasi. Tunaomba hayo kwa jina la Yesu Kristo Bwana wetu. Amen.

**Com. Salome Muigai:** Asanteni.

**Borr:** Wale ambao watabaki pia ni wale wa Civic Education, watu wa 3Cs mbaki na sisi.

Meeting ended at 4.30 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**